ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID - SPIKA

1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake

12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais
19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za

		SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake
28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil	-	Uteuzi wa Rais
33. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
34. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
35. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
36. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
37. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
38. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
39. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
40. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
41. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
42. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
43. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
44. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo

45. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
47. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
48. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
49. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
50. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
51. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
52. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
53. Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
54. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
55. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
56. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
57. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
58. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
59. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
61. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
62. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
64. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
65. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
66. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
67. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
68. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
69. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
70. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
72. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
73. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
75. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
76. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
77. Mhe. Sira Ubwa Mamboya - Uteuzi wa Rais
78. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
79. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake
80. Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Ussi Yahya Haji - Jimbo la Mkwajuni
82. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Jimbo la Fuoni
85. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Nafasi za Wanawake
86. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Kumi na Saba - Tarehe 31 Mei, 2017

(Kikao kilianza Saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti, (Shehe Hamad Mattar) alisoma Dua.

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, katika kikao cha Baraza cha tarehe 23 Mei, 2017, Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub aliuliza swali la nyongeza kwa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko na kuahidiwa kujibiwa kwa maandishi.

Katika kutimiza masharti ya Kanuni ya 40(4) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2016, Wizara hiyo imeleta majibu kama Wizara hiyo alivyoahidi.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, sasa namuomba Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko asome jibu la swali la nyongeza aliloulizwa na Mheshimiwa mjumbe huyo. Mhe Waziri karibu.

Mhe. wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, wakati najibu swali Namba 67 liliulizwa swali la nyongeza na Mhe. Jaku Hashim Ayoub aliyetaka kujua kuhusu kitengo cha ukaguzi kilichopo Dubai kinachofanya kazi za ukaguzi na ukusanyaji wa mapato, mkataba wa kitengo hicho ulitiwa saini lini na muda gani. Jibu la swali hili ni kama ifuatavyo Mhe. Mwenyekiti:-

Serikali iliingia na Mkataba na Kampuni ya Jabal Kilimanjaro *Auto ment* kwa magari yanayotoka Umoja wa Falme za Kiarabu UAE 25 Julai, 2016, Mkataba huo ni wa miezi 36 yaani miaka

mitatu, vile vile Kampuni *East Africa Auto ment Services Company Limited UAA* kwa magari yanayotoka Japan, Singapore, Hong Kong na UK kwa muda huo huo miezi 36. Ahsante.

HATI YA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani hati ya Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. Mhe. Mwenyekiti,. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa:(Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano): Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano naomba kuweka hati mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

HOJA YA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji Mwaka wa Fedha 2017/2018

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha katika Baraza lako Tukufu kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema na ukarimu, naomba kutoa Hoja kwamba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati, ili liweze kupokea, kuzingatia, kujadili na hatimae kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na

Usafirishaji kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia uhai na afya njema na kutuwezesha kushiriki katika kikao hiki cha Baraza la Wawakilishi kinachojadili Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza tena sana na kumshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa ushauri na muongozo mzuri ambao anaupatia mimi na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, ushauri na miongozo hiyo imeisaidia sana kuongeza ufanisi wa kazi na kasi ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, napenda pia kumshukuru Makamo wa Pili wa Rais, Mhe. Balozi mwezangu, Balozi Seif Ali Iddi, kwa kumsaidia na kumshauri Mhe. Rais kwa hekima katika kutekeleza majukumu mazito ya kitaifa. Aidha, naomba kumpongeza tena kwa dhati Makamo wa Pili wa Rais, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, kwa kuongoza na kusimamia vyema shughuli za Serikali katika Baraza lako Tukufu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, napenda pia kukupongeza wewe binafsi kwa hekima, umahiri na busara unazozitumia za kuliongoza Baraza lako Tukufu ambalo limekuwa likifanya maamuzi magumu na muhimu kwa manufaa ya nchi yetu. Aidha, pongezi zangu za dhati ziende kwa Mhe. Spika, Mhe. Naibu Spika kwa kazi nzuri anazozifanya za kusaidiana na wewe Mhe. Mwenyekiti,.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kutoa shukurani zangu za dhati kwa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano ya Baraza la Wawakilishi chini ya uongozi wa Mwenyekiti wake, Mhe. Hamza

Hassan Juma, Mwakilishi wa Jimbo la Shaurimoyo kwa maoni, ushauri na kazi nzuri ya uchambuzi wa kina wa taarifa za utekelezaji wa sekta katika mpango wa bajeti ya Wizara ambao umeisaidia sana Wizara katika kukamilisha maandalizi ya Bajeti tunayoiwasilisha leo. Aidha, naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wawakilishi wote kwa ushauri wao kwetu na tunawaomba muendelee kuwa karibu na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa lengo la kutushauri, kutukosoa na kutuelekeza na hatimae kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, Bajeti hii ambayo naiwasilisha mbele ya Baraza lako Tukufu leo imeandaliwa katika Mfumo wa Programu (PBB) kama Serikali ilivyoelekeza kwa kuzingatia utekelezaji wa Dira ya Zanzibar 2020, Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako ningependa tu kukuambia mapema na Baraza lako Tukufu mapema Hotuba hii itakuwa refu kidogo na sikutaka kuikatisha kwa sababu nilikuwa nategemea kwamba wananchi wanatusikiliza uko na wanataka kujua hasa tumepanga tufanye shughuli gani katika Wizara hii muhimu.

Mhe. Mwenyekiti, katika Mpango Mkuu wa Usafiri Zanzibar *(Zanzibar Transport Master Plan* 2009), Sera ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (2013), Sera ya Taifa ya Nyumba (2008), Sera mbali mbali za Taifa pamoja na Maagizo ya Serikali yanayotutaka kuzingatia ufanisi kwenye matumzi ya fedha za umma kwa kupunguza matumizi yasiyo ya lazima.

B. TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA KIPINDI CHA JULAI, 2016 – MACHI, 2017 KWA KUTUMIA MFUMO WA PROGRAMU

Mhe. Mwenyekiti, itakumbukwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kutekeleza Bajeti kwa kutumia Mfumo huu niliotaja yaani wa PBB, hivyo taarifa hii ya utekelezaji

ninayoiwasilisha imezingatia Programu za Wizara ambazo tuliziwasilisha katika Bajeti ya mwaka 2016/2017 kwa zile taasisi ambazo fedha zake ziliidhinishwa na Baraza la Wawakilishi – Zanzibar. Vile vile taarifa hii imejumuisha utekelezaji wa malengo mbali mbali ya Taasisi zinazojitegemea zilizo chini ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa kipindi hicho cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, kwa heshima naomba uniruhusu kuwasilisha Taarifa ya utekelezaji wa Programu Kuu nne (4) za Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017 kama ifuatavyo:-

B.1. PROGRAMU YA KWANZA: MIUNDOMBINU NA HUDUMA ZA USAFIRI WA BARABARA

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ina lengo la kuwepo kwa miundombinu bora na huduma za usafiri wa barabara zilizo bora, salama na endelevu. Matokeo yanayotarajiwa kupatikana katika programu hii ni uwepo wa miundombinu imara na huduma bora katika Sekta ya Usafirishaji wa Barabara.

Mhe. Mwenyekiti, Programu ya Miundombinu na Huduma za Usafiri wa Barabara inasimamia Programu ndogo mbili zifuatazo:-

(1a) Utunzaji na Matengenezo ya Barabara.
(1b) Usimamizi wa Usafiri wa Barabara.

B.1.1 Programu ndogo ya kwanza: Utunzaji na Matengenezo ya Barabara

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ndogo inasimamiwa na Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara (UUB) ambayo imepewa jukumu la

kujenga, kutunza na kuzifanyia matengenezo barabara zote Unguja na Pemba ili ziweze kutumika muda wote.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi 2017 Programu hii ndogo kupitia Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara (UUB), kazi iliyofanyika ni kukamilisha kilomita 23.4 za barabara kwa kiwango cha lami ikiwemo Barabara ya Mgagadu – Kiwani km 5.85, barabara ya Mwanakwerekwe – Fuoni kituo cha Polisi km 4, barabara ya Maktaba-Golf km 0.35, barabara ya Kwarara-Fuoni km 1, na barabara ya Kinazini (BOT)-Kariakoo km 0.6.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara ilikabidhiwa jukumu la ukamilishaji wa ujenzi wa barabara ya Jendele – Cheju- Unguja Ukuu yenye urefu wa kilomita 11.737 ambayo ujenzi wake ulianza kutekelezwa na Mkandarasi M/s DB Shapriya mnamo mwaka 2014/2015. Hadi kufikia Machi, 2017 jumla ya kilomita 11.660 za barabara hiyo zimekamilika kwa kiwango cha lami sawa na asilimia 99 ya kazi zilizokusudiwa. Aidha, kutokana na usanifu uliofanyika kwenye makutano ya barabara ya Unguja Ukuu (Kaebona), eneo linaloekewa lami limeongezeka urefu kwa kilomita 2 ambazo zinajumuisha mzunguko wa makutano ya barabara *(Round About)*, barabara pacha zinazoingia kwenye mzunguko na upandishaji wa lami kipande cha mita 400 kuelekea Bungi, kazi hizo zinaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Programu hii ndogo ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 1,244,538,000 kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2017 jumla ya TZS 1,011,379,436 zimetumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida na mishahara sawa na asilimia 81. Aidha, Wizara ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 8,690,000,000 kutoka Mfuko wa Barabara kwa ajili ya matengenezo ya barabara mbali mbali Unguja na Pemba na hadi kufikia Machi, 2017 jumla ya TZS 7,691,136,677 zimepatikana sawa na asilimia 89.

B.1.2 Programu ndogo ya Pili: Usimamizi wa Usafiri wa Barabara

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ndogo inasimamiwa na Idara ya Usafiri na Leseni ambayo imepewa jukumu la kusimamia usalama wa vyombo vya moto pamoja watumiaji wote wa Barabara, usimamizi wa mafunzo ya udereva, upasishaji madereva na walimu wao, kuendesha shughuli za ukaguzi wa vyombo vya moto pamoja na kusimamia utoaji wa huduma za usafirishaji abiria na mizigo kwa njia ya barabara. Aidha, jukumu jengine linalofanywa na programu hii ndogo ni kusimamia na kuendeleza Karakana Kuu ya Serikali iliopo Chumbuni na sehemu ya Mitambo Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 kazi zilizofanyika katika programu hii ndogo ni ukaguzi wa vyombo vya moto vya aina mbali mbali vipatavyo 28,675 Unguja na Pemba ili kuhakikisha kuwa viko katika hali ya uzima na salama. Aidha, jumla ya madereva wanafunzi 8,832 wamefanyiwa majaribio kwa Unguja na Pemba kati ya hao jumla ya wanafunzi 7,287 wamefalu na wanafunzi 1,545 hawakufaulu. Vile vile, jumla ya ruhusa za njia na usafirishaji 2,682 kwa gari za biashara za aina mbali mbali Unguja na Pemba zimetolewa na kutoa leseni kwa madereva wanafunzi 16,057. Karakana Kuu ya Serikali ilioko Chumbuni na sehemu ya Mitambo ilioko Pemba imezifanyia matengenezo jumla ya gari 409 kati ya hizo 70 ni gari za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na 339 gari za watu binafsi. KIAMBATANISHO NAMBA 5 kinaelezea ushahidi huo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Programu hii ndogo imepangiwa kutumia jumla ya TZS 561,430,000 kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2017, jumla ya TZS 393,803,430 zimetumika ambazo ni sawa na asilimia 70 ya makadirio ya bajeti kwa kazi za kawaida.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Programu Kuu ya Miundombinu na Huduma za Usafiri wa Barabara ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 1,805,968,000 na hadi kufikia Machi, 2017 jumla ya TZS 1,405,182,866 zimetumika sawa na asilimia 78 ya makadirio ya bajeti.

B. 2 PROGRAMU YA PILI: UHIFADHI WA MJI MKONGWE NA UIMARISHAJI WA MAJENGO YA SERIKALI NA BINAFSI

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ina lengo la kuhakikisha kuwepo kwa majengo bora ya Serikali na upatikanaji wa makaazi bora kwa jamii. Matokeo yanayotarajiwa kupatikana katika programu hii ni upatikanaji wa makaazi bora kwa wananchi wote pamoja na kuhifadhi Mji Mkongwe Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Programu ya Uhifadhi wa Mji Mkongwe na Uimarishaji wa Majengo ya Serikali na Binafsi inasimamia Programu ndogo mbili ambazo ni:-

(2a) Ujenzi, Usimamizi na Maendeleo ya Makaazi
(2b) Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe.

B.2.1 Programu ndogo ya Kwanza: Ujenzi, Usimamizi na Maendeleo ya Makaazi

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ndogo inasimamiwa na Wakala wa Majengo Zanzibar pamoja na Shirika la Nyumba Zanzibar.

Wakala wa Majengo – Zanzibar

Mhe. Mwenyekiti, Wakala wa Majengo Zanzibar imepewa jukumu la kuwapatia makaazi bora na yenye hadhi Viongozi Wakuu wa Serikali pamoja na Watumishi wa Umma, kutoa ushauri wa kitaalamu kwa miradi ya ujenzi wa majengo,

kusimamia na kuyafanyia matengenezo majengo ya Serikali pamoja na kuhakikisha viwango vya ubora vinafuatwa katika ujenzi wa majengo ya Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017, Wakala imelifanyia matengenezo makubwa kwa gharama nafuu jengo la Ofisi ya gazeti la Zanzibar Leo liliopo Maisara. Aidha, Wakala imeweza kutoa ushauri elekezi kwa miradi mbali mbali ya Taasisi za Serikali ikiwemo ujenzi wa masoko na vyumba vya baridi (*cold rooms*) ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, ujenzi wa Soko la Kinyasini Unguja, ujenzi wa Soko la Kengeja na Tibirinzi Pemba, ujenzi wa Ofisi mpya ya *ZRB* - Kwale Pemba, ujenzi wa Uzio wa eneo la kufugia samaki - Beit-el-Raas Unguja, matengenezo ya Ofisi ya Utabiri wa Hali ya Hewa - Uwanja wa Ndege Unguja pamoja na ujenzi wa Ikulu ya Micheweni Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Programu hii ndogo imepangiwa kutumia jumla ya TZS 372,165,000 kwa ajili ya kazi za kawaida na hadi kufikia Machi, 2017 jumla ya TZS 331,465,950 zimetumika sawa na asilimia 89 ya makadirio ya bajeti.

Shirika la Nyumba Zanzibar

Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Nyumba Zanzibar limepewa jukumu la kusimamia na kuratibu masuala yote yanayohusiana na ujenzi, uuzaji na ukodishaji wa nyumba za kuishi na za biashara.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kipindi cha Julai, 2016 – Machi, 2017, nyumba 2 za Serikali zimefanyiwa matengenezo ambazo ni no 45B iliopo Mazizini na 390 Mtaa wa Gizenga Mji Mkongwe. Aidha, Shirika linaendelea kuzitambua na kuziorodhesha nyumba zote ambazo zipo chini ya Shirika ambapo katika kipindi hicho jumla ya nyumba 72 zimetambuliwa kwa Unguja na Pemba. Vile

vile, Shirika limezifanyia matengenezo madogo nyumba za maendeleo Madungu Pemba *block no 4* kwa kuondoa matope katika sehemu ya chini ya ardhi (*basement*) pamoja na kusafisha karo na kutengeneza mfumo wa maji machafu kwa kubadilisha mabomba pamoja na kujenga karo mbili katika Nyumba za Kwamchina.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Shirika (ambalo linajitegemea) lilikadiria kukusanya jumla TZS 3,003,359,811 na hadi kufikia Machi 2017 jumla ya TZS 1,058,297,360 zimekusanywa kutokana na kodi ya nyumba zake sawa na asilimia 45.8 ya makadirio. Aidha, kwa upande wa matumizi, Shirika limepanga kutumia jumla ya TZS 1,969,033,280 na hadi kufikia Machi 2017 jumla ya TZS 883,911,121 zimetumika sawa na asilimia 45.9.

Programu ndogo ya Pili: Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ndogo inasimamiwa na Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe, ambayo imepewa jukumu la kuuhifadhi na kuuendeleza Mji Mkongwe wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 kazi zilizofanyika katika Programu hii ndogo ni maandalizi ya ukarabati wa jengo la Darajani (*Chawl Building*) kwa hatua za kupata miongozo kutoka *UNESCO/ICOMOS*. Aidha, Mamlaka imetoa kibali kwa Mkandarasi kwa ajili ya kulifanyia matengenezo madogo madogo ili kulihami jengo hilo. Kwa upande wa *Darajani corridor*, Mtaalam wa usanifu wa eneo la Darajani (*Phills International*) aliwasilisha ramani zenye dhana tatu (*three concepts*) kwa Serikali, hata hivyo Wataalam wazalendo wametoa maoni yao ili zifanyiwe marekebisho yatakayoendana na hifadhi ya Mji Mkongwe. Hivi sasa

Wataalamu wetu wa ndani wametayarisha michoro mengine ambayo inaendelea kufanyiwa kazi na Serikali.
Mhe. Mwenyekiti, usimamizi wa mradi wa ujenzi wa ukuta wa ukingo wa Bahari wa Mizingani pamoja na barabara katika eneo hilo unaendelea na uko katika hatua za mwisho ambapo umefikia asilimia 80.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Jengo la Beit - el – Ajaib tayari *UNESCO/ICOMOS* wamesharidhia mapendekezo yaliowasilishwa juu ya ukarabati wa jengo hilo. Aidha, ukarabati wa jengo la Makumbusho ya Kasri la Wananchi *(People's Palace Museum)* sehemu ya upande wa Kusini-Magharibi uliofanywa na Mamlaka umekamilika, kumekuwa na khitilafu ndogo ndogo za kiufundi ambazo Mamlaka inazifanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka katika udhibiti wa maeneo ya wazi imefanya uhakiki wa maeneo 20 ya wazi pamoja na kufanya vikao na watumiaji 13 wa maeneo hayo juu ya namna ya kuweza kushirikiana katika kuyahifadhi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Programu hii ndogo imepangiwa kutumia jumla ya TZS 360,900,000 ikiwa ni fedha za Ruzuku ya mishahara na matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Machi, 2017 jumla ya TZS 277,128,400 zimetumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia 77.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Programu kuu ya Uhifadhi wa Mji Mkongwe na Uimarishaji wa Majengo ya Serikali na Binafsi ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 733,065,000 na hadi kufikia Machi, 2017 jumla ya TZS 608,594,350 zimetumika sawa na asilimia 83 ya makadirio ya bajeti.

PROGRAMU YA TATU: HUDUMA ZA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA)

Mhe. Mwenyekiti, lengo la programu hii ni kuhakikisha kuwepo kwa miundombinu na huduma za mawasiliano zilizo bora, salama na endelevu kwa jamii. Matokeo yanayotarajiwa kupatikana ni kuwepo kwa huduma bora na endelevu za *TEHAMA* ambazo zitachochea ukuaji wa pato la Taifa la Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Programu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano inasimamia programu ndogo moja ambayo ni:

(3a) Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Mawasiliano.

Programu ndogo ya kwanza: Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Mawasiliano

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ndogo inasimamiwa na Idara ya Mawasiliano ambayo imepewa jukumu la kusimamia huduma za mawasiliano pamoja na kuratibu uwekaji wa miundombinu ya mawasiliano.

Mhe. Mwenyekiti, Katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 kazi zilizofanyika katika programu hii ndogo ni kuanza maandalizi ya Sheria ya *TEHAMA* na tayari rasimu ya awali imekamilika. Kusimamia ujenzi wa vituo vya *TEHAMA* kwa jamii chini ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*Universal Communication Access Fund*). Vituo vinavojengwa katika Wilaya kumi za Zanzibar vinavyoonekana katika kiambatanisho namba 6**.** Aidha, Idara kupitia programu hii inaendelea kusimamia utekelezaji na uwekaji wa Miundombinu ya Mawasiliano ya mkonga katika taasisi sita (6) za Serikali pamoja na kupeleka mkonga katika vituo vya kurushia matangazo vya *ZBC*. Vile vile mafunzo ya kuunganisha mtandao wa mkonga (*Network Switch SR10)* yamefanyika pamoja na kuzisambaza switch hizo katika Ofisi za Wizara za Serikali zilizoko Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Programu hii ndogo imepangiwa kutumia jumla ya TZS 336,260,000 kwa ajili ya kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2017 jumla ya TZS 210,404,300 zimetumika sawa na asilimia 63 ya makadirio ya bajeti.

PROGRAMU YA NNE: MIPANGO NA UTAWALA KATIKA SEKTA YA UJENZI, USAFIRISHAJI NA MAWASILIANO

Mhe. Mwenyekiti, Progamu hii ina lengo la kuimarisha huduma za ofisi na usimamizi wa rasilimali watu. Matokeo yanayotarajiwa ni kuwepo mipango bora na usimamizi wa rasilimali watu.

Mhe. Mwenyekiti, Programu ya Mipango na Utawala ina programu ndogo tatu ambazo:-

(4a)Utawala na Uendeshaji**;**

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe sauti zenu zimekuwa juu. Endelea Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Programu ya Mipango na Utawala ina programu ndogo tatu ambazo:-

(4a)Utawala na Uendeshaji**;**
(4b)Mipango na Sera katika Sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirshaji;
(4c) Uratibu shughuli za Wizara Pemba

Programu ndogo ya kwanza: Utawala na Uendeshaji

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ndogo inasimamiwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi ambayo imepewa jukumu la kusimamia masuala ya utumishi na uendeshaji katika Wizara.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 kazi zilizofanyika katika programu hii ndogo ni kujenga uwezo wa wafanyakazi wapatao 75 kwa kuwapatia mafunzo mbali mbali ya muda mrefu na muda mfupi. kiambatanisho namba 3**.** Aidha mazingira mazuri ya kazi kwa watendaji yameimarishwa ikiwemo kuwapatia huduma za usafiri, matengenezo ya ofisi mbali mbali, kuimarisha vitendea kazi pamoja na stahiki zao.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa mwaka wa fedha 2016 /2017, programu hii ndogo imepangiwa kutumia jumla ya TZS 1,022,331,000 kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2017 jumla ya TZS 820,137,852 zimetumika sawa na asilimia 80.

Programu ndogo ya Pili: Mipango na Sera katika sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ndogo inasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ambayo imepewa jukumu la kupanga, kuratibu, kusimamia na kutathmini utekelezaji wa sera, mipango, tafiti pamoja na miradi ya maendeleo katika sekta ya Ujenzi, Makaazi, Mawasiliano na Usafirishaji.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 kazi zilizofanyika katika programu hii ndogo ni kuratibu na kusimamia miradi ya maendeleo, kukusanya takwimu mbali mbali sekta za Ujenzi, Makaazi, Mawasiliano na Usafirishaji pamoja na kufanya utafiti kuhusiana na huduma za usafiri wa nchi kavu. Aidha, mafunzo ya bajeti ya PBB kwa watendaji wa Wizara yametolewa.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa upande wa miradi ya maendeleo ambayo inasimamiwa na kuratibiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ni:-

i. Mradi wa Ujenzi wa barabara ya Ole – Kengeja

Mhe. Mwenyekiti, Mradi huu unajumuisha Ujenzi wa barabara kutoka Ole – Kengeja yenye urefu wa km 35. Hadi kufikia Machi 2017 jumla ya kilomita 11 zimekamilika kwa kuwekewa kifusi kuanzia Ole hadi Mfikiwa. Aidha, urefu wa km 6.9 zimewekewa kifusi tabaka la mwisho kutoka Ole hadi Vitongoji. Vile vile eneo la urefu wa km 5.3 kutoka Mfikiwa hadi Pujini limeshafanyiwa usafi. Kazi za ujenzi wa makalvati umefanyika kwa hatua tafauti. Kwa ujumla utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia 88 ya ujenzi wote.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa mwaka wa fedha 2016/2017 mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 5,483,737,000 na hadi kufikia Machi, 2017, Jumla ya TZS 2,205,987,074 zimetumika sawa na asilimia 40 ya makadirio ya bajeti. Kati ya fedha hizo jumla ya TZS 358,000,000 zimetoka Serikalini kwa ajili ya fidia na TZS 1,847,987,074.60 zimelipwa na washirika wa maendeleo hawa ni wafadhili wa (*Opec Fund for International Development*).

ii. Mradi wa Ujenzi wa barabara ya Bububu – Mahonda – Mkokotoni, Pale – Kiongele, Matemwe – Muyuni na Fuoni – Kombeni km 52

Mhe. Mwenyekiti, Kwa kipindi cha Julai 2016 – Machi 2017, hatua iliyofikiwa ni taratibu za kumpata Mkandarasi kwa njia ya zabuni na hivi sasa hatua ya tathmini inaendelea. Kwa upande wa Msimamizi wa mradi (*consultant*) tayari ameshapatikana na kwa njia ya zabuni, kinachofuata ni makubaliano ya mkataba wa kazi husika baina ya Wizara na Msimamizi huyo. Kadhalika, Wizara inaendelea kujenga uwezo kwa Wafanyakazi wake pamoja na

ulipaji wa fidia za Nyumba na Vipando kwa barabara ya Bububu, Mahonda hadi Mkokotoni (kupitia Kinyasini na Chaani) ambapo ndio masharti ya awali ya *AfDB* kabla ya kuanza kwa ujenzi wa mradi huu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 14,700,000,000 na hadi kufikia Machi 2017, Jumla ya TZS 2,447,113,843 zilipatikana sawa na asilimia 17 ya makadirio ya bajeti kutoka Serikalini kwa ajili ya malipo ya fidia za nyumba na vipando kwa barabara hiyo.

Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Chake Chake/Wete urefu wa kilomita 22

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2016 – Machi, 2017, hatua ya utekelezaji iliyofikiwa ya mradi huu ni kuendelea na majadiliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano (Tanzania) kupitia Wizara ya Fedha na Mipango na Mfuko wa Fedha kutoka Saudi Arabia (*Saudi Fund*) kuhusiana na taratibu za upatikanaji fedha. Kwa upande wa *BADEA* tayari taratibu zimeshakamilika za upatikanaji wa fedha hizo ambapo mkataba wa mkopo baina ya Wizara ya Fedha na Mipango ya SMT na *BADEA* ulitiwa saini mwaka 2012 mjini Arusha. Aidha, Wizara iko katika matayarisho ya kuanza kufanya tathmini ya nyumba, vipando na mkonga ambavyo vitaathirika wakati wa ujenzi wa barabara hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 6,380,000,000 na hadi kufikia Machi 2017 hakuna fedha iliyotumika kwa sababu hizo kazi hajijaanza.

iii. Ujenzi wa Jengo Jipya la Abiria katika kiwanja cha Ndege cha *AAKIA*

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na kutokamilika kwa mpango wa fedha za ziada za kuendelea na ujenzi wa jengo jipya la abiria kutoka kwa mfadhili (*Exim Bank ya China*) kumesababisha mradi huu kuendelea kusimama kwa muda licha ya kufikia asilimia 33 ya ujenzi wa jengo hilo. Hata hivyo, Serikali inafanya juhudi za makusudi kuhakikisha mradi huu unaendelea kwa mwaka wa fedha unaofuata. Kwa sasa mazungumzo baina ya Serikali na Mfadhili *Exim Bank* kupitia Serikali ya Jamhuri ya Muungano Tanzania inaendelea ambapo tunatarajia kupata ufumbuzi wa suala hili hivi karibuni.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 144,400,000,000 kati ya fedha hizo TZS 20,000,000,000 zilitengwa kutoka Serikalini. Hadi kufikia Machi 2017, Jumla ya TZS 1,622,186,096 zilitumika sawa na asilimia 8 ya makadirio ya bajeti kutoka Serikalini kwa ajili ya malipo ya Mshauri Elekezi (*Consultant*) *ADPI.* Kwa kipindi hicho hakuna fedha iliyopatikana kutoka kwa Mfadhili.

iv. Uimarishaji wa huduma za Viwanja wa Ndege vya Zanzibar (Unguja na Pemba)

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ina lengo la kuimarisha huduma za viwanja vya Ndege vya Zanzibar na hatua ya utekelezaji iliyofikiwa kwa sasa ni kutangazwa kwa Zabuni kwa ajili ya kumtafuta Mshauri Elekezi (*Consultant*) kwa kazi ya kufanya Upembuzi Yakinifu (*Feasibility Study*), kuandaa michoro na kutayarisha zabuni kwa kiwanja cha ndege cha Pemba, kuandaa Mpango Mkuu wa Viwanja vya ndege vya Zanzibar *AAKIA* na Pemba *Airport* (*Zanzibar Airport Master Plan*) na mpango wa matumizi ya ardhi kwa kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Unguja *AAKIA* (*Land Use Plan for AAKIA*). Jumla ya Kampuni 56 zilijitokeza kununua zabuni kwa ajili ya kufanya kazi hiyo, ambapo baada ya kuzipitia zabuni zote hizo, kampuni tatu ndizo

zilizobahatika kuendelea na hatua ya kufanyiwa tathmini ya kifedha yaani (*Financial Evaluation*).

Tayari Wizara imeshaiandikia Benki ya Maendeleo ya Afrika AfDB ambayo ndiyo inayofadhili mradi huu, kwa ajili ya kupata idhini yao *(no objection).*

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 600,000,000 na hadi kufikia Machi 2017 hakuna fedha iliyopatikana kutoka kwa Mfadhili.

Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri

Mhe. Mwenyekiti, Wizara kupitia Mkopo kutoka *Exim Bank* ya *China* inatarajia kujenga Bandari Mpya ya Mpigaduri kwa lengo la kuimarisha huduma za usafiri wa baharini. Majadiliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Fedha na Mipango ya SMT na *Exim Ban*k yanaendelea ambapo Rasimu ya Mkataba wa Mkopo *(Draft Framework Loan Agreement)* imeshawasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango Tanzania kwa kufanyiwa kazi. Aidha, tayari Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshatiliana saini Rasimu ya Mkataba wa ubia *(Shareholding Framework Agreement)* na kampuni ya *CHEC* kutoka China. Hadi sasa Kampuniya *CHEC* imeshakamilisha Ripoti ya Mazingira *(Environmental Impact Assessment),* na inaendelea kutayarisha michoro ya Ujenzi *(Preliminary Design)*, pamoja na kufanya uchunguzi wa udongo *(Geotechnical Investigation Report)* awamu ya kwanza. Hatua za kutafuta Mshauri Elekezi wa mradi huo pia zimeshaanza kufanyiwa kazi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali kupitia mradi huu ilipanga kutumia jumla ya TZS 400,000,000 na hadi kufikia Machi 2017 hakuna fedha iliyotumika.

Mradi wa Mabadiliko ya mfumo wa Taasisi

Mhe. Mwenyekiti, Wizara inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Mageuzi ya Taasisi zake ambapo tayari awamu ya tatu ya utekelezaji umeshaaza. Mradi huu ambao unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) una lengo la kuongeza tija na ufanisi wa Wizara kwa kutenganisha (a) sera na mipango, na (b) udhibiti, uendeshaji na usimamizi. Kwa upande mmoja Wizara inajikita katika kuandaa sera na mikakati ya Sekta za usafiri, mawasiliano na ujenzi, na kwa upande wa pili, udhibiti, uendeshaji na usimamizi wa sekta utafanywa na Mamlaka zitakazoundwa au kuimarishwa chini ya Wizara. Katika kutekeleza mageuzi hayo, tayari Mamlaka mbili zimeshaanzishwa Mamlaka ya Usafiri Baharini (ZMA) na Mamlaka ya Viwanja Vya Ndege Zanzibar (ZAA). Hatua za mageuzi kwa Idara ya Usafiri na Leseni pamoja na kuifanya Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara (UUB) kuwa Wakala wa Ujenzi wa barabara zinaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 4,000,000,000 kupitia AfDB, na hadi kufikia Machi 2017 jumla ya TZS 591,640,500 zimetumika sawa na asilimia 15 ya makadirio ya bajeti.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara imepangiwa kutumia jumla ya TZS 182,230,000,000 (kupitia kwa Wafadhili na mchango wa Serikali) na hadi kufikia Machi 2017 jumla ya TZS 6,866,927,513 zimetumika sawa na asilimia 4 ya makadirio ya bajeti.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Programu hii ndogo imepangiwa kutumia jumla ya TZS 968,666,000 kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2017 jumla ya TZS 594,189,300 zimetumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia 61.

B.4.3 Programu ndogo ya tatu: Kuratibu shughuli za Wizara Pemba

Mhe. Mwenyekiti, programu hii ndogo inasimamiwa na Ofisi Kuu – Pemba ambayo imepewa jukumu la uratibu wa kazi za Wizara kwa upande wa Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017, kazi zilizofanyika katika programu hii ndogo ni kuratibu na kusimamia shughuli zote za Wizara (Pemba) ikiwemo kazi za Utawala na Utumishi, Kazi za Mipango na Bajeti, Ujenzi wa Barabara, Huduma za Usafiri wa Barabara, Majengo pamoja na Huduma za TEHAMA.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, programu hii ndogo imepangiwa kutumia jumla ya TZS 1,457,810,000 kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2017 jumla ya TZS 999,341,100 zimetumika sawa na asilimia 69.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Programu kuu ya Mipango na Utawala katika sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 185,678,807,000 na hadi kufikia Machi, 2017 jumla ya TZS 9,280,595,765 zimetumika sawa na asilimia 5 ya makadirio ya bajeti.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Usafirishaji kupitia programu zake kuu nne ambazo ziliidhinishwa na Baraza lako Tukufu kwa mwaka wa fedha 2016/2017 zilipangiwa jumla ya TZS 188,554,100,000 kwa kazi za kawaida na maendeleo na hadi kufikia Machi 2017 jumla ya TZS 11,504,777,281 zimepatikana kwa kazi za kawaida na maendeleo sawa na asilimia 6. KIAMBATANISHO NAMBA 1 kinajieleza.

UKUSANYAJI WA MAPATO

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara ilipangiwa kukusanya jumla ya TZS 1,762,800,000 na hadi kufikia Machi 2017 jumla ya TZS 1,121,561,595 zimekusanywa sawa na asilimia 64 ya makadirio. KIAMBATANISHO NAMBA 1 kinahusika.

TAARIFA ZA UTEKELEZAJI KWA TAASISI NA MASHIRIKA YANAYOJITEGEMEA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar imeendelea na jukumu la kuvisimamia, kuviendesha, kuvitunza na kuviendeleza viwanja vya ndege vya Serikali. Katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017, Mamlaka imefanikiwa kuimarisha ulinzi na usalama wa Viwanja, kuanza utekelezaji wa mradi wa mfumo wa kuwatambua abiria, kuimarisha mfumo wa maegesho ya gari, kufanya utanuzi wa kumbi za abiria, kujenga kituo kipya cha zimamoto, utanuzi wa eneo la kusubiria abiria katika uwanja wa ndege wa Pemba, kuimarisha vituo vya biashara (Unguja na Pemba), kupatikana kwa gari 4 mpya za zimamoto, kufanya matengenezo ya taa za kuongozea ndege katika kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Abeid Amani Kurume na kazi hizo zimechangia kuongezeka kwa mashirika ya ndege mapya kama vile shirika la ndege la Tanzania, Malawi na Uturuki pamoja na Mamlaka kutoa mafunzo mbali mbali kwa wafanyakazi wa Viwanja vya ndege ili kuongeza ubora wa utoaji huduma na ufanisi wa kazi.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017, Mamlaka imehudumia jumla ya safari za ndege 55,399 ikilinganishwa na safari 51,710 zilizohudumiwa katika kipindi kama hicho cha mwaka 2015/2016 ikiwa ni ongezeko la asilimia

7.1. Kati ya safari hizo, safari za ndege 45,413 zilihudumiwa katika kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Abedi Amani Karume na safari za ndege 9,986 zilihudumiwa katika kiwanja cha Ndege cha Pemba. KIAMBATANISHO NAMBA 7 kinahusika.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, Mamlaka imehudumia abiria 911,734 ikilinganishwa na abiria 783,207 katika kipindi kama hicho mwaka 2015/2016 ikiwa ni ongezeko la asilimia 16.3. Abiria 833,186 walihudumiwa katika kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume na abiria 78,548 walihudumiwa katika kiwanja cha Ndege cha Pemba na abiria waliopita *(transit)* wamefikia 86,114, ambapo 77,939 walipita katika kiwanja cha ndege cha kimataifa cha Abeid Amani Karume na abiria 8,178 walipita katika kiwanja cha ndege cha Pemba. KIAMBATANISHO NAMBA 7 kinahusika.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa mizigo *(freight)* jumla ya Tani 1,400 zilihudumiwa katika viwanja vya Unguja na Pemba kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2017, ikilinganishwa na Tani 1,397 zilizohudumiwa katika kipindi cha Julai 2015 hadi Machi 2016.

Mapato na Matumizi

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ilipanga kukusanya jumla TZS 9,543,987,682 kutoka vianzio vyake mbali mbali na hadi kufikia Machi, 2017 jumla ya TZS 6,885,196,637.08 zimekusanywa sawa na asilimia 72.14 ya makadirio ya bajeti. Kwa upande wa matumizi Mamlaka ilipanga kutumia jumla ya TZS 9,790,780,648 kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo na hadi kufikia Machi, 2017 jumla ya TZS 6,866,642,128.37 zimetumika sawa na asilimia 70.13 ya makadirio ya bajeti.

C.2. SHIRIKA LA BANDARI LA ZANZIBAR

Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Bandari lina jukumu la kutoa huduma za uingizaji na utoaji meli katika Bandari za Unguja na Pemba, ufungaji na ufunguaji wa meli kwenye gati, uangalizi wa alama za kuongozea usalama wa meli (minara na maboya), uteremshaji na upakiaji wa bidhaa kwenye meli pamoja na vyombo vyengine vya usafiri wa baharini na usimamizi wa usalama wa usafiri ndani ya maeneo ya Bandari hizo.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai 2016 hadi Machi, 2017, Shirika limehudumia vyombo mbali mbali vya mizigo na abiria katika Bandari zake za Unguja na Pemba. Jumla ya meli za Kigeni 98 zenye uzito wa GRT 1,565,798 na meli za ndani 2,681 pamoja na vyombo vya kienyeji 3,007 zimehudumiwa. KIAMBATANISHO 8 kinahusika. Shirika limehudumia jumla ya tani 177,722.47 za mzigo mchanganyiko na tani 80,844.72 za mzigo kwa majahazi pamoja na makontena 43,725 (TEUs 56,824). Vilevile, jumla ya abiria 1,882,178 wa ndani na nje wamehudumiwa. KIAMBATANISHO NAMBA 8 kinahusika.

Mhe. Mwenyekiti, Shirika limebadilisha Maboya ya *solar* sita (6) katika bandari ya Unguja na maboya 10 katika bandari za Pemba ambapo maboya mapya ya plastiki yametumika. Aidha, Shirika limeweza kuyafanyia matengenezo maboya manane (8) yasiokuwa na taa (bubu) na yenye taa katika bandari za Pemba na sita (6) katika bandari za Unguja.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa miradi ya Shirika, Shirika limefanikiwa kununua vifaa vya kufanyia kazi Bandarini kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa kuhudumia mizigo katika Bandari zetu. Hadi kufikia Machi 2017, Shirika limetumia jumla ya TZS 1,079,449,915.81 kwa kulipia vifaa hivyo (vikiwemo *Weigh bridge 1, Reach stacker 1, "Spreader" 4*) na kulipa bakaa la malipo ya vifaa *(Empty Handler 1)* ambapo vifaa hivyo vyote vimeshawasili nchini. Aidha, Shirika limefanikiwa kulipa mkopo wa ununuzi wa Tagi na ununuzi wa Kreni mbili ambapo jumla ya

TZS 3,770,575,637.42 zimetumika. Kwa upande wa mkopo wa ununuzi wa Tagi Shirika limefanikiwa kulipa awamu 32 kati ya awamu 60 za mkopo na kumaliza mkopo wa Kreni mbili.

Mhe. Mwenyekiti, Shirika limeendelea kuimarisha miundombinu yake kwa kufanya matengenezo ya Gati ya Wete, Ujenzi wa Ukuta wa Usalama Bandari ya Mkoani, matengenezo ya mnara wa Matumbini, uimarishaji wa Kituo cha Kigomasha, Uimarishaji wa Kituo cha Mkokotoni pamoja na ukarabati wa Karakana ya zana nzito. Hadi kufikia Machi, 2017, jumla ya TZS. 363,399,321.00 zimetumika kwa ajili ya kazi hizo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande uimarishaji wa Ulinzi na Usalama, Shirika limenunua mashine mbili za kukagulia mizigo na abiria. Hadi kufikia Machi, 2017, jumla ya TZS. 110,757,632.00 zimetumika ikiwa na sehemu ya gharama za ununuzi huo. Aidha, Shirika linaendelea na uimarishaji wa Kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT) na hadi kufikia Machi, 2017 limetumia jumla ya TZS 13,506,000.00 kwa kazi za utengenezaji wa mfumo wa mtandao wa usalama katika Bandari ya abiria pamoja na kupatikana kwa mkandarasi wa utayarishaji wa mfumo wa mawasiliano ya ndani *(LAN).*

Mapato na Matumizi

Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Bandari kwa mwaka wa fedha 2016/2017 lilipanga kukusanya jumla TZS 29,895,185,265.61 kutoka vianzio vyake mbali mbali na hadi kufikia Machi 2017 jumla ya TZS 20,979,844,866 zimekusanywa sawa na asilimia 70 ya makadirio ya bajeti. Kwa upande wa matumizi Shirika lilipanga kutumia jumla ya TZS 25,613,085,391 kwa kazi za kawaida na hadi Machi 2017 jumla ya TZS 14, 977,308,700 zimetumika sawa na asilimia 58.5 ya makadirio yote ya bajeti. Aidha Shirika limepanga kutumia TZS 10,921,155,759 kwa kazi

za maendeleo na hadi kufikia Machi 2017 jumla ya TZS 5,548,394,801 sawa na asilimia 51 ya makadirio zimetumika.

C.3. SHIRIKA LA MELI NA UWAKALA ZANZIBAR

Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Meli na Uwakala limepewa jukumu la kuendesha meli za serikali pamoja na kutoa huduma za Uwakala kwa meli za kigeni zinazoingia bandari za Zanzibar. Shirika ni moja kati ya taasisi muhimu katika utoaji wa huduma za usafiri wa baharini kati ya visiwa vya Unguja na Pemba na Mwambao wa Afrika Mashariki.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Shirika kupitia meli yake ya MV. Mapinduzi II limefanya safari za ndani 85 na safari 1 nchini Kenya kwa kipindi cha miezi tisa na kuhudumia jumla ya abiria 161,477 kwa safari za ndani na abiria watatu (3) kwa safari ya Kenya pamoja na kuhudumia tani 14,959 za mizigo ikiwemo magari na mizigo tofauti.

Vile vile, Shirika kupitia meli ya MV. Mapinduzi II lilifanya safari ya nchini Comoro katika kipindi cha mwezi wa Aprili, 2017 ikiwa na abiria 26 na tani 35 za mizigo kwa lengo la kukuza biashara na mahusiano baina ya Visiwa vya Zanzibar na Comoro. Kwa upande wa MV. Maendeleo jumla ya safari 17 zimefanyika na jumla ya abiria 6,828 na tani 5,724 za mizigo zimehudumiwa, kwa hivi sasa meli ya MV. Maendeleo imesita kufanya kazi kutokana na uchakavu, na mchakato wa kuiuza meli hiyo unaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa MT. Ukombozi, meli hii imeendelea kukodishwa kwa kampuni binafsi *ya GAPCO Zanzibar Ltd* kwa mkataba maalum na kwa kipindi chote hiki imeweza kubaki katika kodi isipokuwa mwezi mmoja tu ambapo meli ilipelekwa chelezoni nchini Kenya kwa ajili ya matengenezo.

Aidha, Shirika limepokea na kutoa huduma za uwakala kwa meli za kigeni zipatazo122.

Mapato na Matumizi

Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Meli na Uwakala kwa mwaka wa fedha 2016/2017 lilipanga kukusanya jumla TZS 12,926,187,580 kutoka vianzio vyake mbali mbali na hadi kufikia Machi, 2017 jumla ya TZS 8,512,254,158 zimekusanywa sawa na asilimia 66.3 ya makadirio ya bajeti. Kwa upande wa matumizi, Shirika lilipanga kutumia jumla ya TZS 11,946,808,362.32 kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi, 2017 jumla ya TZS 8,904,245,013.90 zimetumika sawa na asilimia 75 ya makadirio ya bajeti.

C.4 MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka hii ina jukumu la kusimamia usalama na ulinzi wa vyombo vya baharini pamoja na kusimamia shughuli za ukaguzi na usajili wa meli. Kwa kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 Mamlaka katika kuimarisha usalama na ulinzi wa vyombo vya baharini imeweza kuandaa vikao mbali mbali vya wadau wa sekta ya usafiri baharini ikiwemo vikao vya ushirikiano na *SUMATRA*, Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na Wilaya zote za Zanzibar na Wakuu wa Madiko mbali mbali Unguja na Pemba. Aidha, Mamlaka imefanya zoezi maalum Unguja na Pemba la ukaguzi wa upakiaji wa abiria kwa kiwango stahiki, udhibiti wa tiketi za magendo na utumiaji wa vitambulisho wakati wa ununuzi wa tiketi na uingiaji bandarini.

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ilisajili meli 4 zenye uzito wa jumla *GRT* 3,320 kwa usajili wa ndani (*Tanzania Zanzibar Registry*). Mamlaka kupitia wafanyakazi wa Mamlaka wailioko nchini Falme za Kiarabu (UAE) walisajili jumla ya meli 186 zenye uzito wa jumla *GRT* 439,312. Jumla ya mabaharia wa kigeni 601

wanaofanyakazi katika meli za kigeni zilizosajiliwa kupitia *TZIRS* wamethibitishwa vyeti vyao. KIAMBATANISHO NAMBA 9. Aidha, Mamlaka kwa kushirikiana na serikali, tayari imeshafanikisha usajili wa kampuni inayojulikana kwa jina la *Zanzibar Internationl Maritime Service Limited* nchini Falme za Kiarabu UAE na hivi sasa Kampuni hiyo imeshaanza kufanya kazi ya usajili wa meli za kimataifa kwa niaba ya Mamlaka.

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka iliendelea kutoa leseni za usajili kwa vyombo vidogo vidogo 132 pamoja na kutoa vitabu vya mabaharia (*Discharge Book*) 233 na vitambulisho vya kimataifa vya mabaharia 11, na vile vile kwa kipindi hiki Mamlaka ilitoa leseni 70 za manahodha na uhandisi (*Boat Master Licences & Boat Engineer licences*). Vilevile Mamlaka imeidhinisha mikataba 111 ya mabaharia wanaosafiri na meli za nje kupitia kampuni ya *DANAOS*.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi hicho, Mamlaka ilikagua meli 72 ambazo zenye *GRT* = 72,063. Aidha jumla ya vyombo vidogo vidogo 257 vyenye jumla ya *GRT* = 20,611 vilikaguliwa. Pia jumla ya leseni 63 zimetolewa kwa Makampuni na Taasisi mbali mbali zinazotoa huduma za usafiri baharini.

Mapato na Matumizi

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Usafiri Baharini kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ilipanga kukusanya jumla TZS 3,642,689,600 kutoka vianzio vyake mbali mbali na hadi kufikia Machi, 2017 jumla ya TZS 2,685,935,486 zimekusanywa sawa na asilimia 75 ya makadirio ya bajeti. Kwa upande wa matumizi Mamlaka ilipanga kutumia jumla ya TZS 3,492,378,460 kwa kazi za kawaida na hadi Machi, 2017 jumla ya TZS 2,440,849,240 zimetumika sawa na asilimia 70 ya makadirio ya bajeti ikiwemo gharama za kufungua Kampuni ya *TZIRS* huko UAE.

D. MASHIRIKIANO NA TAASISI ZA MUUNGANO

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji imeendelea kushirikiana na Taasisi za Muungano zilizopo hapa Zanzibar katika utoaji wa huduma na usimamizi wa Sekta ya Ujenzi, Makaazi, Mawasiliano na Uchukuzi. Miongoni mwa hizo ni Mamlaka ya Usafiri wa Anga ya Tanzania (*TCAA*), Mamlaka ya Hali ya Hewa ya Tanzania (*TMA*), Mamlaka ya Mawasiliano ya Tanzania (*TCRA*), Shirika la Posta la Tanzania (*TPC*), Shirika la Simu Tanzania (*TTCL*) na Mamlaka ya Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (*SUMATRA*). Mashirikiano na Taasisi hizo yamechangia sana kukuza Sekta ya Usafiri na Mawasiliano hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, wizara katika kuimarisha mahusiano mazuri na Wizara za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zinazosimamia sekta ya Ujenzi, Makaazi, Mawasiliano na Uchukuzi, tumefanya vikao vya mashirikiano na Wizara/Taasisi hizo kwa lengo la kubadilishana uzoefu utakaosaidia kuimarisha na kuweka mikakati bora katika kuboresha utoaji wa huduma katika sekta hizo.

E. MWELEKEO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI INAYOTUMIA MFUMO WA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo ya utekelezaji kwa kila programu zinazosimamiwa na wizara pamoja na kutoa maelezo ya utekelezaji wa Mashirika na Mamlaka zilizo chini ya wizara kwa kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017, sasa kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Bajeti inayotumia mfumo wa Programu kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kwa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

Mhe. Mwenyekiti, kufuatia muundo wa Wizara kwa sasa, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji imepewa jukumu la kusimamia Sekta ya Ujenzi, Makaazi, Mawasilino na Usafirishaji – Zanzibar. Hivyo, kwa kuzingatia muundo pamoja na sekta hizo, Wizara itakuwa na Programu Kuu nne (4) zifuatazo:-

Programu ya 1: Miundombinu ya Huduma za Usafirishaji.
Programu ya 2: Uhifadhi na Uimarishaji wa makaazi.
Programu ya 3: Huduma za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).
Programu ya 4: Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na uhalisia wa majukumu ya wizara katika Sekta ya Ujenzi, Makaazi, Mawasiliano na Usafirishaji, programu hizo zilizozitajwa hapo juu zitakuwa na programu ndogo ndogo kama ifuatavyo:-

Programu ya 1: Miundombinu ya Huduma za Usafirishaji

Programu ndogo (1a): Utunzaji na Matengenezo ya Barabara
Programu ndogo (1b): Usimamizi wa Usafirishaji.
Programu ndogo (1c): Ujenzi wa Miundombinu ya Usafirishaji.
Programu ndogo (1d): Huduma za Usafirishaji.

Programu ya 2: Uhifadhi na Uimarishaji wa Makaazi

Programu ndogo (2a): Ujenzi na Usimamizi wa Majengo ya Serikali.
Programu ndogo (2b): Uhifadhi wa Mji Mkongwe.
Programu ndogo (2c): Uimarishaji wa Makaazi.

Programu ya 3: Huduma za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)

Programu ndogo (3a): Usimamizi wa Miundombinu na Mawasiliano.
Programu ndogo (3b): Usimamizi wa Huduma za Mawasiliano.

Programu ya 4: Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji

Programu ndogo (4a): Utawala na Uendeshaji.
Programu ndogo (4b): Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara.
Programu ndogo (4c): Uratibu wa shughuli za Wizara kwa upande wa Pemba.

F. VIPAUMBELE VIKUU VITAKAVYOTEKELEZWA NA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji katika kuimarisha na kuboresha huduma za Makaazi, Mawasiliano pamoja na Usafirishaji hapa Zanzibar, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, imeweka vipaumbele vifuatavyo:-

Sekta ya Ujenzi: Katika kuimarisha Sekta ya Ujenzi Wizara imeweka vipaumbele vifuatavyo:-

- Kuanza ujenzi wa barabara ya Bububu – Mahonda – Mkokotoni (km 31),
- Kuanza ujenzi wa barabara ya Wete – Chake (km 22).
- Uendelezaji wa ujenzi wa barabara ya Ole – Kengeja (km 35).
- Kuanza Ujenzi wa Barabara ya Koani – Jumbi (km 6.3).
- Kuendelea kutekeleza ahadi za Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kukamilisha ujenzi wa barabara mbali mbali Unguja na Pemba.
- Kuzifanyia matengenezo barabara na madaraja mbalimbali yaliyoathirika kwa mvua za masika (zikiwemo Changaweni,

Kiwani, Kipapo, Mangwena, Pujini, Kiungoni, Mwanakwerekwe, Kibonde-Mzungu na daraja la Chamanangwe).

Sekta ya Makaazi: - Katika kuimarisha Sekta ya Makaazi Wizara imeweka vipaumbele vifuatavyo:-

- Kuhakikisha Ujenzi wowote unaofanyika hapa Zanzibar unafuata viwango vya Ujenzi vilivyowekwa kwa mujibu wa sheria.
- Kuhakikisha Mji Mkongwe wa Zanzibar unahifadhiwa na kuendelezwa kiutamaduni na kihistoria.
- Kuzitambua na kuziorodhesha na kuzifanyia ukarabati, nyumba zote zinazomilikiwa na Shirika la Nyumba Zanzibar.

Sekta ya Mawasiliano: - Katika kuimarisha Sekta ya Mawasiliano wizara imeweka vipaumbele vifuatavyo:-

- kuimarisha miundo mbinu ya mawasiliano na mkonga (awamu ya pili).
- Kukamilishwa kwa sheria ya TEHAMA.
- Kuboresha Mawasiliano ya kutumia *Video Conference* katika kila Wilaya Zanzibar.
- Kutoa Elimu juu ya umuhimu wa kulinda Miundombinu ya Mkongo wa Mawasiliano katika sehemu zilizolazwa.

Sekta ya Usafirishaji: - Katika kuimarisha Sekta ya Usafirishaji Wizara imeweka vipaumbele vifuatavyo:-

- Kuanza ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri kwa awamu ya kwanza.
- Kununua meli mpya mbili moja ya mafuta na moja ya abiria pamoja na ununuzi wa boti ndogo za kusafirisha abiria katika maeneo ya visiwa vidogo vidogo ambavyo wananchi wetu wanaishi.
- Kuendelea na uimarishaji wa Bandari ya Mkokotoni,

Bandari ya Wete pamoja na ununuzi wa mashine mbili nyengine za kukagulia abiria na mizigo bandarini.

- Kuimarisha ulinzi na usalama wa usafiri baharini kwa kununua boti nne (4) za *Patrol* ambazo zitafanya kazi kwenye ukanda wa pwani ya Afrika ya Mashariki.
- Kuimarisha huduma za uwanja wa ndege kama vile kumbi, mizigo na maeneo ya kusubiria ndege na huduma nyengne za majengo.
- Kuimarisha Kiwanja cha Ndege cha Pemba pamoja na kuendelea na ujenzi wa Jengo jipya la Abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Abeid Aman Karume.

G. MUHTASARI WA MAELEZO KWA KILA PROGRAMU NA MALENGO YANAYOTARAJIWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

Mhe. Mwenyekiti, programu kuu zilizotajwa hapo juu zimewekewa malengo mahususi, matokeo ya muda mrefu yatakayopatikana, huduma zitakazotolewa, shabaha na viashiria mbali mbali vitakavyotumika kupima utekelezaji wa huduma zitakazotolewa katika Sekta ya Ujenzi, Makaazi, Mawasiliano na Usafirishaji. Maelezo ya programu na malengo yake ambayo yatatekelezwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ni kama ifuatavyo:

G.1 PROGRAMU YA MIUNDOMBINU YA HUDUMA ZA USAFIRISHAJI

Mhe. Mwenyekiti, programu hii ina lengo la kuwepo kwa miundombinu bora na huduma za usafiri zilizobora, salama na endelevu. Programu ya Miundombinu ya Huduma za Usafirishaji ina programu ndogo nne (4) ambazo ni; Programu ndogo (1a): Utunzaji na Matengenezo ya Barabara, Programu ndogo (1b): Usimamizi wa Usafirishaji, Programu ndogo (1c): Ujenzi wa

Miundombinu ya Usafirishaji na Programu ndogo (1d): Huduma za Usafirishaji. Programu hii inatekeleza lengo la MKUZA III la kuwezesha kupatikana kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika sekta mbali mbali hapa Zanzibar.

G.1.1 Programu Ndogo ya Utunzaji na Matengenezo ya Barabara

Mhe. Mwenyekiti, programu ndogo ya kwanza ya Utunzaji na Matengenezo ya Barabara inasimamiwa na Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara (UUB) na ina lengo la kuimarisha miundombinu ya usafiri wa barabara kwa kujenga, kuzitunza na kuzifanyia matengenezo barabara mbali mbali za Unguja na Pemba. Huduma zinatolewa katika programu hii ndogo ni ujenzi na utunzaji wa miundombinu ya barabara mbali mbali, ikiwemo kuzifanyia matengenezo barabara hizo, pamoja na zile zilizoathirika kwa mvua kubwa zilizonyesha mwezi wa April na Mei, mwaka 2017 na uwekaji wa miundombinu ya usalama barabarani.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 wizara kupitia programu hii imepanga kufanya matengenezo ya kawaida ya barabara (*Routine Maintenance*) km 674, kuzifanyia matengenezo ya muda maalum km 26.2 za barabara mbali mbali kwa kiwango cha lami na kifusi kwa Unguja na Pemba pamoja na kuweka taa za kuongozea magari (*traffic lights*) katika maeneo ya makutano ya barabara ya *Muzamil Center*, Mtoni na Kwa Jumapweza (kwa upande wa Unguja) na Mtemani na Chachani (*PBZ junction*) kwa Pemba. Orodha ya barabara zinazotarajiwa kufanyiwa matengenezo ya muda maalum kwa mwaka 2017/2018 kwa Unguja na Pemba zinaonekana katika KIAMBATANISHO NAMBA 4.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, programu hii ndogo imepangiwa kutumia jumla ya TZS 2,241,692,000 ambazo

zitatumika kwa kazi za kawaida. Fedha nyengine za programu hii ndogo ambazo zinahusu matengenezo ya barabara mbali mbali zinatoka Mfuko wa Barabara na zinasimamiwa na Wizara ya Fedha na Mipango.

G.1.2 Programu ndogo ya Usimamizi wa Usafirishaji

Mhe. Mwenyekiti, Programu ndogo ya pili ya Usimamizi wa Usafirishaji inasimamiwa na Idara ya Usafiri na Leseni, Mamlaka ya Usafiri Baharini pamoja na Bodi ya Usafiri Barabarani. Programu hii ndogo ina lengo la kupatikana huduma bora za usafiri wa barabara na baharini zilizo salama hapa Zanzibar. Huduma ambazo zinatolewa katika programu hii ni usimamizi wa upatikanaji wa huduma za usafiri wa barabarani, usimamizi wa usalama barabarani, usimamizi wa usafiri wa baharini pamoja na matengenezo ya vyombo vya moto.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara kupitia programu hii ndogo imepanga kutekeleza malengo kupitia taasisi inazosimamia programu hii ndogo kama ifuatavyo:-

Idara ya Usafiri na Leseni

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Idara ya Usafiri na Leseni kupitia Programu hii ndogo imepanga kuimarisha usalama wa barabarani kwa kuendelea kuwapatia elimu watumiaji wa barabara pamoja na kuimarisha ukaguzi wa vyombo vya moto. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 wizara kupitia idara hii itaanza kutoa adhabu za papo kwa papo kwa madereva wote wa vyombo vya moto ambao watafanya makosa barabarani ili kuondoa mrundikano wa kesi Mahakamani. Vile vile wizara inakusudia kubadilisha mfumo wa uendeshaji wa Karakana Kuu na kuwa Wakala wa Serikali wa matengenezo ya vyombo vya moto ili iweze kutoa huduma kwa ufanisi zaidi na kuongeza mapato serikalini.

Bodi ya Usafiri Barabarani

Bodi ya Usafiri Barabarani imeanzishwa rasmi kwa kifungu cha 14(1) cha Sheria ya Usafiri Barabarani nambari 7 ya mwaka 2003, kwa lengo la kumshauri Mhe, Waziri kuhusiana na masuala yanayohusiana na usafiri wa barabara. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 imepanga kuendelea kusimamia usalama wa vyombo vya moto barabarani pamoja na kutoa elimu kwa watumiaji wa barabara.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Programu hii ndogo imepangiwa kutumia jumla ya TZS 1,116,719,000 ambazo zitatumika kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo jumla ya TZS 766,719,000 ni kwa ajili ya Idara ya Usafiri na Leseni na jumla ya TZS 350,000,000 ni Ruzuku kwa ajili shughuli za Bodi ya Usafiri Barabarani.

Mamlaka ya Usafiri Baharini

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Mamlaka ya Usafiri Baharini, kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018, imepanga kuendelea kuandaa kanuni zinazotokana na Sheria ya Mamlaka ya Usafiri Baharini, kusimamia makampuni yanayotoa huduma ya Usafiri Baharini kwa kuyapatia leseni, kuimarisha usalama wa usafiri baharini kwa kununua boti nne (4) za uokozi (*rescue boats*) kupitia msaada wa Serikali ya Korea ya Kusini ambazo zitafanya kazi kwenye bahari ya Zanzibar pamoja na kuanza na kukamilisha miradi mbali mbali iliyoanza ikiwemo Ujenzi wa Ofisi ya Pemba, usajili wa meli kwa kutumia mfumo wa TEHAMA pamoja na kuanzisha kituo cha kufuatilia mwenendo wa vyombo na mazingira ya baharini.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Mamlaka imepanga kukusanya jumla ya TZS 5,112,728,012. Kati ya fedha

hizo jumla ya TZS 4,829,228,012 ni mapato yatokanayo na huduma mbali mbali zinazotolewa na Mamlaka na jumla ya TZS 283,500,000 ni fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Aidha, Mamlaka imepanga kutumia jumla ya TZS. 4,698,217,200 kwa kazi za kawaida na maendeleo ambapo kazi za kawaida zitagharimu TZS 4,059,717,200 na kazi za Miradi ya Maendeleo zitagharimu TZS 638,500,000.

G.1.3 Programu ndogo ya Ujenzi wa Miundombinu ya Usafirishaji

Mhe. Mwenyekiti, Programu ndogo ya Ujenzi wa Miundombinu ya Usafirishaji inasimamiwa na Idara ya Mipango.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri nakutanabahisha kwamba muda wako uliobakia ni dakika 20 na hotuba yako bado inaendelea. Kwa hivyo, unaendelea lakini ikifika muda kwa mujibu wa kanuni 96(2) itabidi utawasilisha kuwa taarifa iingizwe katika *hansard*. Ahsante endelea.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa hilo, lakini kama nilivyosema awali wizara hii ni wizara kubwa sana ina shughuli nyingi sana na ninaamini wananchi wa nchi hii wanataka kujua tunafanya nini na nitajitahidi nimalize haraka iwezekanavyo, lakini kama nitahitaji muda zaidi nitakuomba Mhe. Mwenyekiti, uweke kando hizi kanuni uniongeze dakika wananchi wapate kujua kunapita nini Ahsante Mhe. Mwenyekiti,.

Mhe. Mwenyekiti, programu ndogo ya ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji inasimamiwa na Idara ya Mipango Sera na Utafiti na ina lengo la kuwepo miundombinu ya usafirishaji iliyo bora, salama na endelevu kwa Unguja na Pemba. Huduma ambazo zinatolewa katika programu hii ni uimarishaji wa miundombinu ya barabara ikiwemo miradi mikubwa ya ujenzi wa barabara,

uimarishaji wa miundombinu ya usafiri wa anga ukiwemo ujenzi wa miradi mikubwa katika sekta ya usafiri wa anga pamoja na uimarishaji wa miundombinu ya usafiri wa baharini ikiwemo ujenzi wa bandari. Orodha ya miradi inayotarajiwa kutekeleza mwaka 2017/2018 inaonekana katika **KIAMBATANISHO NAMBARI 2.**

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, programu hii ndogo imepangiwa kutumia jumla ya TZS 188,799,402,000 ambazo zitatumika kwa ajili ya uimarishaji wa miundombinu ya usafirishaji. Kati ya fedha hizo jumla ya TZS 163,369,402,000 ni mkopo kutoka Washirika wa Maendeleo na jumla ya TZS 25,430,000,000 ni mchango kutoka serikalini.

G.1.4 Programu ndogo ya Huduma za Usafirishaji

Mhe. Mwenyekiti, Programu ndogo ya Huduma za Usafirishaji inasimamiwa Idara ya Mipango, Sera na Utafiti; Shirika la Bandari; Shirika la Meli na Uwakala pamoja na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Programu hii ndogo ina lengo la kuwepo huduma bora za usafirishaji wa abiria na mizigo baina ya visiwa vya Zanzibar na maeneo mengine. Huduma ambazo zinatolewa katika programu hii ni usimamizi wa shughuli za uendeshaji wa meli na uwakala, utoaji wa huduma za bandari pamoja na utaoaji wa huduma za viwanja vya ndege Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 wizara kupitia programu hii ndogo imepanga kutekeleza malengo kupitia taasisi inazosimamia programu hii ndogo kama ifuatavyo:-

Shirika la Bandari Zanzibar

Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Bandari kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018, imepanga kutekeleza malengo mbali mbali katika utoaji wake wa huduma Bandarini Unguja na Pemba. Malengo

hayo ni pamoja na kuhudumia jumla ya meli 130 za kigeni zenye uzito (GRT) wa Tani Milioni 2.2, Meli za ndani zipatazo 3,600 na Majahazi 4,100. Kuhudumia tani 300,000 za mzigo mchanganyiko, makontena 56,500 (TEUs 73,500) pamoja na tani 132,000 za mzigo wa majahazi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa kazi za maendeleo, Shirika litaendelea na programu yake ya uimarishaji wa vitendea kazi na linatarajia kumalizia miradi inayoendelea kutoka mwaka 2016/2017 pamoja na ujenzi wa tishali (*barge*) la kufungia vyombo katika gati ya abiria. Aidha, kwa upande wa miundombinu Shirika linatarajia kuendelea na uimarishaji wa Bandari ya Mkokotoni, Bandari ya Wete, Kituo cha Kigomasha, matengenezo ya minara ya kuongozea meli (*Beacon*) za Unguja na Pemba pamoja na ujenzi wa Nyumba ya Tawi la Shirika Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha Ulinzi na Usalama wa Bandari Shirika linatarajia kuendelea na mradi wa ununuzi wa mashine mbili za kukagulia abiria na mizigo, *"CCTV camera"* za ulinzi pamoja na ujenzi wa Ukuta wa ulinzi katika gati ya abiria Malindi. Aidha, Shirika linaendelea na uimarishaji wa Kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Shirika imepanga kukusanya jumla ya TZS 30,787,758,000 na kutumia jumla ya TZS 25,841,420,000 kwa kazi za kawaida na TZS 10,174,563,000 kwa kazi za maendeleo. Aidha Shirika linatarajia kutumia akiba yake pamoja na mikopo kwa ajili ya kazi za maendeleo kwa mwaka 2017/2018.

Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar

Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Meli na Uwakala kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018, limepanga kufanya safari 168 za ndani kwa

kutumia meli zake, ambapo jumla ya abiria 262,680, tani 28,080 pamoja na magari 1,320 zitahudumiwa. Aidha, shirika litaendelea na mkataba wa kuikodisha Meli ya MT. Ukombozi kwa kampuni ya *GAPCO*. Kwa upande wa Uwakala, Shirika limepanga kuhudumia jumla ya meli 155 za kigeni zikiwemo za makontena, mizigo mchanganyiko, meli za mafuta na meli za kitalii. Vile vile Shirika linatarajia kuhudumia jumla ya kontena 30,240 kwa mwaka.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, shirika imepanga kukusanya jumla ya TZS 15,546,557,200 na kutumia jumla ya TZS 15,476,092,378 kwa kazi za kawaida na maendeleo. Kati ya matumizi hayo TZS 14,882,112,378 ni kwa matumizi ya kawaida na TZS 593,980,000.00 kwa kazi za maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka fedha 2017/2018, serikali imeamua kununua meli ya mafuta na meli ya abiria na mizigo ambapo jumla ya TZS 18,000,000,000; katika vitabu vyenu waheshimiwa vimeandikwa Shilingi 20,000,000,000 tumefanya marekebisho itakuwa ni 18,000,000,000 zimetengwa kufanikisha kazi hiyo. Vile vile wizara imepanga kununua boti ndogo ndogo ambazo zitatumika kutoa huduma za usafiri wa baharini kwa wananchi wanaoishi na wanaokwenda katika maeneo ya visiwa vidogo vidogo ambavyo raia wetu wanaishi hapa Zanzibar, ambapo jumla ya TZS 800,000,000 zimetengwa kufanikisha lengo hilo.

Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018, imepanga kuendelea kuimarisha ulinzi na usalama ili kuongeza viwango vya usalama wa kitaifa na kimataifa, kuendeleza na kuimarisha miundombinu ya Viwanja vya ndege, kuimarisha huduma za uwanja wa ndege kama vile kumbi, mizigo na maeneo ya kusubiria abiria na huduma nyengine

za majengo, kuimarisha mazingira ya kibiashara na kuongeza ukusanyaji wa mapato.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Mamlaka imepanga kukusanya jumla ya TZS 10,240,529,654 na kutumia jumla ya TZS 13,907,252,041 kwa kazi za kawaida na maendeleo, ambapo ziada ya matumizi ya TZS 3,666,722,387 inatarajiwa kupatikana kwa njia ya mkopo. Kati ya fedha hizo TZS 11,450,134,041 ni kwa matumizi ya kawaida na TZS 2,457,118,000 ni kwa kazi za maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, programu hii ndogo ya huduma za usafirishaji imepangiwa kutumia jumla ya TZS 18,800,000,000 kutoka Serikali Kuu ambazo zitatumika kwa ajili ya ununuzi wa meli na boti.

G.2 PROGRAMU YA UHIFADHI NA UIMARISHAJI WA MAKAAZI

Mhe. Mwenyekiti, programu hii ina lengo la kuwepo kwa nyumba bora za Serikali, makaazi bora yenye gharama nafuu kwa jamii pamoja na kuuhifadhi na kuuendeleza Mji Mkongwe, hayo nimekwishayaeleza. Katika programu hizo kuna Programu hii ya Uhifadhi na Uimarishaji wa Makaazi ina programu ndogo tatu (3) ambazo ni; Programu ndogo (2a): Ujenzi na Usimamizi wa Majengo ya Serikali, Programu ndogo (2b): Uhifadhi wa Mji Mkongwe na Programu ndogo (2c): Uimarishaji wa Makaazi. Aidha, programu hii inatekeleza lengo la MKUZA III kama nilivyoeleza.

G.2.1 Programu ndogo ya Ujenzi na Usimamizi wa Majengo ya Serikali

Mhe. Mwenyekiti, programu ndogo ya kwanza ya Ujenzi na Usimamizi wa Majengo ya Serikali inasimamiwa na Wakala wa

Majengo hapa Zanzibar na ina lengo la kuhakikisha kuwepo kwa nyumba bora za serikali. Huduma zinazotolewa katika programu hii ndogo ni ujenzi na matengenezo ya nyumba za Serikali pamoja na usimamizi na utoaji wa ushauri elekezi kwa majengo ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 wizara kupitia programu hii ndogo ambayo inasimamiwa na Wakala wa Majengo imepanga kuzifanyia matengenezo ya nyumba nne (4) za serikali pamoja na kuendelea kutoa ushauri elekezi kwa miradi mbalimbali ya Taasisi za Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Programu hii ndogo imepangiwa kutumia jumla ya TZS 591,812,000 ambazo zitatumika kwa kazi za kawaida.

G.2.2 Programu ndogo ya Uhifadhi wa Mji Mkongwe

Mhe. Mwenyekiti, programu ndogo ya pili ya Uhifadhi wa Mji Mkongwe inasimamiwa na Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe na ina lengo la kuhakikisha Mji Mkongwe wa Zanzibar unahifadhiwa na kuendelezwa kiutamaduni na kihistoria. Huduma zinazotolewa katika programu hii ndogo ni uhifadhi na uendelezaji wa Mji Mkongwe wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 wizara kupitia programu hii ndogo ambayo inasimamiwa na Mamlaka ya Mji Mkongwe imepanga kuuhifadhi Mji Mkongwe pamoja na kuuendeleza kiutamaduni na kihistoria, kuimarisha maeneo ya wazi kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya kijamii, kuendelea kutoa ushauri wa kitaalamu na kusimamia miradi ya Uhifadhi wa majengo, kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa uhifadhi wa Mji Mkongwe pamoja na kuibua vyanzo vipya vya mapato kwa ajili ya kuongeza uwezo wa kifedha wa Mamlaka.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Programu hii ndogo imepangiwa kutumia jumla ya TZS 503,500,000 ambazo ni Ruzuku ya matumizi ya kawaida.

G.2.3 Programu ndogo ya Uimarishaji wa Makaazi

Mhe. Mwenyekiti, Programu ndogo ya tatu ya Uimarishaji wa Makaazi inasimamiwa na Shirika la Nyumba Zanzibar, Bodi ya Usajili ya Wakandarasi, Bodi ya Usajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo, Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba na Bodi ya Usimamizi na Utunzajia wa Majumba (*Condominium*). Programu hii ndogo ina lengo la kuhakikisha upatikanaji wa makaazi bora, salama na yenye gharama nafuu kwa jamii. Huduma zinazotolewa katika programu hii ndogo ni utoaji wa huduma bora za makaazi kwa jamii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara kupitia Programu hii ndogo imepanga kutekeleza malengo kupitia taasisi zinazosimamia kama ifuatavyo:-

Shirika la Nyumba Zanzibar

Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Nyumba kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018, limepanga kutekeleza malengo yake mbali mbali ikiwemo: ukarabati wa majengo ya shirika, kuzitambua na kuziorodhesha nyumba za shirika, kukuza uwezo wa shirika kwa kujenga nyumba za bei nafuu pamoja na kujenga uwezo wa kitaaluma kwa wafanyakazi wa shirika.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Shirika kupitia vianzio vyake vya mapato limepanga kukusanya jumla ya TZS 5,558,000,000 na kutumia jumla ya TZS 5,046,400,000 kwa kazi za kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo miradi ya maendeleo intarajiwa kugharimu TZS 3,000,000,000 na matumizi ya kawaida yanatarajiwa kugharimu TZS 2,046,400,000.00

Bodi ya Usajili wa Wakandarasi Zanzibar

Mhe. Mwenyekiti, Bodi ya Usajili wa Wakandarasi imeanzishwa mwaka 2008 kwa Sheria Namba 6 ya Mwaka (2008) na imepewa jukumu la kusajili wakandarasi wote nchini pamoja na kuweka taratibu na kusimamia upangaji wa daraja kwa wakandarasi kwa mujibu wa viwango (*standards*) vya vifaa vya ujenzi na wataalamu walionao.

Mhe. Mwenyekiti, Bodi ya Usajili wa Wakandarasi kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018, imepanga kutekeleza malengo yake mbali mbali ikiwemo: kuhakikisha Wakandarasi wote wanaofanya kazi nchini wanasajiliwa, Mkandarasi anafanya kazi kwa mujibu wa sheria na kanuni za bodi na katika daraja alilosajiliwa, kusajili miradi yote ya wakandarasi, kuhakikisha ujenzi wowote unaofanyika nchini kwa mujibu wa sheria ya Bodi ya Usajili wa Wakandarasi unafuata viwango vya ujenzi (*Standards*) pamoja na kuandaa mafunzo mbali mbali kwa wakandarasi, wajumbe wa Bodi na watendaji ili kuwajengea uwezo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, bodi imepanga kukusanya jumla ya TZS 437,613,000.00 na kutumia jumla ya TZS 433,175.000 kwa kazi za kawaida.

Bodi ya Usajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo

Mhe. Mwenyekiti, Bodi ya Usajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo imeundwa mwaka 2008 kwa Sheria namba 5 ya mwaka (2008) na imepewa jukumu la kusajili Wasanifu, Wahandisi, Wakadiriaji Majengo pamoja na Mafundi sanifu wa Ujenzi. Aidha, bodi inasajili kampuni zinazohusika na kutoa huduma za Usanifu, Uhandisi na Ukadiriaji Ujenzi.

Mhe. Mwenyekiti, Bodi ya Usajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018, imepanga kutekeleza malengo yake mbali mbali ikiwemo: Kusajili, kuelimisha, kuwaendeleza pamoja na kufuatilia utendaji kazi za wataalamu wote wa ujenzi waliotajwa katika sheria ya uanzishwaji wa bodi hiyo. Aidha, bodi imepanga kusajili Wataalamu bingwa wazalendo 25, Wataalamu wa kigeni 10, Wataalamu wahitimu 30, Mafundi sanifu 15 pamoja na Makampuni ya ushauri wa ujenzi 10. Vile vile bodi inatarajia kusajili jumla ya miradi ya ujenzi wa majengo 280 kwa Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, bodi imekadiria kukusanya jumla ya TZS 403,525,000. Kati ya fedha hizo jumla ya shilingi mia mbili sitini na sita milioni ni makusanyo kupitia katika vianzo vyao mbali mbali ya Bodi na jumla ya shilingi mia moja thathini na saba milioni saba milioni laki tano ishirini na saba elfu zinatarajiwa kupatikana kwa washirika wa Maendeleo.

Aidha bodi imepanga kutumia shilingi mia nne na tatu milioni laki tano ishirini na tano elfu kwa kazi za kawaida. Mhe. Mwenyekiti,.....

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri kwa mujibu wa muda wako umemaliza na sasa nikuombe tu utoe hoja na muda uliobakia sehemu ya hotuba yako iingie katika *Hansard* kama ilivyo taratibu.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliani na Usafirishaji: Niombe kwa ruhusa yako nihitimishe. Nahitimisha tu Mheshimiwa kwa kusema kwamba...

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante endelea fanya hitimisho.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliani na Usafirishaji: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, ningependa katika kuhitimisha kutoa shukurani za dhati zielekezwe kwa washirika wa maendeleo akiwemo Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*), Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Kiuchumi Afrika (*BADEA*), Benki ya Exim ya China, Saudi Fund, Mfuko wa Maendeleo ya Nchi zinazotoa Mafuta Duniani (*OFID*), *UNESCO* na wale wote wanaosaidia katika kutoa huduma za ujenzi, makaazi, mawasiliano na usafiri hapa Zanzibar yakiwemo Mashirika ya Serikali na Binafsi kwa kuendelea kutuunga mkono katika kuimarisha Sekta ya Ujenzi, Makaazi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa lengo kuimarisha maendelea na kukuza uchumi wa nchi yetu.

Pia napenda kumshukuru Naibu Waziri wa Wizara yangu, Katibu Mkuu wangu na wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri walioifanya kutayarisha *Budget speech* hii. Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante, waheshimiwa kabla sijamwita Mhe. Mwenyekiti, kuna tangazo hapa kutoka kwa Mhe. Mwenyekiti,. Naomba kuwatangazia Wajumbe wa Kamati ya Bajeti kukutana kwa muda huu katika ukumbi wa juu. Wajumbe wa Kamati ya Bajeti wanatakiwa kwenda kwenye kikao kilichopo ukumbi wa juu kwa muda huu hivi sasa. Ahsanteni.

Baada ya tangazo hili niwaombe Waheshimiwa Wajumbe waziri anapoondoka hapa au katika kumpongeza utaratibu wetu huu wa kumpongeza uwe na muelekeo mzuri katika kupiga meza zetu hizi hapa. Kwa sababu hauendani vizuri katika kumpongeza.

Kwa hivyo, tungekwenda kwa *uniform* ingekuwa vizuri sana kuliko mmoja anapiga kama mwendo wa farasi. Naomba sana tulifanye hilo. Mhe. Mwenyekiti, wa kamati ya Ardhi na Mawasiliano ahudhurie kuwasilisha.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano): Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru kwa kunipa fursa hii kutoa Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Usafirishaji kwa mwaka wa 2017-2018.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake kwa kunijaalia uzima na afya njema na kuweza kusimama mbele ya Baraza hili kuwasilisha Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano ya Baraza la Wawakilishi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa Mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu kusimamia mbele ya Baraza lako tukufu kuchangia katika Hotuba ya Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka huu wa fedha 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, pia napenda kutoa shukrani zangu kwa Waziri na Naibu Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji pamoja na Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi na watendaji wote wa Wizara hii kwa ushirikiano mkubwa walioutoa katika kufanikisha kumalizika kwa kazi hii ya Kamati.

Mhe. Mwenyekiti, kwa dhati kabisa, napenda tena kuipongeza Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa kuweza kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu Bajeti hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kwa umakini na umahiri wa hali ya juu kwa

Bajeti inayozingatia mfumo wa Programu *"Program Based Budget"*(*PBB*).

Mhe. Mwenyekiti, Vile vile, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano kwa mashirikiano waliyonipatia katika kipindi chote cha kazi za Kamati na hatimaye kufanikisha kazi zetu kwa lengo la kuisimamia na kuishauri Serikali. Naomba sasa niwatambue wajumbe wa Kamati hii amabao ni:

1. Mhe. Hamza Hassan Juma - Mwenyekiti
2. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Khadija Omar Kibano - Mjumbe
4. Mhe. Said Omar Said - Mjumbe
5. Mhe. Mohamedraza Hassanali - Mjumbe
6. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Mjumbe
7. Mhe. Nassor Salim Ali - Mjumbe
8. Ndg. Fatma Omar Ali - Katibu

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Baraza la Wawakilishi liliidhinishia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji jumla ya Tshs. 6.324 bilioni kwa ajili ya Fungu P01 kwa Matumizi ya kazi za Kawaida. Aidha, Baraza pia liliidhinishia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kutumia jumla ya Tshs. 182.230 bilioni kwa ajili ya Matumizi ya kazi za Maendeleo. Vile vile, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara iliidhinishiwa kukusanya jumla ya Tshs. 1.762 bilioni kama ni mapato yatokanayo na vyanzo mbali mbali vya wizara hii ambapo hadi kufikia Machi, 2016 Wizara ilikuwa imeshakusanya jumla ya Tshs. 1.121 bilioni katika vyanzo hivyo ambazo ni sawa na asilimia 64 ya makadirio ya mapato kwa mwaka.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na mafanikio makubwa yaliyotokana na jitihada za Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji

zilizopelekea kuongezeka ukusanyaji wa mapato ya Serikali kupitia fedha za ulipaji wa leseni, faini za makosa ya Barabarani, Usimamizi na Usajili wa Wakandarasi wazalendo pamoja na wakandarasi kutoka nje ya nchi, uuzaji wa tiketi, tozo za bandari na tozo zinazotozwa na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume kwa watumiaji.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Ardhi na Mawasiliano inapenda kuchukua fursa hii tena kuipongeza Wizara hii kwa juhudi zao wanazozichukua kwa kuweza kuvuka lengo la makusanyo ya mapato katika vyanzo vyao mbali mbali viliopo hapa nchini.

Mhe. Mwenyekiti, imeelezwa katika hotuba ya Bajeti ya Wizara hii ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa mwaka huu wa fedha 2017/2018 Wizara hii imepangiwa Tshs. 9.220 bilioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na Tshs. 46.230 bilioni kwa ajili ya kazi za maendeleo. Aidha, Wizara inakadiriwa kukusanyaTshs. 2.883 bilioni kupitia vyanzo vyao vya ndani. Aidha, katika utaratibu mpya wabajeti inayozingatia programu (*PBB*), Wizara hii imepangiwa kutekeleza Programu Kuu Nne (4) na Programu Ndogo Kumi na Mbili (12) kama zilivyofafanuliwa katika hotuba hiyo ya bajeti ya Wizara hii ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu pia inaisisitiza Wizara kuwa makini sana na matumizi ya fedha zitakazoingizwa katika Programu hizo kwani licha ya uhaba wa fedha, matokeo ya fedha zitakazoingizwa yatahitaji kuonekana na kupimwa kwa umakini na umahiri mkubwa hususan katika utekelezaji wa Programu hizo muhimu.

PROGRAMU YA MIUNDOMBINU YA HUDUMA ZA USAFIRISHAJI

Mhe. Mwenyekiti, Miongoni mwa majukumu makuu ya Programu Kuu hii ni kuhakikisha uwepo wa miundombinu bora na huduma za usafiri zilizo bora, salama na endelevu. Aidha, Programu Kuu hii inakusudiwa kutekelezwa kupitia Programu Ndogo nne (4).

PROGRAMU NDOGO YA UTUNZAJI NA MATENGENEZO YA BARABARA

Mhe. Mwenyekiti, kupitia Programu Ndogo ya Utunzaji na Matengenezo ya Barabara, Kamati yangu inaomba Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri kupitia Makatibu wao kuziwekea utaratibu mbadala wa kuzienzi na kuendelea kuzitunza barabara zetu kwa Upande wa Unguja na Pemba kwa kuzifanyia usafi barabara ambazo hujengwa kwa fedha za wavuja jasho la wananchi walio chini.

Mhe. Mwenyekiti, licha ya mafanikio makubwa kwa upande wa Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara *UUB* kwa kukamilisha ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita 23.40 kwa Unguja na Pemba, bado Idara hii inakumbwa na changamoto mbali mbali kama vile ukosefu wa vifaa vya kutendea kazi, uchakavu wa mitambo ya kutengenezea lami pamoja na ukosefu wa wataalamu hususan katika sekta ya ujenzi wa barabara zenye kiwango. Hii inapelekea kujengwa kwa barabara zisizo na viwango na kupelekea kuhatarisha maisha ya jamii. Mfano mzuri na wenye uhalisia ni ujenzi wa barabara ya Mgagadu – Kiwani yenye urefu wa kilomita 5.85 barabara ambayo haikufika hata mwezi tokea kufunguliwa kwake.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na kadhia hiyo, kamati yangu inaiomba serikali kwa kushirikiana na wizara husika kununua mitambo mipya ya utengenezaji lami, ambapo mitambo iliyopo sasa imedumu kwa zaidi ya miaka 25 tangu kuanza kazi mwaka

1992 na kupelekea watendaji kufanya kazi katika mazingira magumu na hatarishi kwa afya zao.

Mhe. Mwenyekiti, sambamba na hilo, Kamati yangu inaiomba serikali kwa bajeti ya mwaka huu ni vyema kuongeza fedha katika fungu la utunzaji na matengenezo ya barabara ili kuweza kuzihami barabara zilizoharibika ambazo zilikuwa hazimo katika mipango ya bajeti hii tunayoipitisha hivi sasa. Pamoja na kuziongezea bajeti halmashauri zetu na mabaraza ya miji ili kuweza kuzikarabati pia barabara zetu za ndani.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, kamati yangu inaitaka wizara kuharakisha ujenzi wa Barabara ya Wete - Chake ambayo imekwama kwa zaidi ya miaka tisa hivi sasa wakati tenda imesajiliwa na tayari barabara mbili ile ya Wete - Gando na Wete - Konde zimeshajengwa lakini hii ya Wete - Chake imekuwa na kigugumizi wakati pesa zipo na mkandarasi alikwishakupatikana. Hali hii haipendezi hata kidogo kwani Miradi mikubwa ya Wizara hii inakuwa na changamoto nyingi ambazo zinaweza kuepukika ikiwa waliopewa dhamana watakua makini katika kusimamia majukumu yao. Pia Kamati yangu inaendelea kusisitiza kuwa kwa vile barabara ile imeshafanyiwa tathmini ya kulipwa fidia wananchi watakaoathirika na mradi huo, basi Serikali iwalipe wananchi hao ili waweze kujiimarisha na masuala yao mengine ya kimaisha.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu inapongeza jitihada zinazofanywa na serikali hivi sasa katika maandalizi ya kuijenga upya barabara ya Mahonda, Kinazini, Chaani hadi Mkwajuni kwani itawaondolea shida ya usafiri wananchi hasa wa Chaani ambao hivi sasa wanapata taabu sana kutokana na barabara yao kuwa iko hali mbaya sana. Hata hivyo, Kamati yangu ingelipendelea zaidi kuona ujenzi huo unaanzia Kituo cha Polisi cha Bububu kwani ubovu wa barabara ile umeanzia hapo.Tunaishauri serikali isione hasara kutumia pesa wakati

watakaofaidika ni wananchi wenyewe ambapo tumeshuhudia barabara za wenzetu tunapokwenda nchi za nje. Mfano mzuri ni majirani zetu Tanzania Bara ambao wameanza kujenga '*Fly-Overs'*. Sasa sisi tunaona hasara ya nini? Hivyo nawaomba Wajumbe wenzangu kwa Baraza hili tuilazimishe Serikali kufanya ujenzi wa Barabara hiyo ukianzia Kituo cha Polisi cha Bububu.

Mhe. Mwenyekiti, pia, tunaitaka serikali kuharakisha kulipa fidia wananchi watakaoathirika na ujenzi wa barabara hii mpya na ya kisasa. Msisitizo wa Kamati yangu ni kwamba kujengwa kwa mitaro ya kutolea maji ya mvua wakati wa ujenzi huo hasa kwa ya yale maeneo muhimu ambayo yanajulikana kuwa hupata maji maji wakati mvua zinaponyesha. Pia, kuweka njia maalum au mabomba ya kupitisha maji pamoja na Mkonga ilikuweza kuzihami barabara hizo na ukataji wa huduma muhimu za mawasiliano kama ilivyotokea katika barabara ya Fuoni. Aidha, kutokana na kadhia hiyo, tunaiomba serikali itueleze kuwa katika hatua ya ujenzi wowote utakaotokezea hapo baadae kwa namna gani hakutoathiri huduma hizo ambazo tayari zishatumia pesa nyingi katika uwekaji wake.

PROGRAMU NDOGO YA USIMAMIZI WA USAFIRISHAJI

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, moja kati ya Programu ndogo iliyotengwa kutekelezwa Kupitia Programu Kuu hii ni Programu ndogo ya Usimamizi wa Usafirishaji ambapo kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Baraza lako tukufu liliidhinisha jumla ya Tshs. 561,430 milioni kwa ajili ya utekelezaji wa huduma za usimamizi wa usalama barabarani, usimamizi wa utoaji wa huduma za usafiri wa barabara, mategenezo ya vyombo vya moto pamoja na kusimamia usafiri wa barabara. Aidha, Kamati inashangazwa kuona kwa mwaka huu kupitia Programu ndogo hii inaombewa jumla ya Tshs. 1,188,974 Bilioni.

Mhe. Mwenyekiti, kitu kinachosikitisha kabisa ni Kamati kuona baadhi ya Idara kuidhinishiwa fedha ila uingizwaji wa fedha hizo huwa haziwi kama zilivyopangwa kutoka Wizara ya Fedha hali ambayo husababishia Idara hizo kufanya kazi katika mazingira magumu kama vile Idara ya Usafiri na Leseni iliopo Mwanakwerekwe ambapo jengo hilo huvujiwa na maji hususan katika kipindi kama hiki cha mvua na wafanyakazi kukosa hata pa kukaa.

Mhe. Mwenyekiti, licha ya hayo, Kamati yangu imeshangazwa kuona Bodi ya Usafiri Barabarani kutofanyakazi tangu Bodi hiyo ilipoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ambapo iliwahi kukutana kikao kimoja tu cha ufunguzi kwa Mweyekiti na Wajumbe wake kukutana ambapo hadi kufikia leo wajumbe hao wanadai fedha zao za kikao hicho hali hii inatusikitisha sana kwa manufaa ya Taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, Vile vile, Kamati yangu inaiomba Wizara kwa kushirikiana na Idara husika kuandaa utaratibu wa kuimarisha usalama wa barabarani kwani barabara zetu nyingi zilizopo mjini na vijijini huwa hazina hata alama za barabarani kitu ambacho hupelekea ongezeko za ajali zisizokuwa za lazima kwa madereva wetu.

PROGRAMU NDOGO YA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA USAFIRISHAJI

Mhe. Mwenyekiti, majukumu yaliopangwa kutekelezwa ndani ya Programu Ndogo hii ni Uimarishaji wa Miundombinu ya Barabara, Uimarishaji wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji wa Anga na Uimarishaji wa Miundombinu na Huduma za Bandari. Kupitia programu hii, Kamati inalishauri Shirika la Bandari Zanzibar kuandaa utaratibu maalum wa ukaguzi wa mizigo ya wageni wanaoingia ndani ya nchi yetu kupitia Bandari ili kuondoa usumbufu unaowakabili wageni

wakati wa kuteremka meli. Pamoja na hayo, Kamati pia inaitaka Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Bandari kuharakisha ununuzi wa mashine za ukaguzi wa mizigo.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, Kamati yangu inalitaka Shirika la Bandari kuwa na mipango sahihi na endelevu kwani nchi yetu inatekeleza sana biashara na usafirishaji wa abiria na mizigo, kwa hiyo ni vyema kuangalia sera zetu pamoja na Sheria kuwaruhusu *'Private sector'* kuekeza katika *ICD's* ili kuhifadhia makontena kwani pale Bwawani yanapokaa Makontena hivi sasa ni pahala pa dharura. Sisi sote ni mashahidi juu ya hali ilivyokua mbaya pale muekezaji alopotaka kulitumia eneo lile jinsi tulivyopata taabu mpaka kupelekea Makamu wa Pili wa Rais kuingilia kati na kuokoa hali. Pamoja hali hiyo ilivyokuwa, lakini hivi sasa tumeshajisahau hatujui kuwa ile hali inaweza kujirejea tena na kuwapa taabu wafanyabiashara wetu pia na watendaji wa Shirika wenyewe. Kwa hakika huu ndio muda muafaka kuwaalika wawekezaji wanaotaka kuekeza kwenye kujenga *ICD's* kwa ajili ya kuhifadhia Makontena.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu pia inamuomba waziri kufuatilia masuala ya maslahi ya wafanyakazi wa Shirika kwa kuzingatia majukumu yao kama shirika na sio idara.

Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Meli tunawapongeza kwa kufanya kazi zao kwa ufanisi mkubwa lakini ushauri wa kamati yangu ni kuharakisha ununuzi wa Meli nyingine ya Mafuta ili kuongeza mapato ya shirika kwani iliyopo imeshakuwa ya muda mrefu sana.

Pamoja na kuwa Shirika limeweza kununua Meli ya Mapinduzi II, Kamati yangu inahisi iko haja ya kununua Meli nyingine ya mizigo yenye muundo ambao utaweza kupakia magari mengi pamoja na mizigo kama zilivyo baadhi ya Meli za watu binafsi ili kuongeza mapato kwa Shirika lakini pia kubana matumizi pale

Serikali inapotokea kuwa na mizigo yao hasa wakati wa Sherehe mbali mbali za kitaifa.

Mhe. Mwenyekiti, licha ya mafanikio hayo bado wananchi wanataka kujua kibiashara kama Meli yetu ya Mapinduzi II inamuelekeo wa kuleta faida kubwa kwa majaribio yanayoendelea kufanywa na Shirika kwa hivi sasa hasa safari za Comoro, Tanga na Mombasa.

Mhe. Mwenyekiti, Hata hivyo, Kamati yangu inaipongeza Mamlaka ya Usafiri Baharini (*ZMA*) kwa jitihada wanazozichukua kwa kuweza kukisimamia Chuo cha Mabaharia hapa Zanzibar (*DANOUS*) kilichopo hapo Chukwani. Kamati yangu pia inawaomba Waheshimiwa Wajumbe tuwapeleke vijana wetu waende wakasome ubaharia kwani vijana wakitoka pale wanaweza kuajiriwa katika Meli za kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu inamtaka Mheshimiwa Waziri kupitia *ZMA* kulisimamia suala la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuharakisha kuridhia mkataba wa "*Panama Convention*" ili Tanzania iweze nayo kufaidika na nafasi za ajira kwani hadi hivi sasa tunawasilisha ripoti yetu kuna vijana wetu wameshushwa kwenye Meli za nje kutokana na Tanzania kuchelewa kuridhia mkataba huo.

Aidha, Tanzania pia inatakiwa kusaini baadhi ya makubaliano ya kimataifa ili kuiwezesha Zanzibar kusajili meli za nje na hivyo kuongeza mapato kwa Mamlaka, lakini pia Tanzania kupitia *SUMATRA* kuharakisha kuwasilisha nyaraka za Zanzibar kupitia *ZMA* kwani *IMO* inazitaka ziwasilishwe kwa pamoja kama Tanzania. Kutekelezwa kwa jambo hili itakifanya Chuo chetu cha Ubaharia vyeti vyake kutambuliwa Duniani jambo ambalo litaweza kuzalisha ajira nyingi kwa Mabaharia wetu wa Tanzania.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mantiki hiyo, kamati yangu inaitaka *ZMA* kuhakikisha wakala wetu tuliompa dhamana ya kusajili Meli za nje anakuwa muadilifu kwa kutokusajili Meli zilizo na matatizo Duniani lakini pia kupakia bidhaa halali ili wasituchafulie jina letu na uhusiano wetu na mataifa mengine Duniani. Vile vile, Kamati inaitaka *ZMA* kununua boti za uokozi ili kuweza kusaidia pale panapotokea ajali yoyote huko Baharini pamoja na kulinda usalama wa abiria pamoja na mizigo yao kwa kupakia mizigo inayolingana na uwezo waliopewa kwa mujibu wa Sheria.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar, Kamati inaipongeza Mamlaka hii kwa uwekaji wa "*Transformer*" mpya katika kiwanja cha ndege cha Pemba ambayo itasaidia sasa huduma zitakazokuwa zinatolewa ni za uhakika na usalama zaidi. Hata hivyo, pamoja na pongezi hizo, Kamati yangu inasononeshwa na kutoridhishwana kauli ya Serikali inayoitoa kila siku hapa Barazani kwa zaidi ya miaka mitano kuhusu ujenzi wa *Terminal II* hapo *Abeid Aman Karume International Airport*, kwani tangu ujenzi umeanza sisi Wajumbe wa Baraza hili la Wawakilishi tulisema sana kuwa kwanza Uwanja hauko katika vipimo sahihi umezidi mbele kwa karibu mita 30 ila mawazo yetu hayakuzingatiwa, lakini pia "*style*" ya ujenzi wa Uwanja huo tulioambiwa eti ni mtindo wa "*Design and Building*."

Mhe. Naibu Spika, pamoja na hayo, kila siku zikienda ukweli umedhihiri kuwa hatukua makini tangu mwanzo wa ujenzi huo. Serikali haikumpata mshauri muelekezi mzuri ambaye ndie mtaalamu anaeishauri serikali matokeo yake amekula pesa zetu nyingi na hakutushauri vizuri na cha kushangaza serikali yetu imekaa kimya jengo limelala, hakuna kauli yoyote ya serikali inayoaminika kwa hivi sasa kwetu sisi Wawakilishi kwani imefika pahala mpaka kiongozi wetu wa nchi aliandikiwa hotuba alipokuja kulihutubia Baraza na kutupa matumaini kuwa Uwanja wetu wa *Terminal II* kuwa utaanza kujengwa, lakini hadi leo

tunashuhudia viongozi wakienda huku na kule, mapesa mengi yameshatumika kwenye ujenzi ule ikiwa ni jasho la wananchi wetu masikini walipa kodi na pia kupitia bajeti hii Serikali inatuomba tena kuidhinisha pesa mengine bila ya kujua kuwa yatatosha na kukamilisha ujenzi wa Uwanja huo. Kamati inaona kizungumkuti kwani hatujui hatma ya ukamilishaji wa Uwanja huo ambao kwa wakati huu unahitajika zaidi hasa kwa kuzingatia idadi ya watalii wanaongezeka kila siku zikienda mbele.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli tumechoka na kauli tupu tunataka vitendo.Wananchi wanataka uwanja wao wautumie kwani tunaona aibu majirani zetu ambao wamechelewa kujenga Viwanja vyao hivi sasa wanakamilisha ili wavitumie, wakati sisi ndio kwanza tunasoma utenzi na kupigiana makofi ya kupongezana lakini mimi na Kamati yangu mwaka huu tunataka kiwanja chetu kimalizike na kuanza kutumika haraka iwezekanavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu pia inaitaka Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kuharakisha ununuzi wa kifaa cha kuongozea Ndege (*ILS*) hasa wakati wa kutua kwenye hali ya hewa mbaya ya ukungu na mvua kubwa. Kifaa hiki ni muhimu sana kwa kiwanja chetu cha kimataifa kwani miongoni mwa vigezo ambavyo kiwanja chetu (ambacho kiko kwenye "*Category Nine*") kimepatiwa ni lazima kuweka kifaa hicho hasa ukizingatia hivi sasa ndege nyingi kubwa za kimataifa zinakuja hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, kamati yangu inaishauri serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kuharakisha ununuzi wa "*Screen Machine*" ya kukagulia mizigo mikubwa kwani hivi sasa ndege nyingi kubwa haziji hapa Zanzibar kwa sababu haziwezi kupakia mizigo ambayo haijakaguliwa kwa mashine hiyo kutokana na usalama wa ndege zao jambo ambalo wafanya biashara wengi wa hapa Zanzibar wanakosa biashara, au

kupelekea mizigo yao Tanzania Bara na kupelekea serikali yetu kukosa mizigo pia mapato kwa Mamlaka.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na matatizo madogo madogo ya kiutendaji lakini Kamati yangu inaipongeza Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kwa maboresho ya Uwanja wetu wa Ndege huku wakisubiri uwanja wetu wa *Terminal II* ukamilike ili na wao wafanye kazi kwa ufanisi zaidi na utulivu. Kutokana na kadhia hii, tunamuomba Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ashirikiane na Bodi yake pamoja na watendaji wengine kwani bado kuna manung'uniko madogo madogo ambapo Kamati yangu haifurahishwi na hali hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inaishauri serikali kuangalia upya mfumo wa uendeshaji wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, ili kuiachia ikusanye mapato yao kama yalivyo mashirika mengine ya Serikali kwani Uwanja mkubwa ukimalizika utahitaji matumizi makubwa ya umeme jambo ambalo kwa mfumo huu wa mapato kuingia serikalini na kusubiri '*retention'itakuja* kuleta taabu kubwa kwa uendeshaji wa Uwanja huo. Pia serikali inatakiwa kuwasomesha na kuwaandaa vijana kwa ajili ya kukabiliana na uendeshaji wa Uwanja mpya (*Terminal II*) kiutawala, kiusalama na kiufundi kwani utatumia technolojia kubwa na ya kisasa. Hayo ni mambo muhimu labda Waziri akija kufanya majumuisho aje kutuambia wamejiandaa vipi na hali hiyo hapo baadae, na je kuna watu ambao kwa hivi sasa wako masomoni kwa ajili ya uendeshaji wa Uwanja huo mpya.

PROGRAMU NDOGO YA HUDUMA ZA USAFIRISHAJI

Kuwepo kwa programu ndogo hii ni kutoa huduma ya Usimamizi wa Shughuli za Uendeshaji wa Meli na Uwakala. Kamati inaiomba Shirika la Meli kutafuta njia mbadala za kuweza kulitatua tatizo la uuzaji wa tiketi za mkononi hali ambayo inaipelekea Serikali na Taifa kwa ujumla kukosa mapato. Hivyo,

Kamati inaendelea kulitaka Shirika kuharakisha utumiaji wa elektroniki kwa uuzaji wa tiketi ili kuisaidia pato letu lisipotee.

PROGRAMU YA UHIFADHI NA UIMARISHAJI WA MAKAAZI

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ina lengo la kuhakikisha kuwepo kwa majengo bora ya Serikali, makaazi bora yenye tija na manufaa kwa jamii pamoja na kuhifadhi na kuuendeleza Mji Mkongwe wa Zanzibar kihistoria na kiutamaduni.

PROGRAMU NDOGO YA UIMARISHAJI WA MAKAAZI

Kamati yangu kupitia programu ndogo hii inachukua fursa adhimu ya kuipongeza Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa kuona umuhimu wa kuzitengea fedha Bodi ya Usimamizi wa Kodi za Nyumba na Bodi ya Condomium, bodi ambazo kwa muda mrefu zipo bila ya kufanyakazi yoyote.

Mhe. Mwenyekiti, mfano mzuri, Bodi ya *Condomium* iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya *Condomium No*. 10 ya 2010 ambapo kifungu cha 28(1) kinampa Mamlaka Mhe. Rais kuweza kuteuwa Mwenyekiti wa Bodi hiyo kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu hayo. Aidha, kitu cha kusikitisha ni kuwa tangu Mwenyekiti huyo kuteuliwa mwaka 2014 na Mhe. Rais na Mhe. Waziri kuteuwa Wajumbe wa Bodi hiyo, bodi hiyo haikuwahi kukutana hata mara moja kwa kipindi cha miaka yote mpaka Mwenyekiti huyo kumaliza uhai wake wa kutumikia majukumu ya Bodi hiyo. Kutokana na kadhia hiyo, kamati yangu inaiomba serikali na wizara nyengine suala kama hili kuliangalia kwa jicho la wazi kabisa lisije kutokea ambapo huzorotesha na kukwamisha utekelezaji ulio imara kwa Sheria zetu tunazozitunga katika Muhimili huu mtukufu.

PROGRAMU YA HUDUMA ZA TECHNOLOGIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA)

Mhe. Mwenyekiti, azma kubwa ya Programu hii ni kuhakikisha kuwepo kwa miundombinu na huduma bora za Tecknolojia ya Habari na Mawasiliano Zanzibar. Aidha, Programu Kuu hii itatekelezwa chini ya Programu ndogo mbili:

(1) Programu ya Usimamizi wa Miundombinu ya Mawasiliano, na

(2)Programu Ndogo ya Usimamizi wa Huduma za Mawasiliano.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu kupitia utekelezaji wa Programu hii inaiomba Idara ya Mawasiliano kwa kushirikana na wizara kuja kuwapatia Wajumbe wa Baraza lako tukufu elimu juu ya umuhimu wa matumizi ya tecknolojia ya Habari na Mawasiliano. Vile vile, kamati yangu inaendelea kuiomba idara kuweza kuharakisha kukamilika kwa ujenzi wa vituo 10 vya usambazaji wa huduma hizo katika sehemu zote za Mjini na Vijijini.

Mhe. Mwenyekiti, pia kamati inaitaka Idara ya Mawasiliano kukaa pamoja na Mamlaka ya Mawasiliano ya Tanzania (*TCRA*) ili kuandaa utaratibu wa kulitafutia ufumbuzi tatizo sugu linaloikabili jamii juu ya matendo ya udanganyifu na utapeli unaofanywa na baadhi ya watu kwa kushirikiana na watendaji wa baadhi ya Mashirika ya simu za mkononi. Hali hiyo imepelekea watumiaji na wananchi kwa ujumla kupoteza imani ya matumizi ya mitandao pamoja na huduma zinazotolewa ambapo hupelekea hata mapato kutofikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, pia, kamati yangu inaitaka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*) Kanda ya Zanzibar kuja Barazani kutoa elimu ya matumizi ya mtandao faida zake na hasara zake pale inapotumika vibaya. Pia kutoa elimu kwa wananchi wetu ili waweze kuitumia mitandao kwa tija tofauti na hivi sasa vijana

wengi wanavyoitumia mitandao hiyo, kwani kwa wakati wa dunia ya sasa mitandao tukiitumia vizuri basi ni ajira kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inaitaka Mamlaka ya Mawasiliano Zanzibar kuharakisha kukamilisha marekebisho ya Sheria ya mtandao ili kuweza kuwalinda watumiaji na pia kuwabana wale wanaoitumia vibaya mitandao ikiwemo simu za mkononi.

PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA USAFIRISHAJI

Mhe. Mwenyekiti, jukumu kubwa la Programu Kuu hii ni kusimamia uendeshaji na uratibu wa Wizara pamoja na kuhakikisha utayarishaji wa sera na mipango bora katika sekta zote tatu zilizo chini ya Wizara hii kama vile Sekta ya Ujenzi, Sekta ya Makaazi, Sekta ya Mawasiliano na Usafirishaji pamoja na usimamizi mzuri wa rasilimali watu.

Mhe. Mwenyekiti, kupitia Utekelezaji wa Programu Ndogo hizo, kamati inaiomba Wizara kuhakikisha malengo yote yaliopangwa katika bajeti hii tunayoipitisha yanatekelezwa kwa umahiri na ufanisi wa hali ya juu ili kuondokana na changamoto zinazoendelea kujitokeza katika mambo mbali mbali yaliopo ndani ya wizara hii, ambapo hii ndio wizara moja kati ya wizara inayogusa maslahi na maendeleo ya jamii.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu baada ya kuzipitia Programu zote nilizozitaja hapo kabla imeona fedha hizo ni kidogo kutengwa kwa wizara kubwa kama hii ambayo ndio muhimili na jicho la serikali yetu, ambayo bado ina changamoto nyingi zinazohitaji kufanyiwa kazi zikiwemo zile za ubovu na uchakavu wa majengo ya nyumba za taasisi zake, uhaba wa vitendea kazi, uhaba wa usafiri kwa ajili ya Idara mbali mbali pamoja na ufinyu

wa bajeti. Hivyo, kamati inashauri kwamba hali itakaporuhusu katika bajeti ya mwaka ujao 2018/2019 watengewe fedha ambazo zitaweza angalau kupunguza changamoto zinazoikabili Wizara hii muhimu ambayo moja kwa moja inagusa maslahi mapana ya wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho napenda kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya kamati yangu kwa niaba ya kamati pamoja na kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza. Sasa niwaombe Wajumbe wa Baraza lako waijadili na hatimae waiunge mkono bajeti hii ili wamuwezeshe waziri kufanikisha na kutekeleza yale waliojipangia katika mwaka huu wa Fedha 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba yangu na kwa niaba ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kumaliza nilikuwa naomba dakika kidogo ili na mimi niweze kutoa mawazo yangu ya dharura.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nafasi umepewa endelea.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, na mimi kidogo nataka nitowe tahadhari kutokana na hali halisi ya mikataba, naweza kusema mikataba mibovu ambayo ndio inayotukumba katika matatizo yetu haya.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la kwanza naomba kutoa mawazo na kuishauri serikali kuangalia upya Bwawani, Darajani koridoo, hatima ya Mji Mkongwe na Ng'ambo tuitakayo. Katika kuingia katika mikataba hii, ningeomba Mhe. Mwenyekiti, yasije yakatufika kama yaliyotufika ya Uwanja wa Ndege. Kwa hivyo, ningeomba sina haja ya kufafanua najua waziri ninapoongea kitu

hiki anakifahamu nini ambacho nimekusudia, ili kuiokoa tusiitie hasara serikali na ujenzi uliokuwa haumaliziki au haufiki mwisho. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, pia niipongeze wizara katika hatua zake ambazo imesema itapeleka taa za kuongozea gari Pemba. Lakini nimesikia wataweka taa Mtemani ya Wete na pale PBZ ya Chake Chake. Lakini ningeomba waongeze na Machomanne barabara inayokwenda Vitongoji pale ningeomba pia itasaidia sana Mhe. Mwenyekiti,.

Pia nimeona katika kitabu Mhe. Mwenyekiti, kuna faini za papo kwa papo ambazo tutazianzisha ili kuweza kupunguza mlolongo wa mahakamani. Sawa. Lakini tungetazama utaratibu mzuri. Pesa za papo kwa papo mara nyengine hatuna. Kwa hivyo, utakapokuja waziri utueleze mwelekeo, itakuwa pesa zinakatwa kwenye leseni ya mtu wakati wa ku-*renew* au zitakuwa zinakatwa katika leseni ya gari wakati wa ku- *renew* leseni yake, wakati pesa za papo kwa papo inawezekana zikawa ngumu kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, niulize kitu kimoja ambacho kipo kila siku, kuhusu upimaji wa barabara ambao tunasema kila siku katika sheria yetu hapa, kwamba mtu anavamia barabara. Lakini leo waziri utakapokuja hapa nataka unielekeze, kwamba mtu anavamia barabara lakini baadae mtu yule anadai pesa analipwa, anadai vipi wakati amevamia. Hili suala nataka ukija uliweke vizuri kwamba watu wakimbie barabara, sio tunafanya kama mchezo serikali inakuwa haiendi, inakuwa sisi tunafuata barabara au barabara inafuata watu. Kwa hivyo, hili ningeshauri kwa sababu ya vipimo.

Mhe. Mwenyekiti, kule Bara Serikali ya Jamhuri ya Muungano ilitenga pesa ikahakikisha inapima Tanzania nzima wapi barabara usiifikie. Kwa hivyo, ningeomba serikali na hapa tukatenga pesa

hebu tukapima barabara zetu tusifikwe na majanga kama haya, ningeomba na hilo.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, nizungumzie hili suala la simu za mikononi. Hizi simu za mkononi kelele zinakuwa katika mambo mengi. Moja ni kudhalilisha watu na mbili uibiaji wa mambo ya pesa. Lakini mashirika haya haya mbona kadi zao ukitia haziibiwi, mbona pesa zao ukiwatilia wao kama wao haziibiwi zinaibiwa za wananchi tu. Hebu utakapokuja Mhe. Waziri hawa ni watu ambao wanajivutia wao, lakini wao hawaibiwi lakini mwananchi wanampa tabu sana. Kwa hivyo, na hili pia ilikuwa ni wazo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, pia natoa rai yangu kwa serikali au wazo ni kwamba mwakani mwaka 2018/2019 mimi ningeiomba serikali, kwamba tutakapotoa maamuzi ya kuweza kufanya kitu, basi tuweze kufanya vitu vitatu au vinne kwa uwezo wetu, lakini vitu vile vimalizike vishe kwa muda na kwa haraka sana, ili viweze kutumika. Sio tuweze kuchukua nusu hapa mwakani tutamaliza *phase* hii. Tungemaliza *phase* ikatumika, haidhuru wengine wanaumia lakini tukamaliza mustakabali huo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nina suala la mwisho, nataka nizungumzie suala la Uwanja wa Ndege *Terminal II*. Mimi ningewaomba Waheshimiwa Wawakilishi masuala mengi tumeshazungumza kuhusu suala hili. Mimi ninachosema, natoa rai yangu tusipoteze muda sana kuangalia nyuma, tutizame mbele zaidi. Lakini kuna misemo isemayo 'Tusiuze ng'ombe kwa kesi ya kuku'.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la mwisho 'yaliyopita si ndwele tugange yajayo' nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, umetumia muda wako vizuri Waheshimiwa Wajumbe tunaendelea na kuchangia hotuba ya Wizara ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji mchangiaji wetu wa mwanzo atakuwa Mhe. Nadir Abdul-latif na baadae atafuatia Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, Bismillahi rahmani rahim nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na jambo la mwanzo nitaipongeza sana Kamati kwa kueleza vitu vya ukweli kabisa vyenye uhalisia hasa kwenye suala la *Terminal II Airport*, kwa sababu suala hili nilikuwa nikilizungumza mimi kipindi cha nyuma waliokuwa hawafahamu walikuwa wakihisi labda naropokwa au labda sina uhakika ninachokizungumza, na unakuta hata wengine wanafika kusema kwamba unapozungumza jambo la kweli mwisho unakuja kutafsirika si mwenzetu katumwa CUF, lakini huu ndio ukweli. Mimi kufika hapa nimepita kwingi watu wamenichunguza sana mpaka nimefika hapa, isiwe Mwana CCM anapokuja kuzungumza ukweli humu ndani halafu anakuja kuambiwa yeye CUF au tunakutafsiri wewe sio mwenzetu tuende kwenye ukweli.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nashukuru sana kwa kamati kueleza vitu na mimi ningeomba Mhe. Spika, aje aniteue mimi kwenye kamati hiyo niende mimi napenda kamati kama hizi kamati zenye ukweli zinazoeleza mambo wazi wazi ndio ninazozitaka mimi. Kwanza niatanza kuchangia suala la hotuba ya Wizara ya Ujenzi na Mawasiliano. Kuna suala moja hili lipo ninayo *document* hapa kuna vijana ambao wako Ofisi ya Majenzi wamefanya njia ambazo kwa ufupi ni za kitapeli, hii nina *document* hizi hapa huyu mmiliki ni wa Asia wahindi wa kihindu wako mjini hawajawahi kununua nyumba maisha yao katika nyumba za Serikali walifuatwa na watu wawili kutoka Wizara hii *official* dukani kwao bwana wee twenda tukakuuzie nyumba, wale wakakubali wakapelekwa Michenzani *block* No. 9 ghorofa ya mwisho ya nne nafikiri wakauziwa kwa milioni 17 wakati sheria hairuhusu

nyumba za Majenzi kuuzwa, wakapelekwa milioni 17 ofisini wakalipa na vibali vyote ambavyo hivi hapa ninavyo.

Matokeo yake huyu aliyekwenda kununua ni mwanamme Harish Jiva na aliopewa fedha hizi ni ni Talib na Rashid, watu hawa ndio waliopokea pesa hizi ofisini. Badala ya hapo yule aliyenunua mwanamme kampeleka mama yake kumkabidhi ile nyumba, kumkabidhi ile nyumbwa mama yake akasema mimi hii siwezi kupanda juu mimi ni mbovu wa miguu. Mhe. Mwenyekiti, cha kusikitisha kabisa yule ambae aliyenunua nyumba yule Harish ambae ni Muasia akawapigia tena wale jamaa simu kama bwana hii nyumba mama yangu hawezi kukaa na sheria na masharti hayajui. Wale wale wakamwambia ngojea tutakutafutia mteja baada ya muda kapigiwa simu na mwanamke nataka nyumba akenda kuwaonyesha wakaagana vizuri akaambiwa njoo siku ya pili. Kwenda kule siku ya pili mmoja kati ya wale alienda na Mkurugenzi na mapolisi wakawavamia wakamwambia tunakumata wakamnyang'anya Mkataba nyumba kanyang'anywa ameshapewa mtu mwengine milioni 17 zake hajarejeshewa mpaka leo. Wanabaki kumwita tu wanamfuata mjini wanamuita ofisini tulia tunakufanyia mambo yako.

Naomba sana Wizara suala hili mimi kwa kanuni ya 111 kifungu (1) na (2) naomba sana tuunde Kamati Teule kuhusu hoja hii na hawa wameshafanya haya zaidi ya suala moja hili moja ninalo mkononi, Mhe. Waziri naomba aje anipe majibu hawa watu wanatumia Wizara yake kwa njia za utapeli kudhulumu watu fedha kama hizi na kwenye mkataba huu bahati nzuri haujaorodhesha kifungu ambacho kinasema nyumba ile hairuhusiwi kuuzwa nimekisoma chote, kimo kinasema usimpe mtu mwengine na usikodishe. Lakini yeye yule mtu hajawahi kununua nyumba hajui masuala ya kwamba nyumba zile haziruhusiwi kuuzwa na wao waliouza ndio watu wenye Wizara ile ndio waliouza ile nyumba kwa huyu mtu naomba sana nije nipate jibu kwa suala hili. Kwa sababu kwenye Wizara hii mimi

nina hoja za Kamati Teule tano nataka nizilete kwenye Wizara moja nikianzia na hii moja.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nakwenda kwenye suala la *Airport* suala hili nina *document* nyengine hii hapa ya *Airport* ambayo fedha za mwanzo zilitakikana Dola milioni 70,400,000/= Bilioni 150 takriban hii ilikuwa mwaka 2009, mwaka 2012 Dola milioni 11,828,000 bilioni 25 kwa Shilingi, 2014 Milioni 46,518,000/= ni sawa sawa na Bilioni 100 shilingi Jumla Dola 128,747,000 zilizotumika mpaka hivi sasa hivi ni sawa sawa na Bilioni 288 Tanzania shilingi. Kwenye kitabu chao sasa hivi wanaomba bilioni 144 nyengine za kuendeleza hii *Airport*, kifungu cha hiyo wanayoiomba nimeandika hapa ambacho ni 0000P015 bilioni 20 zitatoka SMZ bilioni 124 zitatoka Benki ya *Exim Bank China*. *Airport* hii inakopeshwa hizi fedha kwa kulipa deni la miaka thalathini Serikali yetu inatakiwa ilipe *within 30 year* deni hili, *Airport* hii imefeli waliosababisha hasara wapo kwa nini vitu hivi haviletwi wazi tukaelezwa nani kafanya hivi vitu mpaka Serikali imeingizwa *shot* kama hii.

Mhe. Mwenyekiti, *Airport* hii itasimamia bilioni 450 karibu shililngi mpaka itakapokwenda hivi sasa na pengine isimalize, *Airport* hii kwa mujibu wa udogo wake ndio ghali dunia nzima. Mimi naomba nilete hoja ya Kamati Teule kwenye suala la *Airport* na kifungu hichi nakizuia ambacho nilichokitaja hapa hii 0000P015 nakizuia sikubali kwa sababu *Airport* kumesababisha uzembe Serikali imeingia deni kubwa, na cha kushangaza zaidi kwamba walimpeleka Mhe. Rais miaka miwili nyuma nakumbuka hata kabla sijawa muwakilishi kwenda kuzindua na akamuahidi kwamba muda mdogo tu *Airport* itaanza kazi kwenye TV wakati huo ata mimi si Mwakilishi. Leo kwenye kitabu chao hichi *page* ya 18 kifungu No. 55 kinasema kwamba asilimia 39 ndio kwanza *Airport* ile ipo inamaanisha kwamba walimdanganya Mhe. Rais viongozi wote ambao aliokwenda nao.

Mimi ninachosema kwamba kwenye suala la *Airport* nataka tuunde Kamati Teule bila ya malipo maana yake tusije tukaletewa sababu kwamba fedha zitakuwa kuna mtu anataka kulipwa, tuko tayari kujitolea bila ya malipo lakini haiwezekani *Airport* ile ikasimamie bilioni 450 mpaka hivi sasa na nyengine wanazihitaji fedha kifungu hichi kwa fupi sikipitishi mimi.

Mhe. Mwenyekiti, nakwenda kwenye suala la barabara, barabara za Zanzibar mbovu na cha kushangaza zaidi kwa nini tenda zote anashinda huyu mtu anayeitwa *MECCO* kuna usiri gani hapa nani kuna mkono wake ambaye mtu huyu anapewa hizi tenda, tunataka tuje tuelezwe na hii nataka iundwe Kamati Teule suala hili liundwe Kamati Teule barabara mbovu. Serikali tumeona tuna karibu bilioni 150 hapa zinataka kuchukua kwenye masuala ya barabara barabara leo zimenyesha mvua hakuna hata njia moja ya Zanzibar ukiacha ile ya Nungwi iliyojengwa sijui na Wazungu na nyengine mbili tatu zilizobakia zote zilizojengwa na hawa Ma-*contractor* ambao Watanzania wazalendo ni mbovu na zile picha ambazo wanatuletea humu ndani ya ukumbi za kutuonyesha barabara kwamba ziko kwenye kiwango, zile ni picha ambazo wanazitengeneza wenyewe tu wanaambiwa kachimbue sehemu fulani piga watu wanapewa fedha wana watu wanaweka mambo sawa, lakini uhalisia barabara mbovu. Tunataka tuje tuelezwe watu wangapi ambao wana-*bid* kwenye tenda wanapewa na tunataka tuje tujue *MECCO* au kampuni yoyote ambayo iliyojenga barabara ina *guarantee* ya miaka mingapi inaipa Serikali barabara pindipo itachimbuka au itaharibika watalipa na wanaweka *security* bei gani kwenye suala ambalo itakapotokezea *any damage* linakuwa liko *solved* kwa mujibu wa sheria za *International.*

Mhe. Mwenyekiti, Hapa tunaona kuna kitu kinasema *warrant terms* na kuna kitu *warrant period* tujue *warrant period* kampuni yenyewe inapewa miaka mitano au kumi, *guarantee* au vipi na inaweka bei gani *security* kwenye suala ambao litatokezea lolote

kwenye masuala haya ya uharibifu wa njia. Mimi kwa muono wangu na ramadhani hii haya masuala hayako bure tunafahamu na tunawajua. Masuala ya kwamba tunapeleka nchi kwa kujuana kuwa wa fulani apewe mtu fulani lakini matokeo yake tunaua nchi halafu tunakuja kuambiwa humu ndani kwamba wewe si mwenzetu hicho kitu hakipendezi, mimi mwana CCM na hao wanaonitafsiri hivyo wao ndio ma-CUF na hapa wamekuja tu. Mhe. Mwenyekiti, wanaosema hivyo ukija kuwachunguza siku ya siku basi wao hata sio Wazanzibari wala sio CCM wa kweli.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitaendelea kusema suala la *Airport*, suala la barabara, suala la nyumba ambazo nimezitja hapa nataka ziundwe Kamati Teule, nakwenda kwenye Kamati Teule nyengine suala la *fire* ambazo zimennuliwa mbili na Wizara hii. Mhe. Mwenyekiti, Wizara hii imenunua *fire* mbili nikiacha zile za vikosi nilizongumza kipindi cha nyuma zilizogharimu bilioni tatu na milioni mia nne hizi *fire* zimenunuliwa kutoka *South Africa Scania* zimenunuliwa na Wizara hii bilioni tatu na milioni mia sita *fire* mbili kwa mujibu wa maelezo yao niliyopewa *airport* kama mjumbe wa Kamati mimi nilikuwepo. Nataka kujua fire hizi bilioni tatu na milioni mia sita, *fire* za aina gani zifike gharama ya bei hii na kama kwenda kununua vitu hivi kwa nini vikanunuliwe *South Africa* visende kununuliwa kwa bei ndogo huko kwenye kampuni yenyewe Norway inapotengenezwa zilipokuwepo *fire* zile hazifiki kiwango hicho. Naomba na suala hili tuunde Kamati Teule kwa mujibu wa kanuni 111(1) na (2) page ya 96 tuendelee kwenye Kamati Teule suala hili la *fire* mbili sijaridhika nazo haziwezi kufika *fire* mbili bilioni tatu na milioni mia sitahicho kitu *impossible* hakiwezekani kwa mawazo yangu mimi.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ninalokwenda nalo kuna wafanyakazi ambao wamefukuzwa au wameondoshwa kwa njia za kisiasa tu *Airport*, naomba nikutajie mmoja anaitwa Sadala Juma Abdalla ambaye huyu Mabodi na kuna mwengine huyu Borafya yuko wapi, kuna mmoja humu ndani maana yake nina karatasi nyingi

humu anaitwa Soud Borafya Mtumwa, hawa wameondoshwa kwenye taasisi ya *Airport* kwa masuala ya kisiasa tu wako zaidi ya miaka kumi na tano na wengine miaka kumi na mbili ndani ya Wizara ile, lakini vitu vidogo ambavyo wamefanya wao wakosee wameondoshwa kwa njia ya kisiasa naomba na suala hili tuliundie Kamati Teule tukachunguze sababu zipi zinazofanya watu waondoshwe kwa sababu ya masuala ya kisiasa wafanyiane chuki, hii nchi sote ni Wazanzibari sote ni Watanzania lazima tupendane tusitafutiane masuala ya kisiasa tukataka kumfukuzisha mtu kazi, ikiwa chama cha *CCM*, ikiwa *CUF*, ikiwa *CHADEMA* tusifike kwenye masuala ya chuki, lazima tupendane mtu kwenye Chama chake atapenda Chama chake lakini tusifike kumkosesha mtu kazi kwa sababu ya siasa. Hawa watu niliowataja wameondoshwa kwa mazingira ya kusikitisha na *document* zote ninazo walizojibishana walizojibu zikafika mpaka kwa Katibu Mkuu Kiongozi Ikulu kapelekewa nakala ipo hizi hapa.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo nalizungumza kwenye Wizara hii kuna watendaji 8 ambao walihamishwa kutoka Shirika la Meli kupelekwa Mawasiliano Wizarani hawana kazi yoyote wamepelekwa wakakae chini ya miti tu wanalipwa, mshahara unatoka Shirika la Meli, likizo linatoka Shirika la meli lakini wao wako Afisini Wizara ya Mawasiliano hawana kazi yoyote na hawa majina yao ni Ramadhan Haji, Haroun Iddi, Hafidh Khamis, Hasnuu Masoud, Abdalla Abeid, Khadija Muhana, Rehema Adnani na Khadija Juma.

Utaratibu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nimuombe tu ndugu yangu wale wafanyakazi wamesharejeshwa kwa niaba ya kamati nimuombe tu afute kauli hiyo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub sijakusikia rejea.

Mhe. Mwenyekiti, Mjumbe aliyekuwa akichangia nimesimama kwa kanuni ya 63 tu wale wafanyakazi aliowataja orodha washarejeshwa kwenye kazi zao nimuombe radhi tu kwa hilo afute kauli hiyo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe taarifa ndio kama hiyo umesikia.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mimi nimemfahamu kwamba katoa taarifa washarudishwa ni vizuri lakini sijui kwamba nimuombe radhi au nifute kauli basi suala hili.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub sijakupa ruhusa kuzungumza nilimpa nafasi ni Mheshimiwa Mjumbe.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Naondosha kauli ya hili suala la wafanyakazi wanane ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Kwa sababu Mhe. Jaku ni mmoja ya mzee wangu kaniliea sasa na hii ramadhani nampa heshima yake.

Mhe. Mwenyekiti, nimefika kwenye suala hilo nikaambiwa kwamba lishakuwa lakini sasa niende kwenye masuala ya njia, tunachoomba Wizara ieke alama za barabara ikiwa hapa kuna mto, kuna njia haipitiki, kuna *speed limit* kama 50 kama ilivyowekwa kwa Mhe. Rais maeneo ya Mazizini lakini ubaya zaidi kwamba zile herufi ndogo kuna watu wengine hawazioni, tunataka tuweke *sign board* kubwa hasa barabara za shamba watu wengi wanasumbuliwa tukiwemo sisi wenyewe, wazungu na maaskari kukaa na vikamera halafu matokeo yake *sign board* hazipo utamlaumu nani na utamkamata nani. Kwa ufupi lile kosa linakuwa la polisi sio la watu wa kawaida raia hakuna *sign board* kutoka mwanzo mpaka mwisho halafu unakuja kumpiga mtu kamera unamwambia kwamba hili suala umevuka *speed* nani atafahamu wakati hii nchi ya *Tourism Country* ya watalii. Mtalii akifika *Airport* haambiwi kama huku kuna hivi kuna hivi lazima

kuwekwe alama watu wafahamu na hili litaepusha rushwa litaepusha migogoro mikuu katika masuala ya *traffic*.

Mhe. Mwenyekiti, suala langu jengine kwenye Wizara hii yapo magari ambayo yanafanya kelele njiani wanatia maekzos sio yao, vespa wanatia ekzos sio yao, ile milio inayolia sio ya honda halisi wala sio gari halisi. Ningeomba sana Wizara ikapiga marufuku *otherwise* iwe gari yenyewe *original* yake kutoka kwao imekuwa *imported* kwamba inafanya sauti si tatizo, kwa sababu ziko gari ambao zinafanya zogo, lakini sio ambazo tunazo Zanzibar za hawa *T. one* na watu wengine ni vitu vya uongo, naomba sana zipigwe marufuku wazikamate ikiwezekana wakikataa hata zitaifishwe.

Mhe. Mwenyekiti, suali langu jengine liko kwenye *speed limit* kwa masuala ya hawa abiria madereva wa daladala wako tayari kuua kuua watu 20 kwa shilingi mia tatu, wanagombaniana barabarani wanafukuzana kwa kuharakia abiria mmoja tu, ningeomba sana ziwekwe faini kubwa sana na ikiwezekana gari zizuiliwe hata mwaka mzima kwa mujibu wa Sheria iwepo, kwamba atiwe adabu tu. Leo tunaona ajali kubwa inasababisha na dereva kwa kufukuzia shilingi mia tatu au shilingi mia tano.

Mhe. Mwenyekiti, kuna jambo jengine kwa sababu hii Wzara nakwenda mbio mbio kubwa suala la Uhifadhi wa Mji Mkongwe bajeti iliyowekwa kwenye Mji Mkongwe ni ndogo bajeti iliyokuwepo milioni 503 kwa ajili ya kuhifadhi Mji Mkongwe, leo tuagalie Mji Mkongwe ule umekwisha umekufa karibu majumba asilimia 70 ya majumba yale mabovu. Sasa inakuwaje milioni mia sita, milioni mia tano na hamsini kwamba itatosheleza kazi hizi wakati vitu vyengine vimewekwa bajeti kubwa? Hili kwa kweli linasikitisha Mhe. Mwenyekiti, bajeti ya Mji Mkongwe ili kuweka majumba yale katika *candition* nzuri unahitaji fedha za kutosha ili waweze kukamilisha.

Lakini ninachoendelea Mhe. Mwenyekiti, barabara yangu ya Chaani humu mimi nimeshaiona lakini wananchi wangu sasa hivi wengi wao wanaumwa na vifua, wana pumu, hawaoni vizuri kwa mavumbi, hili suala wananchi wangu wanaumia kuanzia huko Gamba huko mpaka ukija maeneo ya Kikobweni, kwa ufupi wananchi wameathirika hasa watoto wadogo wanaokaa mazingira ya barabarani. Leo barabara hii tunaambiwa itaanza Bububu wakati ilipokufa zaidi ni maeneo ya jimbo langu ndio imekufa. Lakini cha kusikitisha zaidi Mhe. Mwenyekiti, barabara zote za Zanzibar wakisikia kiongozi mkubwa anakwenda kwenye barabara hiyo *wallahi laadhim* na Ramadhani hii inatiwa kifusi au hapitishwi njia hiyo. Ukweli unafichwa kwa nini wasipitishwe viongozi kwenye njia mbovu kama ile na wao wakaona hali halisi mnawapangia njia nyengine au mnakwenda kuziba mbio mbio, wananchi wangu wanaumia na wanalalamika sana kuhusu suala hili mimi mwenyewe binafsi nalalamika dhahiri kwenye njia hii.

Ningeomba sana ujenzi huu utakapoanza uanzie Chaani kuanza Gamba mpaka kuja Chaani Kikobweni ndio waingie Bububu. Njia ya Bububu inapitika njia ya chaani haipitiki wazee wameumia wanaumwa na macho, vifua matatizo matupu sasa hivi *complain* nazipata mimi muwakilishi sikatai kuzichukua lakini inakuwa siwezi kuzihimili.

Mhe. Mwenyekiti, suali jengine ukienda kwenye Wizara hii *Airport* kuna mashine pale ya kuweka *cover* mabegi mashine ile uksafiri ukitaka begi lako litiwe *plastic* lisichunike unachagijiwa elfu kumi na saba kwa begi moja. Ningependa kujua mashine ile anaemiliki nani au ipo pale kwa niaba ipi. Kwa sababu nchi zote mashine ile haizidi elfu saba au elfu nane kutia lile *plastic*. Kwa nini Zanzibar nchi ambayo ya wanyonge nchi ambayo ndogo imewekwa shilingi elfu kumi na saba kwa begi moja au kuna mtu yake kaipeleka pale anataka kufanya mtaji. Ningependa kujua wanaruhusu mtu mwengine apeleke kwa bei nafuu au vipi kwa sababu inawezekana kaweka mtu mmoja ndio maana anafanya

anavyotaka kwenye bei kama hiyo. Bei elfu kumi na saba kwa begi moja kuweka *plastic* ni bei kubwa sana, hata kwa wageni ni bei kubwa. Tunasafiri siku zote bei haizidi elfu nane na huko kuna mashine za ghali zaidi wanaweka vitu *quality* zaidi kuliko mashine iliyokuwepo pale.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ningeomba sana *Airport* waweke watu wa kubeba mizigo leo kuna watalii kuna wazee wetu kuna sisi wenyewe wengine pengine wabovu wa migongo hatuwezi kubeba mabegi, leo mtu anabebeshwa mabegi wakati wa kushuka. Pale VIP *lounge* naona tabu mimi hata kumbebesha mwanamke begi nabeba mwenyewe mabeki wakati mwengine ekeni ma-*bouncer Airport* wa kubeba mabegi atapewa *trip* tu au kama kuna sehemu ya kulipa ikalipwe elfu mbili au elfu tatu apate mtaji wake mtu. Nchi nyingi zipo zipo watu ambao wanabeba mabegi unakwenda kulipia elfu tatu, elfu tano wanabeba mabegi mpaka kwenye *check in* au mpaka kwenye gari. Kwa nini Zanzibar mfumo huo hakuna tunasumbua watalii, tunasumbua wazee wetu na sisi wenyewe. Leo tunakwenda kumbebesha pale VIP au tunawabebesha wanawake ndani tunawabebesha mabegi ya nini inaleta picha nzuri wapi mimi nabeba mwenyewe.

Mhe. Mwenyekiti: Una dakika moja.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri nimetaka Kamati Teule tano, kiti chako ndicho kitachochagua tuanze na ipi, mimi katika vifungu ulivyovizungumza suala la *fire*, suala la *Airport*. Suala la *Airport* najua halina jibu, jibu lake litakalokuja hapa sio la sahihi kwa sababu vitu tunavyo hasara kubwa imepatikana watu kwa mujibu wa sheria ya *International* anapokwenda *against the law* au sheria anapofanya *constructer* au *construction* yoyote ikifeli anatakiwa ipigwe faini nije nielezwe alilipa vipi yule mtu kalipishwa na leo tunakuta Benki ndio kwanza inakwenda kukopwa fedha nyengine tuzipitishe.

Mhe. Mwenyekiti, wizara hii siipitishi hata asilimia mia moja nasubiri jibu langu na lawama zangu simlaumu Mhe. Waziri wala Naibu Waziri wote wapya ndani ya Wizara hii, lakini nataka nipate majibu ya sahihi kabisa.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa muda wako umemaliza.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy : Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe sasa nitamwita Mhe. Jaku Hashim Ayoub na baadae atafuatiwa na Mhe. Asha Abdalla Mussa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nami nikushukuru kunipa nafasi hii na Mwenyezi Mungu akitujaalia kuwa tuko katika Ramadhani ya tano hivi na tuendelee kumshukuru Mwenyezi Mungu kutii amri zake na kama msemo unaosema *Manswama Ramadhan wa Ihti sabah* mwenye kufunga Ramadhani ategemee malipo kwa Mwenyezi Mungu na dhambi zake kusamehewa.

Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza Waziri rafiki yangu na Naibu Waziri wake na Watendeji wake akiwemo Katibu Mkuu wa Wizara hii na baadhi sio wote. Mhe. Waziri ile nia yako Mungu akitujaalia huko mbele usije ukaiondosha panapo uhai na mpangaji Mungu, Mungu si athumani na tuombe uhai sisi wengine pengine *inshaallah* tukaa tuangalie mbele huko, nia hiyo usije ukaiacha utendaji wako tumeuona. *(Makofi)*

Mhe. Waziri Bajeti yao hii kama utaitekeleza hichi kitabu ni Waziri wa mwanzo kupigiwa mfano humu ndani maana yake tukae pia tukaihoji hii Mhe. Waziri mie naona huruma sana katika Mwezi huu Mtukufu. Hii bajeti kama itatekelezeka pana

kazi kubwa na mengine sijui yameandikwa saa ngapi humu ndani kwa hivyo sitaki kuichambua, lakini kama itatekelezeka bajeti hii ni waziri wa kupigiwa mfano humu ndani na kwa kukwambia nia yako tuendelee huko mbele kunako uhai. *(Makofi)*

Mheshimiwa baada ya utangulizi huo nije katika Shirika la Bandari niendelee kumpongeza Mkurugenzi Mkuu wa Bandari Abdalla Juma, kazi alioifanya katika Ukurugenzi wake tumeiona na Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein hakukosea kumpeleka pale alijua ndipo alipotokea ndio mzizi wake ulipo, sisi sote mashahidi. Kwa upande wangu msongamano wa makontena sasa hivi umepungua na lile eneo la Bwawani naona aendelee kulitumia vile vile, pale hapana dalili ya ujenzi aweke kontena zake kama kawaida Serikali ni hii hii moja. Zaidi eneo la abiria juzi wameweka *screen* pale mbili jambo la kupongezwa sana tumpigie makofi Mheshimiwa, kazi aliyofanya pale siku zote Wajumbe tulikuwa tunalalamika humu ndani amefanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa kuna kilio kidogo tu pale *slip way* nacho kifanyie kazi katika kukaa meli lakini jengine kuhusu vifaa umenunua Mheshimiwa kwa pesa chungu nzima Mkurugenzi pana hii dola 250 kwa kontena waliochukua wenye mameli au wakala wa meli, sasa kama umenunua vifaa hivi wafanyabiashara wanalalamika dola 250 kwa kontena moja si pesa kidogo Mhe. Mkurugenzi DG hili liangalie na wakati mwengine msongamano unakuwa haupo hizi pesa hazirudi Humu umenunua vifaa kwa pesa chungu nzima jambo la kupongezwa, lakini hizi dola 250 kila kontena inaumiza, na wakati mwengine msongamano haupo kwa hili nalo lifanyie kazi nafikiri Mhe. Waziri umenielewa utakaa na Mkurugenzi ataeleza yeye ni msikivu.

Baada ya hapo Mheshimiwa nije katika katika Shirika la Meli. Mheshimiwa kama tumepata mtihani Meli yetu ya M.V Mapinduzi II tumepata mtihani tumenunua kwa pesa chungu

nzima utendaji wake mtihani. Dola milioni 33 ulikuwa hupo hapa Mhe. Waziri nilihoji mimi katika kipindi kilichopita miaka mitano ile, dola milioni 33 unanunua meli tatu mpya, leo meli ile pale sijui kama inafanya kazi wiki ya pili sasa, ilikaa muda inasubiriwa kutoka wapi, dola milioni 33 nilisema mimi Kampuni ya Azam haifiki wakati huo kabla hajaongeza meli mbili yote nzima. Pesa za walipa kodi bajeti zimekatwa humu za wizara chungu nzima ,ndio nilimwambia Mwanasheria mikataba aiangalie. Siku zote serikali itakula hasara kwa mikataba. Meli ile pale dola milioni 33 leo ukienda hapo Mnazi Mmoja dari imeshaanza kuja chini Hospitali Kuu inayotaka kuitwa ya Rufaa, wewe dola milioni 33 *convert to shillings*, shilingi ngapi sijui trilioni ngapi. Imefanya safari imekwenda Comoro sijui utafiti gani uliofika kule, awaulize Mhe. Waziri watendaji wake haikufunga gati Comoro meli ile imepakia gari, imerudi na gari. Abiria 26 yamezungumzwa kwenye kitabu jambo la kuridhisha ni kweli *crew* wangapi, *crew* wengi walikuwa abiria waliokwenda. *(Makofi)*

Mhe. Waziri afuatilie mwezi wa Ramadhani huu kama nimekosea unaweza kuja kumkosoa rafiki yangu mimi, lakini usijaribu kwenda hivyo, imekaa pale sasa hivi. Kwa hivyo, hilo liangalie imepakia gari, imekwenda Comoro meli haikuweza kufunga gati, imekwenda kufanya kazi gani. Safari hizi kubwa sifikirii zifikirieni na dude linakunywa mafuta khatari ya kiama, *consumption* ile meli ni kubwa biashara zipimwe watafutwe wataalamu.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze tena Mkurugenzi wa Uwanja wa Ndege naye nitakuwa sijamfanyia haki Said Ndugugani kapteni huyo. Kipindi cha miaka mitatu au minne nyuma mimi mmoja katika niliyempa kazi humu ndani siku zote tunakorofishana hoja baada ya hoja akasimama anakuja, waziri aliyekuwa wa wizara hii alifika humu hee, hata mengine hayasemeki kilichomkuta humu ndani, Ndugu Said kazi amefanya sisi ndio shahidi, uwanja wa ndege tunauona hivi sasa ulivyo. Sizungumzii jengo jipya

lililojengwa kwa gharama duniani hakuna siligusi hilo, kazi Ndugu Said amefanya tumeiona, mimi mmoja niliyekuwa nikipiga makelele humu ndani amerekebisha kwa kiasi kikubwa "mnyonge mnyongeni haki yake apewe", Kepteni amefanya kazi kubwa Sheikh Said uwanja wa ndege. Sasa hivi ndege masaa 24 *run way* ya kuridhisha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije katika Mji Mkongwe kuhusu *hall building* na eneo la Darajani zima. Mheshimiwa hapa pana mtihani naendelea kuzungumza tena na tena na iko siku nitaondoka tu hapa duniani wakati wowote. Mkurugenzi tumeona majengo mengi yakifanyiwa marekebisho *Hayatt Park*, Sinema ya Malindi ile pia imefanyiwa pia marekebisho leo inataka kuondoshwa skuli Vikokotoni jengo la asili baada ya kusema tunataka kuendeleza jengo lile akili gani jamani tunafanya hii, inabidi wanafunzi wa Mji Mkongwe leo wasipate skuli, tukishavunja ile keshokutwa tuvunje Haile-se-Sellasie na Ben-Bella ndio mwelekeo wake ndio huu. Tuangalie huyo mfanyabiashara anayetaka kujenga pale kama hakupata elimu atafanya biashara, elimu mwanzo.

Mkurugenzi Mkuu wa Mji Mkongwe aishauri serikali asione haya, asiwe kama Mkurugenzi wa Mipango Miji. Serikali inataka kushauriwa haikufuata ushauri wa Mkurugenzi basi lakini umeshaeleza ukweli historia itabaki historia kujiandika, leo kweli tukaondoshe skuli zile wanafunzi wa Mji Mkongwe wakasome wapi Hamamni na Vikokotoni, skuli zenye thamani kama ile haielekei, na Mkurugenzi kabla ya ujenzi haujaanza nakumbuka anaweka tangazo wananchi waje watoe maoni yao *Shawl Building* halikutolewa tangazo lile kwa wananchi tumetumia nguvu lakini ndio serikali mkono wake mkubwa. Mwanasheria ishauri Serikali usiogope.

Mhe. Mwenyekiti, imekuja hoja ya umeme humu ndani nikaonekana mimi mbaya, historia imejiandika Mwanasheria

asiogope nilimwambia yeye wa kumi na mbili au kumi na tatu wameondoka wengine watakuja, ishauri Serikali Mwanasheria asiogope ndugu yangu utaitia hasara sana serikali, hali yenyewe tunaijua sisi hiyo misaada ndio tunaiona, ishauri Serikali asiogope kuwa anapanda Prado mimi napanda Vitara ndipo tulipoanzia. Serikali mikataba ya uwanja wa ndege, mkataba wa Bwawani, barabara hizo mimi kazi yangu kusema tu, kwa skuli zile za historia Mkurugenzi akija akitoa kibali pale sijui, hii Serikali isingekuwa madarakani bila ya kuwepo wananchi tungetawala nini serikali jama?

Wananchi ndio Serikali tufike tuwe na moyo wa huruma sio mdomo tu na vitendo. Leo imekuwa *mall* pale muhimu kuliko skuli zile, Michenzani wanataka kuweka *mall*, Bwawani *mall* na Darajani *mall* huku wanasema wanataka kuondoa msongamano wa watu, huku wanataka kuzidisha mlango wa mbele wa nyuma umefungwa wa nyuma unafungua vichekesho vikubwa. Mkurugenzi nakuomba kashauri Rais wetu ni msikivu sana tena sana, msikivu kweli kweli na anawahurumia wananchi wake na anawajali. Tumeona kanunua meli kwa sababu ya safari za Pemba, tumeona Sekta ya Afya kafanya nini Rais wetu. Mimi nafikiri akenda kushauriwa hawezi harudi nyuma kwa suala hili. Itafutwe njia nyengine ijengwe japo *mall* ndogo, nyembamba skuli zibakishwe mimi hoja yangu zile skuli zibaki tafuteni njia nyengine ya eneo lile.

Mhe. Mwenyekiti, hapo hapo Mji Mkongwe Mkurugenzi wa Mji Mkongwe mji sasa hivi hata serikali yenyewe nafikiri hawautaki sasa hivi Mji Mkongwe nasema kwa sababu. Serikali imefuta jimbo la Mji Mkongwe hakuna umuhimu sana Mji Mkongwe kuwa na nguvu kama vile, sasa tupunguze madaraka Mji Mkongwe ushauri huo sasa Mhe. Waziri sikiliza vitu hivyo. Ardhi yetu ni ndogo kutoka Bwawani pale barabara ya Malindi, Darajani mpaka Mnazi Mmoja chukueni kule eneo la Mji Mkongwe huku kuwacheni, mnashindwa kusimamia majukumu majumba

yanaporomoka tu watu wanakufa. Kutoka njia ya Bwawani mpaka Mnazi Mmoja barabara imegawa huku kubaki Mji Mkongwe hichi tulokuwa nacho, tunashindwa kusimamia halafu unataka kuongeza tu iwe kama hati za kiarabu ukiandika unavutia kwako tu kiarabu.

Waziri ushauri huo uchukue leo ukishuka bandarini Dkt. Ali Mohammed Shein siku moja alisema katika sherehe pale Maisara za Umoja wa Vijana, ukeshashuka tu bandarini unaona majumba yanavovutia bandarini pale ardhi yetu ni ndogo, leo eneo la Mji Mkongwe, Mhe. Nadir alisema bajeti waliopewa ni ndogo na ndogo kweli. Sasa leo liachiwe huku Serikali Mji Mkongwe jimbo ishalifuta halipo, sasa lina kazi gani?

Mheshimiwa nije katika ujenzi unaotaka kufanyika Michezani Mhe. Waziri pana Ofisi pale Michenzani ile ndogo ya chini Mhe. Waziri kwa hekma zako na Busara na mwezi huu Mtukufu wa Ramadhan mimi nikuombe wale watu mna sekta karibu 5 mle, kuna Bodi ya Usajili kuna Bodi ya Majengo ingawa wengine unawateua hata sifa hawana Mhe. Waziri.

Lile jengo wameamnbiwa tarehe 15 waondoke, lakini na mimi siamini Serikali kama itafanya jambo pale kwa muda huu, kwa hivyo pale hawana pa kwenda wale watu ndio nyie Serikali kwa Serikali tusaidiane wale wabaki, mpaka tuje kuona mchoro hapa. Mhe. Mwenyekiti, nilipata shida sana mie miaka 5 iliyopita katika Wizara ya Afya humu ndani kwa kuwaonea huruma wananchi, wakati huo Wizara hiyo inaongozwa na Mhe. Juma Duni, wananchi pale nilisema wanaokwenda kuangalia wagonjwa wao hapapikwi pilau wala biriani wala hapatolewi sadaka wanaroa, nikagombana na Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban akatoa eneo na Mkurugenzi wa Mji Mkongwe hakubisha kufikiria wananchi. Eneo mpaka leo halijajengwa mimi ndio nnohangaika ramani imechorwa mwaka wa 7 huu mwisho nikataka kutafuta njia wafadhili nijenge mimi nikakataliwa kupewa ramani.Kesho kutwa

panapo Wizara ya Afya si mbali Mungu akituweka hai, hasa huu ni utaratibu gani mpaka leo hatujafanya chochote, kwa lile jengo pale mpaka tuone michoro hapa na waondoke wale pana taasisi (4) pale, pana pesa zinapatikana pale ndio lile suala nilozungumza na Mhe. Omar Haji Kheir jana hapa nikaja nikaoneka Kanuni tunashindana, hamjawa tayari kujenga kuvunja rahisi kuliko kujenga. Waache kwanza pana taasisi (4) pale utawapeleka wapi. Mheshimiwa utakapokuja kwa umakili wako ninavyokujua mimi hili utaliachia haielekei.

Mhe. Mwenyekiti, kama kweli hii ripoti aliyoiandika Mhe. Waziri au kama alivyoisoma hapa nataka kumueleza tusiwe na huruma kwa mdomo tu, vitendo vinatakiwa ukurasa wa 9. Shirika la Nyumba limepewa jukumu la kusimamia na kuratibu maswali yote yanayohusiana na ujenzi na uuzaji wa ukodishwaji wa nyumba au kibiashara. Kuna watu wangapi wanalalalimika nyumba za Serikali mmeshindwa kuzisimamia na nyengine ziko chini na anayejenga mtu wa hapa hapa pao imekuwa kama nyoka wa mdimu. Nyoka wa mdimu hukaa kwenye mdimu yeye hana kazi nazo na ukenda kuchuma anakurukia. Waziri tunataka vitendo sisi tunakuamini, majumba mengine hamuwezi kujenga pesa hazipo, ndio nilipokwambia hii bajeti yako kutelezeka ni hatari, huku mwisho ukurasa 45. Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali imeamua kununua meli ya mafuta na meli ya abiria na mizigo jumla Tsh. bilioni ishirini vichekesho hivi. Mhe. Waziri hiyo boti hasa ya uhakika ya tanga huwezi kufanya kitu hichi, hivi vichekesho. bilioni ishirini huo mkuko hata hauwezi kuanzan nikakwambia kusema rahisi kuliko kufanya sasa hizi nyumba watu wanahangaika, tena wanajenga hapa hapa pao. Humu mmeandika mngesema vitendo havipo, mdomo rahisi au domo jumba ya maneno.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika chombo za ZMA usajili wa meli.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa una dakika tatu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, ZMA imesajili Meli humu hapa na Ofisi mbili kule Dubai moja ikafutwa ikatengenezwa nyengine, hebu watueleze katika Meli 146 waliosajili, sijui tuna Kanuni, kila meli Wazanzibari kama watano watiwe, sikumbuki uzuri hapa waziri kidogo aje anielimishe ndio vile nilivyokwambia elimu yangu mimi ni ndogo, ajira hatuna meli kule kwanini Wazanzibari wasitiwe angalau kila moja wawe vijana watano. Meli hizi tangu 146 tungekuwa tuko wapi sisi? Au ndio ile huruma yetu ya mdogo vitendo havipo. Tunasajili meli si hivyo kulikuwa na mkataba nafikiri kama hivi, kila meli Wazanzibari watano wawemo leo wametiwa wageni watupu humu ndani. Hasa njia nyengine hizi riziki tunazipata tunazipiga teke.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nije kuhusu barabara mwaka jana Mhe. Waziri uliniahidi huku ndani kuwa UUB, mimi hawa siwapongezi niwape pole sana UUB katika watu wanaopata shida hawa sana tena. Mzigo mzito mbebeshe mnyamwezi, hawa vijana kazi wanayoifanya UUB hakuna mfano. Tumenesha pia mkataba ule umeshindwa Serikali imefutwa, hiyo tungeiweka kazi walioifanya Ungujaukuu hakuna chochote kilichoengezwa humu, vifaa vya kutendea kazi *spanner* mkononi.

Mhe. Mwenyekiti, Ilani ya Chama cha Mapinduzi, kuna barabara Uzini mara mbili imeshaahidiwa kule, hakuna utekelezaji wake nitahitaji maelezo. Mhe. Mohammed Raza alikuwa akipiga kelele mwenyewe na wala mimi hakunituma yeye.

Lakini nyengine kuna sehemu inaitwa Fuoni kuelekea Fumba, pana barabara iangalieni kule kibondeni, kuna wapiga kura wetu kule. Mhe. Mwenyekiti, nisije nikajisahau na mimi mwenyewe hali yangu jimboni maafa yaliyonikuta naomba nisaidiwe angalau vifusi, nisiwe natetea watu tu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub, muda wako umemaliza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Mwenyekiti: Anayefuata ni Mhe. Asha Abdalla Mussa na baadaye atafuatiwa na Abdalla Maulid Diwani na baadaye na Mhe. Zulfa Mmaka Omar.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi hii ili kuweza kuchangia hotuba hii ya Mapato na Matumizi ya Mwaka 2017/18 ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirisha.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi niungane na Wajumbe wenzangu kwa kuiunga mkono hotuba hii kwa asilimia 95 mpaka nipate maelezo ya kina juu ya haya nitakayoyazungumzia hapa. Kwanza niipongeze sana Wizara hii ya Ujenzi, nikianza na Mhe. Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wake wote. Pia nimpongeze sana Mhe. Rais wetu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ahadi mbali mbali alizozitoa na nyengine kuzitekeleza.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze na programu ya masuala ya barabara. Katika hotuba yake Mhe. Waziri ameelezea utekelezaji alioufanya katika mwaka 2016/17, pia tumeona mafanikio na tumeona barabara ambazo hazijafikiwa mwisho wake na barabara hizi kwa mwaka 2017/18, zimeletwa tena kuombewa fedha kwa ajili ya matengenezo.

Mhe. Mwenyekiti, cha kusikitisha kwamba serikali inatoa fedha kwa ajili ya kutengeneza barabara hizi lakini hatimaye bajeti inaisha yale makusudio yanakuwa hajafikiwa. Niiombe sana Wizara hii ihakikishe kwamba vile vipa umbele ambavyo

wamevitenga basi ihakikishe kwamba fedha zinapatikana na vinatekelezwa kwa wakati.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 44 kifungu cha 118 mpaka ukurasa wa 45 kifungu cha 120 kuna Shirika la Meli na Uwakala wa Zanzibar. Shirika limepanga kununua meli mbili moja ya mafuta na meli ya abiria. Jumla ya pesa zilizotengwa ni bilioni 20. Kwanza niipongeze serikali kwa kununua meli ambayo ilikuwa inatoa huduma kuchukua abiria pamoja na mizigo kutoka Unguja kuelekea Pemba. Lakini kama alivyosema Mhe. Jaku Hashim cha kusikitisha mpaka sasa meli hii imesitisha huduma zake kwa muda wa wiki mbili sasai. Tumeambiwa kwamba kifaa hichi kilichoharibika mpaka kitoke Ujerumani.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri watakapokuja hapa atueleze mambo haya:

Kifaa hichi kitapatikana lini na meli hii itaanza huduma zake kama kawaida kwa muda gani. Niseme kwamba kabla ya kupitisha hizi pesa bilioni 20 nilitaka kujua, Mhe. Waziri atakapokuja hapa atueleze kwamba:

a) Meli zinazotaka kununuliwa zina thamani gani kwa kila meli moja.
b) Serikali imetoa *tender* kwa Makampuni ya utengenezaji wa meli hizo ambazo zinazotaka kununuliwa. Ni kampuni gani iliyopewa *tender* hiyo na wataalamu wetu wazalendo wameshirikishwa vipi.

Pia Mhe. Waziri atakapokuja Mhe. Mwenyekiti, atueleze hizi meli zinazotaka kununuliwa zitakuwa na uwezo wa kuchukua abiria wangapi pamoja na tani ya mizigo. Lakini meli ya mafuta itakuwa na uwezo gani wa kitaalamu wa kupokea na kutoa mafuta.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri aweze kuja kunipa ufafanuzi katika maeneo haya. Pia amesema kuna boti nne zitanunuliwa kwa shilingi milioni 800 zimetengwa kwa ajili ya kununua boti ndogo kwa ajili ya kuwapelekea wananchi waliyokuwepo katika visiwa vidogo vidogo kwa mfano Tumbatu na maeneo mengine. Je Mhe. Waziri hizi boti ambazo zinazotaka kununuliwa hizi pesa zitatosheleza. Pia atueleze kwamba boti hizi nne wanazotaka kununua kwa kuwa visiwa hivi vipo vingi watapeleka maeneo yepi na yepi waliyokusudia.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye barabara inayotaka kujengwa ya Bububu mpaka Mkokotoni. Barabara hii ilikuwa katika vipaumbele vya mwaka 2016/17. Hatimaye mpaka sasa wananchi baada ya kuona kimya kimezidi wameamua kupanda majani katika barabara hiyo. Pia tunaona kwamba kuna maeneo ya Kihinani pamoja na Chaani watu wa UUB wameanza kuziba mashimo madogo madogo. Hivi hatuoni kwamba barabara hii inatarajiwa kujengwa katika kipindi hichi cha mwaka 2017/18, sasa hivi wameanza kuziba na zinatumika pesa.

Mhe. Waziri tunataka ukija hapa utueleze ni gharama gani ambazo zinatumika kwa sasa na hamuoni kwamba serikali tunaibebesha mzigo baadaye tunakuja kubomoa katika barabara ile wakati pesa zimeshatumika. Hakuna haja yoyote ya kuona kwamba fedha hizi badala ya kuziba katika eneo lile linalotaka kufanyiwa matengenezo barabara ile yakazibwe mashimo ambayo yapo katika barabara mfano barabara inayotoka Kiembesamaki kuelekea *Airport* yaani kwa Mchina pamoja na barabara nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, nasema hayo kwa sababu Wizara inapoweka malengo yake iangalie kwamba hichi kima cha fedha tunachokiweka kutekeleza mradi fulani waone kwamba mradi ule na fedha zile zilizotengwa zinaweza kufikia lengo. Kuliko kutenga fedha kidogo na badala yake baadaye tunapata hasara kubwa. Kwa sababu tunaweka fedha labda tuseme kwa ajili ya

kutengeneza barabara hiyo ya Bububu mpaka Mkokotoni tumetenga labda bilioni 14, lakini je zinatosheleza? Kama hazitoshelezi tutafanya kazi ya kila siku kujenga barabara hizo kwa muda na baadaye tena mashimo yanakuwa mengi, lakini pia zinasababisha ajali barabarani kila wakati. Tukiangalia kwa kweli barabara nyingi hapa Zanzibar zikiwemo za Unguja na Pemba zimejengwa muda si mrefu lakini baada ya kunyesha mvua tu kubwa zilizonyesha basi tunakuta athari zinajitokeza.

Mhe. Mwenyekiti, nimuombe sana Mhe. Waziri kupitia mfuko huu wa barabara basi tunapopanga mradi tuhakikishe kwamba fedha zinazotengwa kwa mradi ule tuone kwamba zinatosheleza na kuwa lengo linafikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa wenzangu wengi wamechangia niseme la mwisho Mhe. Waziri nimuombe sana katika jimbo langu la Kiwengwa kuna miradi miwili ya barabara na ni ahadi za Mhe. Rais Amani Abeid Karume, lakini kuna ahadi ya Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein. Barabara hizo ni barabara inayotoka Pengeni kuelekea Kitope imeahidiwa tokea mwaka 2007 mpaka sasa barabara ile ipo kwenye ilani tu. Kwenye bajeti hii ya mwaka 2017/18 katika bajeti haimo. Namuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja hapa basi anambie kwamba barabara ya Pangeni kuelekea Kitope itatengenezwa lini.

Pia kuna ahadi ambayo Mhe. Rais wetu Dkt. Ali Mohamed Shein alitembelea katika kijiji cha Mgonjoni na aliagiza wizara zinazohusika ikiwemo Wizara ya Afya, Wizara ya Elimu, Wizara ya Ardhi Maji Nishati pamoja na ya Barabara basi zipeleke huduma muhimu katika kijiji kile. Niwapongeze sana Wizara zilizobakia zote zimeshatekeleza wajibu wao, lakini mpaka sasa Wizara hii ya Ujenzi ile ahadi aliyoitoa Mhe. Rais kule Mgonjoni haijatekelezwa. Nimeona humu katika bajeti yao wametenga fedha kwa ajili ya kuweka kifusi katika njia ile. Niseme kwamba watoto wanapata shida sana wakati wa kwenda skuli na inafika

pahala wanakatisha masomo yao kwa ajili ya kuona ile njia na viongozi wanashindwa kufika katika maeneo yale kutokana na uharibifu wa njia ile.

Mhe. Mwenyekiti, kwa haya machache niseme naunga mkono hoja kwa asilimia 95 na tano mpaka atakapokuja kunipa majibu ya kina Mhe. Waziri basi nitaunga mkono kwa asilimia 100. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti,.

Mhe.Mwenyekiti: Tunamwita Mhe. Abdalla Maulid Diwani na baadaye atafuatia Mhe. Zulfa Mmaka Omar na Mhe. Ali Suleima ajitayarishe.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa ya kuchangia hotuba ya Makadirio ya Matumizi na Mapato ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafiri inayoongozwa na Komredi Mhe. Ali Karume.

Awali ya yote napenda kumshukuru *Subhanahuu Wataala* kutujaalia kusimama mbele ya Baraza hili Tukufu. Baada ya hapo niwashukuru viongozi wote waliokuwa kwenye wizara hii kwa umakini wao na utendaji wao, kuanzia mwenyewe Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Wakurugenzi wa sehemu mbali mbali kwenye taasisi hii.

Nije katika hoja zangu moja kwa moja bila ya kupoteza muda nakwenda kuchangia hoja yangu katika ukurasa wa 23(c) Taarifa za Utekelezaji kwa Taasisi na Mashirika Yanayojitegemea, nakwenda katika Viwanja vya Ndege. Nimpongeze sana Mhe. Mkurugenzi kwenye Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kwa ufanisi anaopata hadi hii leo uwanja wetu wa ndege kuona kuna ufanisi mzuri. Kila mtu ni shahidi wa mabadiliko yale yaliyokuwepo pale katika kile kiwanja kile cha Ndege.

Katika mabadiliko yale ningeomba Mheshimiwa aangalie miundo mbinu rafiki kwa wale wenzetu wenye ulemavu kwa upande wa kusafiria wanapoingia wageni. Mimi nimeshawahi kumuona mlemavu kwa macho yangu anaanguka kwa sababu *slip way* ya kushukia hapana kwa watu wenye ulemavu, imekalia vibaya sana.

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba sana katika kuboresha hilo basi lile suala la miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu lipewe *priority*. Hao wote ni wenzetu, Mwenyezi Mungu tu kawajaalia mitihani hii na sisi wengine ni watarajiwa wa hayo ili wasione kama tunawanyanyasa katika kutumia nyara za taifa za serikali kwa sababu na wao wana nafasi yao kutumia. Panapotengenezwa hivyo basi kama panachelewa basi kipindi hichi ambapo hakuna ile miundombinu rafiki kwa walemavu wangetumia lile geti kubwa la kuingilia, pale ni karibu kwao kutumia na karibu kufika sehemu ya kuondokea, hata miundombinu haitowasumbua. Tofauti na kwenda kule kwenye *packing* waweke gari kule, washuke pale ambapo ni mazingira ambayo siyo rahisi.

Ningeomba sana Mhe. Waziri katika hilo uliangalie kwa umakini zaidi ili na wao wenzetu wasiwe na masikitiko. Masikitiko yao makubwa ilikuwa ni kwa upande wa Uwanja wa Ndege pamoja na maboresho mazuri ningeomba sana hili suala liangaliwe.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mbele nakwenda katika Shirika la Bandari C.2. Kwanza nampongeza sana Mkurugenzi wa Shirika la Bandari, wenzangu waliopita walimpongeza na mimi kwanza na *declare interest* yangu. Mimi nilikuwa ni mmoja ya watumiaji wa bandari ya Zanzibar kwa asilimia kubwa sana. Mimi ni mdau pale katika Bandari, nimeona mabadiliko ya dhati kabisa Mhe. Mkurugenzi anayoyafanya katika bandari yetu ile. Lakini kuna changamoto zake naomba azichukuwe ili zitatusaidie kuona yale maboresho yanazidi zaidi.

Kwanza nimpongeze hata juzi tumekuwa shahidi tayari ile *screen machine* pale imeshawekwa. Ilikuwa ni kilio cha muda mrefu, kila siku watu walikuwa wanasema lini Zanzibar itakuwa na *screen machine* ya kupitishiaa mizigo, kukagua. Sasa hivi tayari kwanza hongereni kwa hilo na hongera zake Mkurugenzi wa Shirika la Bandari. Kuna changamoto, na kumekuwa na utitiri wa maofisi ndani ya Shirika la Bandari, vitengo vimekuwa vingi sana vinaleta usumbufu kwa wafanyabiashara. Mle ndani sasa hivi kuna vitengo havipungui tisa mpaka kumi na zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, ningeiomba serikali itafute utaratibu mzuri wa kupunguza vile vitengo kama itawezekana au kuviwekea utaratibu mzuri au mpango mzuri ili yule mfanyabiashara asiwe na masikitiko akiingia mle akileta mzigo wake anatakiwa aende ZMA akitoka huko aende ZFBE Kitengo cha Udhibiti wa Vyakula na Dawa, akiondoka pale kuna Miyonzi akiondoka hapo kuna ZBS, akiondoka hapo yaani utitiri wa vituo umezidi na bandari yenyewe kama tunavyoiona ni ndogo. Kwa hivyo msongamano unakuwa mkubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba sana Mhe. Waziri katika hilo uliangalie ili ufanisi wa wafanyabiashara wetu wasisikitike na ule msongamano wa mle katika kupata huduma zao na kurahisisha kupata huduma kwa muda. Mambo mengine yote sasa hivi mazuri nimpongeze, *conjunction* za meli na makontena ndani ya bandari hayapo. Hongera sana katika hilo, japo yalikuwa ni maamuzi magumu lakini yamepita na sasa hivi imekuwa ni faraja, niwapongeze sana kwa hilo.

Nikiendelea mbele bado kuna zogo baina ya yale mashirika yake yanayofanya kazi mle ndani ya Shirika la Bandari kwa mfano yale Sindikeri na Jitihada Njema na mengineyo bado wana changamoto zao. Kwanza walikuwa wana changamoto kuona namna gani makato yanavyokatwa kupitia taasisi zetu za fedha. Hilo muwasaidie kwa sababu wale wanakuwakilisheni nyinyi,

kubeba mizigo bila ya wale mizigo ndani isingetoka. Kwa hivyo vile vilio vyao muwasaidia kuona kwamba vinatatulika vitatuliwe ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi na kuipenda ile kazi yao.

Mhe. Mwenyekiti, nikisogea mbele nakwenda katika C.3 Shirika la Meli na Uwakala. Nalo vile vile nimpongeze Mkurugenzi wangu wa Shirika la Meli, pamoja na kumpa mzigo mkubwa sana usiobebeka, mmoja alisema mzigo mzito mpe Mnyamwezi, huu umeshampita hata Mnyamwezi haumfai. Tumempa mzigo mzito sana wa kuendesha Meli yetu ya Mapinduzi II ambayo meli hiyo sasa hivi najua kwamba imesimama lakini kwa maelezo tu kifaa kile nimeshaambiwa kwamba kinafika kesho na baada ya wiki moja meli hiyo itakuwa inafanya kazi. Nimpongeze kwa jitihada zake ambazo alizozifanya mpaka hiyo meli kipindi kidogo kwamba kimeharibika lakini tayari ile meli imepangiwa mpango mzima kuhusu kufanyakazi.

Mhe. Mwenyekiti, meli yetu ya MV. Mapinduzi tunaitia katika biashara bado haijaweza kuingia katika ushindani kutokana na muundo wa ile meli. Najua serikali hampo tayari meli ile kuikata au kuifanyia jambo lolote ili kuweza kuingia katika ushindani ya biashara. Ningeomba basi itafutwe mbinu angalau kuweza kuisaidia kwenye bandari zetu iwe rahisi, katika upakiaji mfano wa magari iwe rahisi ile meli ipakie magari kuelekea Tanzania Bara na kwenda Pemba na sehemu nyengine Tanga leo hii imekwenda Comoro nikupongezeni mshafika mpaka Comoro bado Comoro watahitaji magari lakini jee kwa mlango tuliokuwa nao tunao uwezo huo. Uwezo haupo mnasema tufanye kazi meli ile ifanye kazi izalishe ni hatua tutachukua miaka mingi sana kufika huko kunako matarajio yenu. Matarajio yenu si mabaya ni mazuri lakini muundo wa ile meli ni changamoto.

Niwapongeze vile vile juzi imeenda Comoro cha kufurahisha au cha kupendeza zaidi Uongozi mzima wa Wizara hii kuanzia Waziri, Naibu Waziri, Naibu Katibu sijui Meneja mmekwenda

kutangaza biashara yetu ya meli kule Comoro hongoreni sana, lakini jee hapo hapo kulikuwa na haja ya msafara wote huu kwenda Comoro kutangaza hii biashara? Hatuoni kama tumetumia rasilimali ya nchi hii pengine tumetumia rasilimali au tumetumia pesa nyingi ambapo angeweza kwenda Meneja tu au Mkurugenzi tu wa Shirika la Meli na Naibu Katibu wake wakenda kutangaza ile meli yetu kufanya kazi lakini leo uongozi mzima wa Wizara ile umekwenda kule Comoro ni kweli jamani tumeitendea haki, nilitaka hilo moja tu nilizungumziye mambo yengine yote yanakwenda vizuri wale wafanyakazi tayari saba washarudi Shirika la Meli nimpongeze sana kwa uongozi wake Mhe. Katibu wa Wizara hii na Meneja kushirikiana juu ya suala zima la wale watendaji.

Nikiendelea mbele nende katika C4 nakutana na ZMA nayo vile vile kwa upande mmoja niipongeze nimeona huku wamesajili meli nyingi sana meli 186 hongera zao sana hawa ZMA lakini kama na wao vile vile panapo mafanikio na changamoto hazikosi, ziko changamoto. Ningeomba Mhe. Wazari utakapokuja ZMA wamesajili meli 186, mwaka 2016/2017 nitaka kujua jee usajili wa meli hizi Zanzibar imepata kiasi gani Zanzibar katika usajili wa meli hizi imepata kiasi gani, kwa sababu katika kitabu chako hujaandika, umetuandikia tu katika kiambatanisho chako kwamba mumesajili meli 186 hongereni sana kuona kweli Kampuni inafanya kazi lakini yako matumizi kufungua ofisi tu pale ya bilioni 2,000,000,000 mbona ni pesa nyingi sana, kwa mujibu nilivyokisoma hiki kitabu nimeona mumetumia pesa kwa ajili ya ufunguzi wa ofisi ni pesa nyingi sana vile vile naziona haziendaji na hivi zilivyo katika maelezo yako kwa hiyo ningeomba tuu unipe mchanganuo ule ili niweze kujiridhisha na masuali mengine.

Mambo mengine kidogo afadhali japo juzi kulikuwa na changamoto ya kutaka kuongeza matozo kwa upande wa kontena pale bandarini kutoka elfu 5,000 kwenda elfu 8,000 mlitaka

muweke pesa nyingi lakini mmefika pahali mmekubaliana ni vizuri kuweza kuwasaidia watu wetu hongereni sana katika hicho.

Mbele katika mchango wangu vile vile nikiendelea katika suala zima la upasishaji wa magari kule kidogo kuna changamoto sasa hivi ukitaka kupasisha magari yako basi uwache kazi siku nzima kwa kweli kuna changamoto nyingi sana. Upasishaji wa magari kule karakana wananchi wetu wa nchi hii wanasikitika, zamani ilikuwa *just* unakwenda *one hours, two hours* umeshamaliza kazi yako gari ishapasi lakini sasa hivi sayansi na teknolojia imezidi imekuwa siku nzima inapotea katika suala la kupasisha magari. Kule Karakana pamoja na changamoto nyingi kuanzia malipo benki mpaka kufika kule kuchukua magari yako ni siku nzima inapotea, hamuoni kwamba tunadumaza maendeleo, baada ya watu wafanye kazi waende mbele sisi tunadumaza tunarudi nyuma kutokana kupoteza muda ambao hauna muhimu.

Kuna tofauti gani pale mwanzo sawa hatukatai pesa zilipwe benki wacha zilipwe lakini ilikuwa kuna mambo lazima yarahishwe pale kunakusanywa pesa nyingi, basi kwa nini msiongeze hata mkaweka mtu wa benki pale katika chumba kimoja pale akakusanya zile pesa akaondoka nazo akapeleka benki kwa sababu pale hapatakiwi kulala pesa, kuliko sasa hivi msongamano ni mkubwa sana, wa ulipaji kuja benki kwenda Karakana pale watu wanapiga kelele katika hilo.

Ningekuomba sana Mhe. Waziri, ulingalie najua mnatafuta taratibu lakini bado hamjalifikia lakini ningeomba zaidi ulichukuliwe kwa umakini kuona zile kero na changamoto za pale zinaondoka. Malamiko yako mengi sana katika suala lile kule la upasishaji ni lazima tupasishe, hivi sasa tu kuna toleo limetoka juzi kuhusu leseni watu wanachanganyikiwa hawafahamu kitu gani. Ningeomba nalo kama Serikali militolee kauli ili watu wetu wapate elimu tosha juu ya kadhia iliyotangazwa juzi kupitia *police traffic* nafikiri na *ZRB* kuhusu hizi leseni kuna tatizo watu

hawajafahamu wanadanganyana hawajui kitu gani pengine Serikali inataka pesa tu kumbe vile taratibu ipo, sheria ipo lakini kutokana na elimu ndogo kwa watu wetu imekuwa wanasema maneno mbali mbali. Ningeomba sana muwaelimishe watu wetu ili wafahamu waweze kuwa watiifu katika yale yote yanayohitajika na Serikali hii.

Nikiendelea mbele nimekuta UUB kwanza niwapongeze Idara ya UUB ujenzi na uangalizi wa barabara kwa kufanya kazi nzuri sana barabara ya Jendele, Unguja Ukuu imemalizika bado kidogo tu nafikiria sasa hivi inasubiriwa jua litoke imalizike lakini bado kuna kilio cha kupatiwa vifaa, inafanya kazi vizuri sana UUB lakini tatizo la vifaa, vifaa vichakavu leo hii tunamuiona Mecco siku zote anafanya kazi vizuri kwa sababu ana vifaa vya kutosha kazi zile anazofanya Mecco anaweza kufanya huyu UUB na tukazi-*maintain* pesa zetu za ndani kuliko tunampa mtu anaondoka nazo zile pesa.

UUB ukishawapa zile pesa huwalipi mkataba wale wanafanya kazi kwa ajili ya Serikali hii wanalipwa mshahara, kwa hivyo ningeomba sana vifaa kwa ajili ya ujenzi wa barabara UUB lazima vinahitajika, vifaa ni vya muda mrefu vimeshachoka Mhe. Waziri lazima utenge fungu katika hilo humu sijaliona kwenye kitabu chako kwa ajili ya ujenzi wa barabara ili upate vifaa kuweza kufanya kazi nzuri na kuboresha mambo mbali mbali katika vifaa vyetu vile katika barabara zetu.

Lakini vile vile nikienda mbele katika UUB bado kuna matatizo kidogo tu, hivi nyuma tulihangaika sana wakati tunapitia kamati zetu mbali mbali kupewa tenda au kupewa kazi watu ambao waliokuwa hawajawa *registered* wanapewa kazi *tender* watu ambao hawana *Tax registration number, Tin number* hawana, hawana *VAT* wala ofisi hawana katika nchi hii wanapewa kazi vipi? Kwa mfano kuna Kampuni moja ya *Abdalla Construction* vipi ile kampuni imepewa kazi ya kujenga barabara kuweka kifusi

karibuni barabara tatu. Chukwani/Buyu wamejenga barabara ya Fuoni Kibondeni, wamejenga barabara ya *Wireless* Kikwajuni, yule mtu ukimuangalia hayupo hana hata utambulisho wa *VAT,* hana utambulisho namba maana tunampa pesa zetu lakini pesa zetu hatupati kodi jee katika hilo Mhe. Waziri liko vipi tuna changamoto japo tunabebana katika hilo lakini katika hili suala la *Abdalla Construction* hapa hapajakaa sawa, ningeomba sana Mhe. Waziri utakapokuja unipe majibu katika suala hili la *Abdalla Construction* ili kuweze kujiridhisha. Kujiridhisha katika kadhia nzima ya hawa jamaa ambapo tunawapa *tender* zetu katika kufanya shughuli zetu nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, nilitaka niseme hayo machache nafikiri nimefahamika na nashukuru sana kunipa nafasi hii. Ahsante sana siungi mkono hoja mpaka hapo *time* ambapo nitapojiridhisha na majibu yangu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Abdalla anayefuata ni Mhe. Zulfa na baadaye Mhe. Ali Suleiman ajitayarishe.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia machache katika Wizara yetu hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze na pongezi ambazo ndani yake zina pole. Mhe. Mwenyekiti, niwape pole sana Wizara ya Mawasiliano kwa kazi nzito ambayo walikuwa nayo katika kipindi hiki cha maafa na pia niwape pongezi sana wafanyakazi wote waloshirikiana katika kuweka sawa barabara zetu zile.

Mhe. Mwenyekiti, pongezi hizi nizipeleke hasa kule Pemba. Mhe. Mwenyekiti, tumeona kwamba miundo mbinu ya barabara upande wa Pemba zimeharibika kwa hali mbaya sana, madaraja mengi sana yalikatika, watu walikosa mawasiliano, kuna barabara ambazo ni watu wanatumia kama Mkoani zilikatika kwa kweli

Mheshimiwa watu walifanya kazi ya ziada. Nilimuona Afisa Mdhamini wa Pemba Mheshimiwa ana homa kabisa kwa kuchezea mvua, *engineer* pale ana homa lakini hawakusita wakasema kwamba kazi hii wanaifanya na kazi ile imefanikiwa. NSiwape pongezi sana na naamini kwamba kwa ujira ule ambao wameufanya watapata thawabu nyingi sana na *Allah* atazidi kuwazidishia imani ya nchi yao juu ya hilo.

Mhe. Mwenyekiti, nikiotoka hapo kwenye pongezi naomba nianze katika suala la Shirika la Meli. Mhe. Mwenyekiti, hapa kuna hii meli yetu ya MV Mapinduzi II. Mhe. Mwenyekiti, meli ile tumeinunua kwa pesa nyingi sana na Wapemba sana tulifurahi sana kupata meli ile, kwa sababu tulijua kwamba usumbufu wa kila siku kupanda meli mbovu tukifika kati kati tukaambiwa *engine* imegoma sijui kitu gani hapo ilikuwa imefika mwisho wake.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba meli ile ni mpya imenunuliwa juzi tu na sasa hivi tunakuta kwamba yanatokezea matatizo ambayo hatuyafahamu kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, kwenye meli hii tusifanye masihara kwasababu wenzetu wa upande wa pili hawa walisema kwamba jimeli lile ni bovu, leo kwenda na kurudi ikawa siku mbili inafanya kazi siku ya tatu haifanyi kazi Mheshimiwa kwa kweli mutatufanya kwamba sijui tuwajibu nini. Kwa hiyo nimuombe sana Mhe. Waziri anieleze kitu gani hasa kimefika katika meli hii kwa sababu kuna siku sijui iliharibika *engine* na sasa hivi kwa kweli hata kuona hatuioni kama inafanya *route* zake.

Watu wa Pemba wanasumbuka hasa kipindi hiki cha Ramadhani tunajua kwamba watu wa Pemba wanafanya vibiashara vyao kuleta huku Unguja wapate riziki zao za halali lakini watu wale wanaumia sana kupanda meli ambazo sio za Serikali wanatozwa pesa nyingi sana tunaona sasa hivi kuna meli moja tu ambayo pale inafanya kazi na watu ni wingi sana na siye tunagemea meli yetu

ile tunamuomba sana Mhe. Waziri atueleze kitu gani hasa kimeifika ile meli yetu mpya.

Tukiona hapo Mheshimiwa mimi naomba niende katika Idara ya usafiri na Leseni. Mhe. Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba Idara ya Usafiri na Leseni inafanya kazi kubwa sana na Idara hii inaingizia mapato mengi sana Serikali yetu ambayo hata na sisi tunafaidika. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kweli mzigo wape wale upande mwengine ambao hawajajwi lakini sasa ile Idara ambayo inafanya kazi ile kwanini tunaitupa.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Usafiri na Leseni inaingiza pesa lakini inasikitisha ukienda hasa kule Pemba Idara ya Usafiri na Leseni jengo lao ambalo wamegawiwa na UUB ni dogo sana unakuta *section* tatu wameingizwa chumba kimoja. Mheshimiwa tunajua kwamba Idara ya Usafiri na Leseni inahudumia madereva na makonda na kama tunavyowajua madereva na makonda hasa wa vi-*carry* Mheshimiwa kishindo chao hebu niambie Mheshimiwa unaingiza watu wale wanne katika chumba kimoja unawahudumia akitoka pale kwenye *route* aende kwenye leseni na biashara unakuta kwamba vyumba vile viko pamoja na wakati hao hao Idara ya Usafiri na Leseni, wana jengo lao ambalo limeharibika na hapa nimekuta kwamba pesa mara ile ziliingizwa Idara ya Usafiri na Leseni nilijuwa kwamba kwa pesa zile jengo lile la Idara ya Usafiri na Leseni mutalifikiria kulitengeneza ili watu waweze kuhamia katika jengo lile na kufanya kazi.

Lakini kwa kweli ukienda kuiona hiyo Idara ya Usafiri na Leseni Mheshimiwa huwezi kuamini kama humu wanafanya kazi ambao wanakusanya kodi kubwa ya Serikali. Kwa hivyo naiomba sana Serikali mimi hapa kwenye hili fungu la Idara ya Usafiri na Leseni nitazuia, kwa sababu kila siku tunaambiwa kesho, keshokutwa jengo lile litatengenezwa watu wale watawekwa pahali pazuri pa kufanyia kazi. Lakini niseme kwamba watu wale tunawahatarisha hata afya zao, kwa sababu mule unakwenda siku

nyengine hizo *AC* hazifanyi kazi chumba chenyewe kina watu wanne, watu watano kwa kweli hata hiyo nidhamu ya kufanya kazi pale inashindikana. Kwa sababu mkisha kukaa watu wengi sana katika ofisi tena inakuwa si kazi mnaweza kufanya *story* na mitihani mengine. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri kwa hapa mime leo patakuwa na kazi kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende katika Karakana, tumeona hapa kwamba kuna magari mengi sana yametengenezwa katika Karakana zetu lakini nijuulize sijui kwamba gari zile zimetengenewa na *spanner* mbili tatu zilizozopo kwa sababu katika karakana bado kuna haja kubwa kupeleka vifaa katika sehemu ile na tunajua kwamba magari yetu ya Serikali ni vizuri sana kutengenezwa katika karakana zile kuliko mafundi wa nje. Naamini kwamba Waziri yoyote au Wizara yoyote inayoipenda hasa gari yake haiwezi kuipeleka Idara ya Usafiri na Leseni Karakana kwenda kutengezwa, kwa sababu vifaa venyewe havipo na hivyo viliovyopo ndio hivyo hivyo mtihani.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo niombe sana ile sehemu ni nzuri na ni nyeti kwetu sisi kwa sababu hata sisi tunatakiwa kwamba tuyapeleke magari yetu pale ili tuwe na amani na gari zetu kuliko kuzipeleka nje huko kwenda kutengenezwa. Kwa hivyo niombe sana katika bajeti hii basi wawatengenezee vile vitu ambavyo wanavitaka na wao, ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi.

Nikitoka hapo Mheshimiwa nataka nizungumzie suala la *Airport* Pemba Mheshimiwa mara ile tulipitisha pesa nyingi sana tukapiga makofi mingi sana utengenezaji wa *Airport* Pemba lakini nashangaa hata mwaka mmoja ndio unataka kutimia haujatimia *Airport* Pemba mbovu, inavuja, Mhe. Naibu Waziri ni shahidi kwa sababu tulikwenda kumuonesha na jengo lile alilifanyia marekebisho kwa pesa nyingi sana. Nimuuliza Mheshimiwa tu hizi pesa mulimpa *engineer* gani ambaye hafahamu, kwa sababu jengo lile ni *fail* tukitoka hivyo hivyo jengo la *Airport* Pemba

Mheshimiwa sasa hivi ukweli usiofichika lile jengo tayari ni dogo sana. Tukiwa abiria wengi sana tu Mheshimiwa hatuwezi kupata nafasi za kukaa utambiwa wewe simama, wewe kaa kwa sababu nafasi ishakuwa ndogo na tukiangalia kila siku ukienda ukuta huu umekatwa huu umewekwa sawa hapa pamewekwa hivi, hapa pamewekwa hivi Mheshimiwa pale tunahatarisha roho za abiria.

Kwa sababu jengo lenyewe si zima hivyo halafu kila siku mnalikana kuta Mheshimiwa hapa tutakuja kupeana pole kwa jambo ambalo tumelisababisha sisi wenyewe. Kwa hivyo nikuombe sana, hapa nimeona pesa za marekebisho Uwanja wa *Airport* Pemba Mheshimiwa hizi pesa zitapitishwa lakini zikishapitishwa tutakuja kukuhoji na ikiwa hatutoridhika mwakani Mheshimiwa hapa hatutokupitishia pesa kwa sababu tutajua kwamba tunakupa pesa unakwenda kufanya ambavyo sivyo.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende katika Idara ya UUB Idara ya UUB niipongeze sana inafanya kazi vizuri na tumeona kigezo kidogo tu juzi hapa tulipopata maafa, hawakuwaja Mecco wala hawakuja kampuni nyengine yoyote walifanya kazi zao UUB na zile barabara waliziweka sawa tukapata kupita lakini sasa hawa UUB vifaa vyao vishakuwa vibovu sana kwa hivyo niwaombe sana waende mbio zote, hawa UUB hebu tuwanunulie hivi vifaa waweze kutengeneza barabara. Kwa sababu tunaona kwamba Mashirika mengine hao ambao tunawapa pesa kututengenezea barabara wanatutengenezea barabara ambazo hazina viwango.

Mheshimiwa mimi nishaenda katika ukaguzi wa barabara tumekuta barabara nyingi sana ziko chini ya viwango pesa anazoingiziwa ni nyingi lakini barabara unakuta haiko kwenye kiwango chake. Lakini hebu tuchunguze tena wewe Mhe. Waziri nenda tena kafanye uchunguzi kaangalie barabara zilizojengwa na UUB, kaangalie barabara ambazo zimejengwa na watu wengine kwa pesa nyingi sana uangalie ipi barabara nzuri, utapata jibu

kwamba UUB wanatengeneza barabara nzuri sana lakini hawana vifaa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hizi pesa tusizipeleke nje hapa kwetu tunazitaka. Tukiangalia watu wa nje hao tunawapa pesa nyingi sana lakini UUB pesa kidogo wanazopewa wanatengeneza barabara nzuri yenye viwango na hao ambao wanapewa pesa nyingi sana wanatengeza barabara mbovu hazina viwango. Kwa hivyo nikuombe sana Mheshimiwa hizi pesa usiende kunufaisha watu wa nje hebu zipeleke hapo Serikalini tutengeneze barabara zetu nzuri na sisi tuondoke na ile bugudha kwamba barabara hazina viwango, barabara mbovu, barabara hivi tuwatizame hawa UUB Mheshimiwa tuwape pesa tuwatizame watatufanyia vipi. *(Makofi)*

Nikitoka hapo Mhe. Mwenyekiti, nataka niende katika bandari ya Mkoani. Tunakuta kwamba bandari ya Mkoani kuna *distance* kubwa kutoka katika bandari hadi sehemu ya kupandia gari, na pale kama unavyojua watu wanasafiri na watoto wengine wagonjwa, wengine wana hali ambazo si nzuri lakini tatizo Mheshimiwa nilikuja kukuomba hapa pale bandari ya Mkoani basi kama haiwezi kuezekwa barabara nyembemba tu basi japo tuwekewe maturubali kutoka juu ambapo watu wanapanda gari mpaka kufika kwenye meli.

Mhe. Mwenyekiti, mimi juzi nimekwenda nakuta watu wanakwenda panda meli wana watoto wachanga wanarowa, kwa kweli hali mbaya hebu tuwahurumie ile *distance* ni kubwa sana basi kama huwezi hivyo watafutie japo mabasi, wakishuka pale ambao wanahitaji mahitaji maalumu wapande mabasi waweze kwenda kupanda gari Mheshimiwa. Lakini kwa kusema kwamba wale wakulima na wakwezi wakishuka pale meli ambao wako katika hali za mahitaji maalumu wanarowa, wanapigwa jua ahaa kwa kweli si vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, tuwahurumie sana wapiga kura wetu wananchi wetu wanaipenda hii Serikali na wasikivu sana kwa hivyo nikuombe sana na wale wananchi wetu na sisi tuwaangalie tuwape msukumo kidogo ile bandari itiwe japo maturubali kama kuezekwa kwa bati kama kwa huku ambapo wamefanya Unguja ni ngumu basi tuwekewe japo maturubali ili watu waweze kwenda kupanda meli huku wanajisikia kwamba Serikali inawathamini.

Nikitoka hapo niende katika suala zima la mikataba, tunafunga mikataba na wakandarasi mbali mbali, lakini hapa katika sehemu ya ukandarasi wananchi wa hapa tunapiga kelele. Kuna watu wanapewa hizi tenda kufanya kazi wakati wa kutaka kuwachunguza mheshimiwa watu hawa tunakosa kuwaona. Kwa hivyo, niwaombe wakati wa kutangaza hizi *issue* za ujenzi waangalie sana watu wa ndani ambao wanaweza kuchukua tenda zile na kufanya kazi, kuliko kuchukua watu ambao hawafahamiki au hawana maana wakapewa hizi kazi na mwisho wa siku wanataka kukaguliwa watu hawa wanakuwa wanakosekana. Kwa kweli mheshimiwa ndio inakuja kupitishwa kwamba hapa sisi Abdalla hatumuoni, sisi fulani hatumuoni, kwa kweli hili si jambo zuri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi hii wizara naipenda sitaki niseme maneno mazito na nataka niunge mkono wizara hii kwa asilimia tisini na tano na asilimia tano naziweka hadi pale nitakapokuja kusikia kwamba hili jengo la Idara ya Usafiri na Leseni nalo limewekwa katika hali ambayo itaniridhisha. Bila ya hivyo Mheshimiwa hapa mimi leo nitavaa soksi ili nipige buti, si kawaida yangu lakini nasema kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo nawashukuru sana nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe muunge mkono hoja hii, muichangie sana hoja hii, hii ni wizara ambayo iko karibu na nyinyi na inasikia maoni yenu. Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Zulfa Mmaka Omar sasa naomba nimwite Mhe. Ali Suleiman Ali na baadae Mhe. Omar Seif Abeid ajitayarishe na Mhe. Bahati Khamis Kombo na yeye ajitayarishe.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa bajeti yake ya mwaka 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nampongeza sana Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi wetu wote, Ma-*engineer* wetu wote na wafanyakazi wote wa wizara hii ambayo ni wizara hatari kwa kazi nzito wanazofanya juu ya kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanapata faraja ya kutembea vizuri katika barabara, bahari na anga yetu. Lakini pia Mheshimiwa nawashukuru Wakuu wa Mashirika wote kama Shirika la Bandari, Shirika la Meli na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kwa kazi nzuri wanazofanya na kusimamia vyema kwanza kukuza pato la taifa na pia kupata huduma bora katika mwenendo wetu wa kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ningesema tu kwamba kuongeza serikali ni jambo zito, na kuongoza jimbo vile vile ni jambo zito. Kwa hivyo, tukizingatia mawili hayo kwamba serikali ina mzigo mkubwa na mwakilishi na yeye ana mzigo mkubwa juu ya kuhakikisha kwamba mafanikio yake yanapatikana kwa uwezo wako wote wa kufanya ili ufanikiwe na serikali yetu ifanikiwe vizuri. Wizara ya Fedha na Mipango ndio mwenye kubeba mambo yote haya katika wizara zote, kwa hivyo nayo tuipongeze kwa dhati kabisa kwa kusimamia mapato mazuri ili kufanikisha haya yote tunayoomba au inaomba wizara kwa mafanikio ya maendeleo yao. Mimi naipongeza wizara hii kupitia kazi nzuri

wanazofanya hasa kwenye barabara, pamoja na wenzangu wengi wamesema na wanaendelea kusema, lakini naipongeza UUB kwa kazi nzuri wanayoifanya, pia na *MECCO* kwa kazi nzuri waliyoifanya ambayo barabara yake moja ya Mwanakwerekwe/Fuoni tunaitumia na tunawashukuru sana. Ningetoa ombi moja tu Mheshimiwa pamoja na ujenzi wetu huo mzuri lakini bado viwango vyetu tuwe tunaviangalia kuhakikisha kwamba viwango vinakidhi haja.

Mhe. Mwenyekiti, ilipojengwa barabara ya Kinazini/Bububu wakati huo Marehemu Mzee Aboud Jumbe Mwinyi barabara ile ilijengwa nyembamba hatukutegemea mbele tunakokwenda, lakini ilijengeka vizuri kuliko barabara nyingi zinazojengwa sasa hivi. Kwa hivyo, ina maana wakati ule kampuni iliyojenga ilikuwa nzuri na viwango vyake vilikuwa vinaridhisha. Mimi ningeomba wataalamu wetu kupitia UUB wawe ni watu ambao wa kuangalia viwango barabara hii inakidhi mahitaji yenyewe kutoka siku hadi siku. Sasa hivi mheshimiwa magari yamekuwa mengi, makubwa, mazito kwa hivyo uwezo wa barabara nao pia uangaliwe li kuhakikisha kwamba tunajali barabara nzuri kwa kuhifadhi usalama wa barabara zetu na kupunguza gharama mbele tunakokwenda.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kwenye barabara hiyo niipongeze serikali kupitia wizara inayohusika kwa kupata barabara yangu ya Meli tano/Kwarara nimeona kwamba katika kitabu hiki cha malengo au mategemeo ya mwaka huu wa fedha kwamba barabara ya Kwarara mpaka Skuli ya Tumaini imo itatengenezwa kwa kiwango cha lami. Hapa nawashukuru sana lakini natoa rai.

Mhe. Mwenyekiti, tumeshuhudia hapa Mwanakwerekwe shida inayotupata siku hadi siku, na mimi mwaka uliopita nilikuwa mmoja nilisimama hapa nikasema tungejenga daraja na kwa kuzingatia daraja lingetuokoa mengi yasingetukuta juu ya adha tunayoipata kupitia Nyumba mbili kwenye daraja la Mhe. Shamsi.

Niseme kwamba serikali pamoja na kujenga hii barabara ya Kwarara kutoka pale kwa Ngulangwa kuna barabara unatokea Maungani/Langoni. Naiomba wizara kwa makusudi iangaliwe barabara hiyo kwa kupigwa *grader* na kutiwa fusi tu vizuri inaweza kutusaidia sana siku za mvua.

Mhe. Mwenyekiti, wakati wa shida hujali unapita mbali lakini unataka ufike. Kwa hivyo, naomba hili kwa kuwa matarajio ya hapo Mwanakwerekwe yatakuwa muda mrefu, lakini barabara hii inaweza kuchukua muda mfupi sana hata mwezi mmoja mwingi, kupigwa *grader* na kuweka fusi. Kwa hiyo, naiomba serikali hili tuliangalie kama la dharura na litatusaidia sana kutokana na msongamano ambao kama huko Dar es Salaam unatoka Kariakoo unakwenda Jangwani utachukua saa nzima. Sasa ndio yaliyotukuta kutoka Nyumba mbili kwenda Kwa mchina. Hilo naomba nishauri lakini naiomba wizara madhali ushauri huo utakuwa mzuri wawauangalie na utatusaidia.

Mhe. Mwenyekiti, jengine mimi nitazungumzia Shirika la Bandari, wengi wamezungumza Shirika la Bandari, mimi katika shirika hili nimekaa na nimekuwa Mjumbe wa Bodi nnakotoka, naipongeza sana wizara kupitia Shirika la Bandari. Shirika la Bandari la leo si la miaka iliyopita kwa hivyo kila zuri lilokuwepo tulisifu na tuwape changamoto wenzetu waongeze bidii, kwa sababu Mheshimiwa itakuwa mtu mbaya sana katika maisha yako kama huna imani ya kushukuru. Mwenyezi Mungu anasema ushukuru ikiwa umepata zuri au kidogo limetokea baya, shukuru kwa njia mbili. Mimi nalishukuru Shirika la Bandari kwa dhati kabisa, namshukuru Mkurugenzi na nampongeza na watendaji wake wote kwa bidii inayooneshwa. Harakati za Shirika la Bandari Mheshimiwa zimekuwa, harakati za shirika hili zinakubalika kwenda na wakati. Kwa hivyo, niombe tu vitendea kazi vizuri wamepata, uelekezaji wao mzuri wafanye kazi zao na waongeze bidii ili pato la nchi liongezeke.

Mhe. Mwenyekiti, jengine Shirika la Meli nalo nawapongeza kwa jitihada zinazoendelea hivyo hivyo kidogo, nao wamejitahidi kwa sababu tumepata meli ambayo bahati mbaya nasema tu chombo kuharibika ni jambo la kawaida na siwezi kutoa lawama kwa nini kimeharibika, kwa sababu binadamu unaumwa na ukiumwa Mwenyezi Mungu ndio anavyotaka na chombo kile umekiunda wewe binadamu. Kwa hivyo, tuseme tu kwamba wenzetu wamejitahidi kutafuta chombo hicho haraka kutoka Ujerumani, niwaombe wasimamie vyema ili wananchi wetu wapate huduma. Hasa nampongeza Mhe. Rais kwa uamuzi wake wa kusema kwamba meli hii ianze kutafuta safari za nje kuelekeza Comoro na kwengineko. Hata jana nilimsikia Mheshimiwa kazungumza kwamba tunaweza kwenda na mwelekeo wa kutumia bahari zetu mpaka alipokuwa anazungumza na Balozi wa nchi moja hapa hapa Kusini mwa Afrika ambao ni wenzetu sana. Kwa hivyo, niseme tu kwamba iongeze bidii ifanye kazi zake vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu Mamlaka ya Viwanja vya Ndege pamoja na matatizo yaliyokuwepo lakini huduma zake zinakidhi haja na tunaweza kusema kwamba uwanja wetu una mwelekeo wa kimataifa kabisa zaidi kuliko tulikotoka. Kwa hivyo, niseme tu kwamba Mamlaka ya Viwanja vya Ndege na wao wasimamie shughuli zao vizuri ili kuhakikisha kwamba pato letu la taifa linaongezeka siku hadi siku.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo nataka kulisema hapa kazi kubwa inayofanywa na vyombo vyetu hivi vya wizara hii ni vingi, tuna sehemu ya usafiri na leseni mpaka sasa hivi tumeona data zao humu nyingi tu, kuna waliopata leseni na waliokataliwa. Kwa hivyo, mimi ningeomba uwezo wa mtendaji kupata leseni dereva iangaliwe vizuri kwani maajali yamezidi katika nchi yetu, wananchi wetu wanakufa ovyo Mwenyezi Mungu atunusuru. Ukisikia leo vespa kapigwa mtu na mke wake, huyu imetokea hivi ni jambo la kusikitisha sana. Lakini katika kuangalia hilo ningeiomba mamlaka kupitia polisi *traffic* na mambo mengine

waangalie, kwa sababu kubwa tunalolitegemea hivi sasa watu waende salama katika barabara lakini leo ukipanda vespa au honda unatetemeka akili yako haiko sawa.

Kwa hivyo, niseme tu kwamba Mamlaka ya Leseni na Usafiri Idara hii iangalie vizuri kwamba wanapotoa leseni zao wawe na uhakika kwa madereva wetu. Madereva wengi ni watoto na madereva wengi hawana leseni, wengine Mwenyezi Mungu atuepushie mbali wanaweza kutumia hata leseni za bandia iliwahi kutokea hapa. Kwa hivyo, niseme hili liangaliwe ili kupata uhakika wa maisha ya watu wetu siku hadi siku.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu meli nilizungumza suala la usafiri, narudia tena Mhe. Rais jana alizungumza na Balozi wa Namibia alipanga nae juu ya kupata safari hizi na kwa bahati nzuri hii ni changamoto kwa Shirika la Bandari ili kutafuta mbinu za kufatilia vipi wanaweza kupeleka nini na kuchukua nini. Kwa sababu wanapokwenda kule hutegemei kupata abiria, unategemea bidhaa ndio kitu muhimu cha kuingiza katika Shirika letu hili la Meli.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine nitalozungumzia kwa ufupi kabisa kwa sababu mimi nimeunga mkono hii wizara sina tatizo nayo. Nasema tu kwamba kubwa tunaloliamini hivi sasa katika utendaji wa shughuli zetu mbali mbali kuna kitu ambacho kinawahangaisha wananchi kidogo, tatizo la mamlaka zetu hizi. Tuna mashirika ambayo tunayategemea sana katika nchi yetu, tuna Mamlaka ya Hali ya Hewa, hali ya hewa Mhe. Mwenyekiti, ni kitu kikubwa sana katika nchi, na taarifa ya hali ya hewa ni miongoni mwa usalama kwenye usafiri wa bahari na anga. Kwa hivyo, niwaombe wenzetu hawa wanajitahidi kutoa taarifa kama leo tumesikia taarifa tu kwamba Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inatoa wito kwa wasafiri na watu wengineo utavuma upepo mkali wakati wowote. Kwa hivyo, mambo kama haya wahusika katika bandari zetu wawe waangalifu kuwaelimisha

wanaotumia vyombo vyetu kwa ajili ya usalama wetu huko tunakokwenda.

Mhe. Mwenyekiti, jengine pia niseme tu kwamba navipongeza vyombo vyetu vya *TTCL*, Posta kwa kazi nzuri wanazozifanya kwa kushirikiana na wananchi katika kupata huduma zao bila ya matatizo. Kwa sababu tunaamini kwamba pamoja na yote Mheshimiwa Posta ni chombo muhimu na *TTCL* ni chombo muhimu kwa sababu ni mashirika ambayo yako serikalini kuungana nao katika shughuli yoyote ya serikali ni rahisi kuliko vyombo vyengine.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, mimi nawapongeza tena watendaji wote wa wizara hii kuanzia waziri mpaka watendaji wote wa chini kwa kazi nzuri wanazofanya na naiomba wizara hii inavyosimamia kazi zake baada ya kutokea maafa au kabla Mhe. Waziri na Naibu wake wanatembelea kila wakati, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu hata Wakurugenzi wetu wa Ujenzi wa Barabara nawashukuru kwa kazi zao nzuri. Lakini pia na mimi nitoe pongezi za pekee kwa Afisa Mdhamini Pemba tumpongeze kwa hali na mali anafanya kazi katika mazingira magumu na anajitolea kukiwa na jua ama mvua maana kadhia iliyotukuta Pemba Mwenyezi Mungu atuepushie isitokee tena si ndogo, lakini alisimama kidete japo njia za dharura watu walipata kupita bila ya matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho nilipongeze Jeshi la Polisi kupitia *traffic* wetu tuliokuwa nao, wamefanya kazi nzuri Mwanakwerekwe/Makaburini pale njia mbili mpaka kwa Mchina kuhakikisha gari zinapita pale kwa zamu elekea huku rudi huku. Kwa hivyo, tuwapongeze kwa kazi nzuri wanazofanya ili kuhakikisha kwamba tuko salama katika mazingira yetu wakati wa shida.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kijitoupele hasa nikizingatia kwamba barabara yangu ya Kwarara itajengwa vizuri kwa lami, naipongeza asilimia mia moja wizara hii na naomba yote waliomba wapewe ili wafanikishe kazi zao. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Ali Suleiman sasa ninamwita Mhe. Omar Seif Abeid na Mhe. Bahati Khamis Kombo ajitayarishe.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa ya kuchangia katika wizara hii, sina budi kurejesha shukurani zangu kwa *Allah Subhana Wataalah* aliyetujaalia tukakutana tena hapa leo Ramadhani ya tano tukiwa ni wazima wa afya, tuko vizuri kufanya kazi kwa ajili ya kuwatumikia wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza nataka nianze na langu mimi mwenyewe binafsi kabla ya kwenda kwa wenzangu, mimi nataka nianze na barabara yangu ya Konde. Mheshimiwa barabara yangu ya Konde ni kilio, nimekuwa nikiizungumza barabara hii kila ninaposimama, na maswali mengi huwa naielekeza wizara kwa barabara hii, lakini hadi leo bado kilio changu kinakuwa ni machozi ya samaki yanayoishia baharini. Naomba, nakuomba Mhe. Waziri mpendwa, mchapakazi madhubuti, mzuri na Naibu Waziri wako muniambie lini wananchi wangu wa Msuka mtawatengenezea ile barabara waweze kupita? Leo barabara imekatika pamoja na kufadhiliwa na kusaidiwa sisi na wafadhili lakini ile barabara tunaiacha inapotea.

Barabara inamaliza hiki kilio Mhe. Waziri tutafika siku baada ya kuziba ufa tunakuja kujenga ukuta. Ili tusije tukajenga ukuta Mhe. Waziri nakuomba chonde, chonde, chonde itupie macho ya huruma barabara ile ili na sisi nguvu zetu na wale waliotusaidia

waone kama kweli zile fedha zao walizotusaidia zimeleta faida. Haitakuwa busara wala haitakuwa ni vyema kwamba tumesaidiwa ikisha kesho na keshokutwa tukakuta watu waliotusaidia zile nguvu zao zinapotea bure, lile ni jasho la wavuja jasho wao wamejitolea kwa hisani na mapenzi ya nchi yetu kutusaidia. Kwa hivyo, na sisi tuliosaidiwa ni wajibu wetu na sisi kile tulichosaidiwa tukakitunza.

Mhe. Mwenyekiti Mhe. Waziri najua hili analo na nimeshajibiwa sana lakini ni wajibu wangu kukumbusha, kwa sababu hata kusali hakuna asiyejua kama sala ni wajibu lakini ikifika wakati wa kusali tunasoma adhana. Na mimi hii kwako wewe ni adhana na nitaendelea kuadhini kila wakati unapofika mpaka lengo langu litimie.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo ya kwangu sasa nakuja ya jumla. Mheshimiwa mimi naingia katika ukurasa wa 6 kuhusu matumizi mabaya yaliyokithiri ya barabara. Mheshimiwa imekuwa ni kilio kikubwa kwa ajili ya matumizi mabaya ya barabara hasa kwa madereva wa daladala. Madereva wa daladala na waendesha vyombo vya miguu miwili maarufu kama Tone, hawa Mheshimiwa mimi sitafuni maneno ni watu ambao pamoja na faida tunayoipata ya kusaidia usafiri, lakini imekuwa ni chukizo kubwa, kwa sababu mwenzangu Mhe. Nadir alisema wako tayari kutoa roho ya mtu kwa ajili ya nauli ya shilingi 300/-, shilingi 300/- kwao ni thamani kubwa kuliko maisha ya mtu.

Kwa hiyo, naiomba serikali iliangalie jambo hili na isiliangalie kwa kulizungumza tu lakini iliangalie kwa vitendo. Mimi nafikiri moja katika sababu inayosababisha hivi ni kukosekana kwa vituo maalumu vya kupandia abiria kwenye mabasi ya daladala. Sasa naishauri wizara natoa wito kwamba tujengeni vituo maalumu na tuweke vibanda maalumu ili msafiri ajue kwamba mimi napanda basi pahali fulani maalumu, itakuwa ni wepesi kwetu kumtambua dereva ambaye atavunja sheria. Lakini leo ikiwa hatuna kituo mtu

kasimama barabarani abiria kwa sababu wengi wao inapofika kipindi cha kusafiri anaharakishia safari tu na mwenye daladala kamuona anasimama kumchukua bila ya kujali nini kitatokea nyuma yake sambamba na waendesha vespa maarufu *T. One*.

Mhe. Mwenyekiti, zaidi ya kero ya lile wanalolifanya la kuendesha vespa zao vibaya kwenye barabara lakini wanazitoboa kwa makusudi *ekzosi* za vespa zile kuleta ghasia na usumbufu mkubwa kwa watu. Mimi Mhe. Waziri nataka nimuulize, hivi sisi hatuwaoni wale kama wanaleta adha, wanaleta usumbufu kwa baadhi ya watu? Wao wenyewe wameshajitolea kuharibu maisha yao, maisha yao wao wameshaamua kuyaweka rehani lakini wengine bado hawajaamua kuyaweka rehani.

Kwa hivyo, naomba sana ile sheria kama imeshapitishwa ya adhabu ya papo kwa papo ianze kufanya kazi mara moja ili hawa wanaovunja sheria wapatikane, wakipatikana na ile adhabu wanapata kulipa faini pale pale ikiendelea kusimamiwa vizuri Mheshimiwa mimi imani yangu kwamba tatizo hili la hawa watu wanaoleta dhiki ya matumizi mabaya ya barabara litapungua, vyenginevyo tutaendelea kulizungumza suala hili kila siku kwa sababu wanajua hawa kwamba hakuna jambo watakalofanywa.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa na jambo jengine ambalo nataka kulizungumza ambalo ni ukaguzi. Ukaguzi serikali nilitaka kujua ina mpango gani wa kuanzisha hii adhabu ya pale pale nao wanapokwenda kuvikagua vile vyombo ambavyo haviko vizuri kabla ya kuvipa tena leseni mpya. Kwa sababu tumeona kwamba wanapokwenda kukagua pale wanawaambia aa wewe rudi karekebishe gari yako, lakini pale inatakiwa chombo kimekwenda hakikukidhi haja wanapewa adhabu, hii itatusaidia sisi katika kuchukua tahadhari kwa madereva na wenye vyombo kurekebisha vyombo vyao na kuwa makini kwa ajili ya matumizi ya barabara.

Pia sambamba na hili la adhabu ya papo kwa papo ilikuwa kuna haja ya wizara na Mahkama wakakaa pamoja kwa ajili ya kushughulikia kesi hizi ili pale watakapokwenda na itakapokuwa chombo kimepatikana au dereva kapatikana na hatia anapigwa faini ambayo itamzuia yeye kutokurejea tena kwa kosa kama lile na mwengine atakua anaogopa kufanya kosa kama lile.

Mheshimiwa jambo jengine ambalo nimeliona wakati zinapotokea ajali huwa kuna tatizo la kwamba lazima apatikane VECO kutoka mawasiliano. Polisi wamemkamata gari inaletwa kituoni, lakini unaambiwa mpaka apatikane mkaguzi kutoka Idara ya Mawasiliano. Mimi naomba sana kwamba yawepo mashirikiano na wizara yake iridhie kuwaruhusu polisi kufanya ukaguzi huo. Kwa sababu inapotokea hii inachukua muda kwa chombo kukaguliwa na huwezi kukipeleka chombo Mahkamani bila ya kukaguliwa. Kwa hivyo, mimi naomba awepo VECO yule wa polisi naye awe na uwezo wa kuvikagua vyombo hivi wakati vinapopata ajali au vinaposababisha ajali.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nende sasa katika *page* namba 15 ya ujenzi wa barabara, naomba kusoma kidogo. 'Mradi huu unajumuisha Ujenzi wa barabara ya kutoka Ole-Kengeja yenye urefu wa km 35. Hadi kufikia Machi, 17 jumla ya kilomita 11 zimekamilika kwa kuwekewa kifusi kuanzia Ole hadi Mfikiwa. Aidha, urefu wa km 6.9 zimewekewa kifusi tabaka ya mwisho...". Lakini tukija katika matumizi na utendaji wa kazi nauona katika maelezo yao iko tofauti, kwamba pesa wamepata asilimia 40 lakini utendaji wa kazi wako asilimia 38 kwa nini upatikanaji wa pesa na utendaji wa kazi usiwiane? Ningeomba nijue hilo. Lakini pia nataka nijue kuhusu habari ya barabara ya Wete-Chake Chake njia kongwe.

Mhe. Mwenyekiti, wenzangu wamezungumza mengi kuhusu habari ya barabara, lakini mimi kuna kitu kimoja ambacho nataka nikishauri ambacho ni hivi juzi tu nimejibiwa swali hili, lakini

narudia tena kwamba kama fedha zimeshapatikana na wenzangu wamesema hapa ni sababu gani inayozuwia wale watu wasilipwe fidia zao wakaanza kuondoka mapema pale, ili kupisha ule ujenzi wa barabara ile. Pia nilitaka kujua huu ujenzi wa kilomita 22 wa barabara hii ni kuanzia Wete mpaka Meli Tano au ni kuanzia Wete mpaka Machomane au Gombani. Nilitaka nijue huu ujenzi utaishia wapi.

Sambamba na hilo nikienda kwenye kitabu huku naona wamejipangia shilingi 25 bilioni kwa ujenzi wa barabara hiyo, lakini bila shaka humu itakuwa *VAT* tayari imeingizwa. Lakini ukii-*calculate* hiyo pesa ambayo imetajwa itakuja karibia 1.17 bilioni kwa kilomita je, tuulize barabara itakayojengwa itakuwa na upana gani? Je, hii fedha ya bilioni 1.17 itaweza kukidhi barabara ya kiwango ambacho kitakuwa kina sifa ya kutumika kwa muda mrefu? Isijekuwa tunajenga barabara kwa sababu tumefuata urahisi keshokutwa tukaja tukapata kama ambayo wenzangu wameanza kuyazungumza.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nina kilio kwa barabara ya Konde-Wete, barabara imejengwa na nataka niambiwe barabara ile imegharimu kiasi gani cha fedha. Leo barabara imebonyea imeshaanza kuwa upande, kuna babu yagu mimi alikuwa akinambia ishakhatafu kama punda aliyebeba mzigo upande mmoja. Mimi naona iko haja ya kuwatumia wataalamu wetu wa ndani wa wizara, mimi nakubaliana zaidi na kuwapa UUB kazi hizi kuliko kuwapa hata hao wakandarasi wengine. Mimi naomba sana serikali kwa kutumia wataalamu wetu wa wizara tufanyeni tununueni vifaa na tuwawezeshe UUB kuwapa pesa na vifaa vya kujengea barabara, vyenginevyo Mheshimiwa hakuna mkandarasi yeyote atakayekubali kuchukua fedha yake kwa kuiweka kwa muda mrefu, watatupa *guarantee* ya muda mfupi, watatujengea barabara zilizokuwa hazina kiwango, lakini ikiwa UUB vijana wetu tuliowatuma, tuliowasomesha zana tunazo, pahali pameharibika wao ni wepesi kwenda kufanya kazi hiyo kuliko kuwapa watu

ikisha ikawa kazi zetu sisi hazina *guarantee*. Barabara zetu kukosa *guarantee* ni kilio kikubwa pamoja na kuwa wafadhili wanakuwa na masharti yao, lakini ni vyema na sisi tukaangalia uzito uliokuwa unatukabili. Sisi ni nchi masikini tunapojenga barabara tunategemea kwamba kitu kile kidumu kwa muda mrefu, leo kuja kutujengea barabara baada ya miaka mitatu ikawa imeshaanza kuchakaa kama alivyonijibu juzi kwamba barabara ya Konde-Wete imeanza kuchakaa na ndio ukweli wenyewe kwamba imeanza kuchakaa. Barabara imechakaa kwa muda mfupi.

Kwa hiyo, mimi *concern* yangu kwa hili nakubaliana na wenzangu kwamba miradi mingi ya ujenzi wa barabara wapewe UUB sio mtu mwengine na mimi kwa hili Mhe. Waziri niko radhi kwa lolote, lakini kuhakikisha kwamba UUB wanapewa *set* za vifaa vya ujenzi ili wao imani yangu kuwa wao wanaweza kutengeneza barabara nzuri kuliko hata hao wengine. Leo ukienda kwenye barabara iliyojengwa na H.Young barabara imepasuka, barabara ya Mtambwe ile yote imeanza kufanya crake mpaka imeanza kujengwa sehemu nyengine, imezibwa viraka, barabara hata miaka miwili haijafika.

Mhe. Mwenyekiti, tukiwatumia watu wetu UUB ni vijana wetu tumewaajiri, tumewasomesha, wanalipwa mshahara na serikali imani yangu kwamba wao wanaweza kufanya vizuri kuliko mashirika mengine na makampuni kutoka nje.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nakuja katika ukurasa wa 11, niliruka lakini nilitaka nije kwenye ukurasa huo kuulizia suala la Beit-el-Ajaib. Kwenye bajeti yake ya mwaka 2016/2017 alisema kwamba, Serikali ya Oman kupitia idara yake walikubali kutusaidia kufanya ukarabati wa lile jengo. Mimi nilitaka kujua je hawa Waomani wameghairi tena kutupa hizi pesa au vipi. Kama hawajaghairi ni kitu gani kilichosababisha mpaka leo ule ukarabati wa lile jengo ukawa haujakamilika.

Nikitoka hapo naendelea kidogo kuchangia mbio mbio kwa sababu naogopa kupigiwa kengele, nilikuwa nataka nijue kuhusu uwiano na taasisi zinazojitegemea. Nimeona hapa kwamba Idara ya Nyumba kuhusu idara hiyo kwamba wao hawa wanajitegemea, lakini ukiangalia matumizi yao ni makubwa kuliko wanachokikusanya. Sasa ikiwa hii ni taasisi inayojitegemea haya makadirio yao ya kutumia na wao tushaambiwa wanajitegemea zinatoka wapi, wanazipata kutoka wapi. Wito wangu ni kwamba, kwa sababu sote sisi tunachangia na tunajenga nyumba moja mimi nilikuwa napendekeza kwamba isitajwe taasisi inayojitegemea fedha zote za serikali zipelekwe Hazina, anayetaka aombe kupitia Hazina.

Mhe. Mwenyekiti, leo ukiitizama *airport* wanayosema wao wanakusanya ukienda makusanyo yao na matumizi ni tofauti, wanachokiomba na wanachotegemea kukitumia ni tofauti, utakuta karibu kuna 1.945 bilion ambapo ni *different,* ambapo zitatoka wapi pesa hizo ikiwa wao wanajiegemea. Wito wangu naiomba sana seriki na Wiara ya Fedha, naomba sana serikali tubadilisheni mwelekeo kwamba pesa zetu zote za serikali ziingie Hazina ikisha kama ni *airport,* ni bandari, aombe pesa kutoka Hazina. Haya ya kusema kwamba huyu awe na mamlaka ya kutumia, huyu ana mamlaka ya kujiendesha hili litatupeleka pabaya bado mzigo utarudi Wizara ya Fedha na Wizara ya Fedha watakuwa hawana uwezo wa kukidhi kuviendesha hivi. Kwa sababu...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa una dakika mbili.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa nimepita mbio mbio mwisho narudia tena kutoa wito na mimi sizuwii bajeti nasema naunga mkono bajeti hii, lakini namuomba sana waziri ile ahadi ambayo ananipa ya barabara yangu ya Konde-Msuka barabara ile namuomba Mheshimiwa kwa heshima na taadhima tukimaliza bajeti hii wananchi wangu wa Msuka wanataka wasikie na waone wanafika Konde. Namuomba sana kazi hiyo

aitekeleze ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Omar Seif, sasa niombe kumwita Mhe. Bahati Khamis Kombo kuendelea kuchangia wizara hii na baadae atafuatiwa na Mhe. Masoud Abrahman na Mhe. Mussa Foum Mussa ajitayarishe.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwanza kabisa nichukue fursa hii ya kumpongeza sana Mhe. Rais wetu kwa kuwaondolea wananchi matatizo mbali mbali yanayohusiana na barabara.

Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa ya pekee ya kuwapongeza Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji lakini shukurani za kepee ziende kwa Katibu Mkuu pamoja na Afisa Mdhamini wake kwa kazi kubwa ambayo wameifanya kwa kipindi kifupi tu, baada ya kutokea maafa Pemba. Tunawapongeza sana juhudi kubwa sana aliyoifanya katibu huyu na leo tunaona kwamba zile barabara zetu katika hali ya kawaida.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa mimi nitakwenda moja kwa moja katika mradi wa barabara. Mheshimiwa tunajenga barabara ili kuwaondoshea wananchi matatizo, lakini tumeona kwamba kuna barabara ambazo zimejengwa karibuni tu hivi sasa hazifai zikiwemo barabara ya Kengeja, Chambani, Mtambile na pia barabara inayotoka Chanjamjawiri kuelekea Kilindi. Barabara zile zilijengwa kwa mkono ili kuondosha na serikali isiingie hasara kubwa, lakini tukiangalia barabara zile tumepata mtihani. Sasa naiomba wizara ili tuweze kuondokana na mtihani ule basi wizara mara hii iwe makini sana, iwe makini kufuatilia zaidi kwa wale wakandarasi ambao tunawapa zile *tender* tusiwe mbali nao. Kwa sababu tuna wasiwasi mkubwa wa kwamba watendaji wetu wanakaa ofisini na kule wanawaamini sana wale wakandarasi. Sasa nawaomba watendaji wetu tuondoshe ile dhana ya

kuwaamini tu na sisi wenyewe tuwe makini ili serikali isiendelee kuingia hasara.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende moja kwa moja katika barabara yetu ya Ole-Kengeja. Barabara hii tunashukuru sana na tunamshukuru sana Afisa Mdhamini kwa usimamizi wake mzuri anaoufanya, lakini pia kuna kitu kidogo wananchi kimewapa shida, kwamba barabara ile ya Ole-Kengeja katika eneo la Chaka la Kati Mheshimiwa ile barabara mwanzo ilipopimwa ilikuwa iko sawasawa na iko vizuri, lakini ni juzi tu walipokwenda watendaji wanaoweka X katika majumba ile shemu ambayo imekusudiwa mwanzo imeachwa na badala yake zimetiwa X zile nyumba nyengine. Hapa kidogo Mhe. Mwenyekiti, tunaomba wananchi waelimishwe wajue ni sababu gani zilizofanya mpaka barabara ile ikaondolewa ile sehemu ya mwanzo na badala yake ikawekwa katika sehemu nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile wananchi hawa wana wasiwasi kwamba ni lini watalipwa fedha yao ya zile nyumba na kwa sababu baadhi yao hawana viwanja na sasa hivi imewabidi kutafuta viwanja kwa hali yoyote. Kwa hivyo, wanaomba wapewe hizi pesa mapema ili wasije wakaadhirika wakati yatakapovunjwa majumba yale.

Vile vile hapa nilizungumza ndani ya wiki mbili zilizopita kwamba Mhe Rais wakati anagombea alipokuwa kwenye kampeni katika Kiwanja cha Chokocho aliiwekea ahadi barabara ya Ukutini kuelekea Matele. Lakini ni juzi tu baada ya kupita hawa watu wanaoweka X katika majumba barabara ile imeachwa na hivi sasa tayari wako karibu na Kiwani**.** Wananchi wanataka kujua je, hii ahadi ya Rais imeondolewa au bado ipo. Kama ipo basi na wao wanaomba wachukuliwe hatua za haraka kwa sababu ile barabara hivi sasa haipitiki daraja ni mbovu na yanapita magari makubwa.

Mhe Mwenyekiti, niende moja kwa moja katika eneo la Zawadini. Nadhani Mhe. Naibu Waziri ni shuhuda tulipopita katika eneo la pale Zawadini pana daraja kubwa na daraja lile ndio liliondoshea amani wananchi hivi sasa kwa sababu ya kuleta maharibiko makubwa yaliyotokea ndani na mvua hizi kubwa tulizonazo. Sasa barabara ile inahitaji kufanyiwa matengenezo ya kina kwa lile daraja ambalo liko pale.

Daraja lile Mhe. Mwenyekiti, liko chini sana maji hivi sasa yanafika katika ile skuli wanayosomea watoto pale watoto wale ni wadogo na kama tunavyojua mtoto ni mtoto leo tumepata maafa ya karibu tu kufa kwa mtoto na hayuko katika maji ilikuwa ni Madrassa. Lakini leo pale pana skuli kubwa na pia zile nyumba zilizopo pale hivi sasa wananchi wana hofu kubwa sana endapo itaendelea kunyesha mvua. Kwa hivyo, naomba Mhe. Mwenyekiti, suala hili Katibu, Afisa Mdhamini waende kuliangalia lile daraja na ipewe ufumbuzi wa haraka.

Mhe. Mwenyekiti, nije moja kwa moja katika Bandari yetu iliyopo Mkoani. Mhe. Mwenyekiti, nadhani hapa mmemsikia Mhe. Zulfa aliizungumzia Bandari ile jinsi ya magari yalivyo. Lakini pia mimi naitilia mkazo zaidi Bandari ile kule ndani wananchi wanapata tabu sana na watoto kwa sababu masafa yaliopo pale ni makubwa. Tunaomba alau wajengewe sehemu ndogo pale kati na kati ili waweze kujificha mvua.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nje pale yanapokaa magari, yale magari kwa kweli sehemu iliyopo ni ndogo tunaiona sote. Lakini ni vizuri wale madereva wakapewa taalamu nzuri kwa sababu wanaopita pale ni wananchi wengine wana watoto, lakini wanapokuja abiria kutoka melini wao kwao ni kuchukuwa abiria tu hawajali mtu yoyoye. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, iko haja ya kuangaliwa zaidi katika uwanja ule yanapokaa magari.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile katika eneo lile lile la Bandari tuone kwamba pale kipo kikosi cha Wazima moto na magari yanakaa mpaka sehemu ya mlango hasa ya Wazimamoto. Kwa kweli lile ni tatizo. Tunaiomba wizara iangalie kwa kina ili na wale askari walioko pale waweze kupata fursa nzuri ya kuondokana na lile tatizo la msongomano ulioko mbele yao.

Mhe. Mwenyekiti, nije moja kwa moja katika ujenzi na nyumba. Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Afisi hii wanaoshughulikia na mambo ya ujenzi na nyumba. Kwa kweli walifanya kazi kubwa sana Madungu pale ya kuondosha ule uchafu wote uliokuwepo katika nyumba zile. Hivi sasa ukipita kwa kweli unapita unaridhika vizuri sana.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia nyumba zilizopo eneo la Miembeni pale Kilimatinde. Zile nyumba ni mbovu kwa kweli zile nyumba zina mtihani mkubwa sana, niseme kwamba zile nyumba ni sawa sawa na nyumba zilizoko Mji kongwe. Kwa hivyo, naiomba wizara iziangalie zile nyumba kwa sababu wanakaa wananchi na mporomoko ukitokea ule unaweza ukatokea usiku tutakuja kuwa wananchi wengi sana. Kwa hivyo, naiomba serikali, naiomba wizara iziangalie nyumba zile kwa kina sana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitokuwa na mengi sana baada ya hayo naunga mkono hotuba hii asilimia tisini na tano na tano naziacha mpaka nitakapopata jawabu ya Chaka la Kati. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Bahati Khamis Kombo sasa naomba nimwite Mhe. Masoud Abdraham Masoud na Mhe. Mussa Foum Mussa ajitayarishe pamoja na Mhe. Mwanaidi Kassim.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kukutana hapa kwenye Baraza hili tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi moja kwa moja nianze na suala la ujenzi wa barabara na hasa nizungumzie barabara inayotoka Mdo, Kizimbani kwenda Miwani. Mhe. Mwenyekiti, barabara hii bajeti ya 2016/2017 ilikuwa tayari inaonekana kwenye kitabu hichi, lakini kwa bahati mbaya utekelezaji wake haukuonekana. Mhe. Mwenyekiti, na mara hii inaonekana iko katika bajeti, lakini mwaka jana kwenye kipaumbele haikuwepo na mwaka huu kwenye kipaombele haikuwepo. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, imeanza kunipa wasi wasi mwaka jana kwenye kipaumbele haikuwepo haikujengwa mwaka huu kwenye kipaumbele haipo lakini kwenye kiambatanisho inaonekana.

Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri atakapokuja atwambie barabara hii ina mpango wa kujewga mwaka gani, kwa sababu barabara hii sawa sawa na barabara zinazokwenda kwenye *beach* ambako wanakwenda watalii. Mhe. Mwenyekiti, barabara hii wakulima wengi wanaitegemea wakulima wanaotoka Kiboje, Miwani na maeneo ya Kizimbani lazima wapite na magari yao wakiwa na mizigo. Sasa hivi wakulima wale wanapata usumbufu mkubwa sana kwa sababu mvua hizi barabara zimechimbika kwa hivyo inabidi wazunguke Ndagaa wapite Bumbwi Sudi, Kitundu waelekee mjini. Kwa hiyo, kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, ahadi hii ni ya muda mrefu haidhuri inaonekana lakini kwenye kipaumbele haionekani. Kwa hivyo, Mhe. Waziri atakapokuja atwambie.

Mhe. Mwenyekiti, barabara za ndani, barabara za ndani Mhe. Waziri wa Tawala za Mikoa mara nyingi huwa anazisema kuwa watajenga watu wa Halmashauri au Manispaa. Lakini Mhe. Mwenyekiti, sina uhakika bajeti yao kama inatoka ndani ya Halmashauri na Manispaa au bajeti yao inatoka Mfuko wa

Barabara kwa sababu inawezekana ikawa kwenye Mfuko wa Barabara hatupati lakini pia na Halmashauri hawana bajeti za kujenga barabara.

Kwa hivyo, nimuombe tu Mhe. Waziri atakapokuja atwambie yeye mwenye Mfuko wa Barabara anategemea atutasaidia kwenye barabara gani angalau na sisi kwa mvua hizi zilizonyesha kipindi hichi barabara nyingi zimekuwa mbovu hasa eneo la Bububu, Kizimbani, Dole wakulima hata lile gari la ng'ombe linashindikana kupitishwa kwenda kuchukuwa mazao yao kwa ajili ya kupeleka mjini na kupata fedha kwa ajili ya kujikimu na maisha haya ambao tunayaendesha sasa hivi.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende Idara ya Usafiri na Leseni, wenzangu wamelizungumzia suala la usumbufu mkubwa ambao unapatikana wakati wa upasishaji wa magari. Ni kweli mimi mwenyewe nishawahi kwenda na nikapoteza siku mbili bado huduma haijamilika. Unaanza kwenda kwenye magari kupasisha ukitoka hapo uende ukachukuwe risiti Mwanakwerekwe, ukitoka hapo urudi tena Karakana ni usumbufu.

Kwa kweli tunaomba sana wenzetu hawa zile huduma zote waziweke karibu pamoja na hawa Benki ya *PBZ* ili wananchi wasipoteze muda wa siku moja au mbili kufuata huduma na bahati nzuri sana hata hawa watu wa Idara ya Usafiri na Leseni walioko pale Mwanakwerekwe hawatumii mashine za kompyuta wanaandika kwa kalamu tu kwa nini wasiende pale ili wakawaidia wananchi wasipate usumbufu mkubwa. Mhe. Mwenyekiti, nionmbe sana Mkurugenzi hili ajitahidi ili arahishe kazi.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo niende kwenye suala la Alama za barabarani wenzangu wamelizungumzia na mimi naomba nilizungumzie. Suala hili kwa sasa hivi imekuwa kama tatizo, kwa sababu sasa hivi tukikubali, tukikataa askari

wanafanya majukumu yao, lakini kati wanapofanya majukumu yao pia wanasumbua wananchi. Bahati nzuri mimi Baraza lililopita nilikuwa naondoka nyumbani kwangu muda wa saa mbili na nusu nikafika maeneo ya Sheli ya Kitundu wakati huo na gari yangu nilikuwa natembea *speed* 50-60 wakanimurika na kamera lao wakanambia natembea *speed* 69. Kwa hivyo, wananishitaki, nikawaomba sana wakataa wakanambia tupe funguo nikataa na mimi wakanambia basi tupe leseni yako nikawapa leseni. Eneo lile pale halina majumba hakuna alama ya aina yoyote lakini wakaamua kunishitaki kwa kwenda *speed* 69, ni usumbufu kwa sababu alama haipo mimi sikujua kama pale hutakiwi kwenda zaidi ya *speed* 69. Kwa hivyo, niombe sana watu wa Idara ya Barabara waweke alama ili na sisi tuwe tunatambua katika eneo hili tutembee *speed* ili tusipate usumbufu, lakini pia wasipate usumbufu wananchi wetu kwa askari.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo niende moja kwa moja wananchi au matajiri wenye magari, sasa hivi imekuwa mtindo Mhe. Mwenyekiti, barabara ya Dole na barabara ya Mndo kwenda Bububu imekuwa ni msitu wa kuchomea magari, ukiikuta gari pale magharibi, magharibi inazubaa zubaa mara unaikuta imeshawashwa moto sina uhakika kama wanatengeneza mpango ili wapate kulipia magari yao bima lakini pale barabara sasa hivi inaharibika, zile barabara zimejengwa kwa gharama kubwa ya serikali na zile ni nguvu za wananchi, lakini wananchi wanaamua kuja kuchoma magari yao yaliokwisha kuwa mabovu ili baadae wakalipwe na Shirika la Bima.

Niombe sana pale patakapoonekana na kwa sababu inakuwa ni mchezo wa kawaida barabara kila baada ya hatua 20 unakuta kuna gari ilichomwa mwezi uliopita na hatua nyengine unakuta kuna gari nyengine ilichomwa. Kwa hivyo, inaonekana kama ni mchezo wa kawaida. Kwa hivyo, waangaliwe sana kisheria watu wanaomiliki zile gari zinazochomwa kwa eneo hilo hapo kila baada ya muda.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo kuna malalamiko ya wananchi ambao tayari sasa hivi kuna barabara inataka kujengwa hii ya Mahonda. Mhe. Mwenyekiti, kuna baadhi ya wananchi ambao nyumba zao ziko karibu na barabara walitakiwa wahamishe nyumba zao. Lakini kwa bahati mbaya mtu anaweza kuja wataalamu wale wakasema wewe utatoa tofali tatu kwenye nyumba yako na wengine wamelipwa ashilingi milioni moja na nusu, wengine wanasema wamelipwa shilingi milioni mbili, wengine milioni tatu.

Sasa nimuombe tu Mhe. Waziri atakapokuja atwambie ni kigezo gani anachotumia mpaka mwananchi yule anaambiwa atoe tofali zake za mbele halafu alipwe shilingi milioni moja na nusu au milioni mbili au milioni tatu na kwa sababu ujenzi sasa hivi ni gharama na mtu anapojenga anakuwa kaweka ramani yake ya nyumba lakini hatima yake unaambiwa ukate kwenye eneo hilo ili barabara ipate kujengwa na mwanachi huyo tayari keshaweka ramani yake nzuri ya kuhakikisha nyumba yake iko katika utaratibu ambao mwenyewe kajiwekea.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nichukuwe nafasi kumshukuru sana Mhe. Waziri lakini pia nimshukuru Naibu Waziri kwa kazi nzuri anazofanya lakini Katibu Mkuu pamoja na watendaji wake. Lakini Mhe. Mwenyekiti, matengenezo ya barabara sasa hivi kwanza niwape pole Mkurugenzi wa barabara na timu yake kwa jinsi ya barabara zilivyochimbika hasa hasa barabara ya Bububu imechimbika sana, Mhe. Asha Abdalla Mussa wa Kiwengwa alisema kidogo tunajitia hasara kwenda kutia kifusi kwenye yale mashimo.

Lakini mimi niwapongeze kwa juhudi zao za kwenda kufukia yale mashimo. Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi barabara ya Bububu ilivyochimbika kama hawatofanya kazi ya kwenda kuziba yale mashimo basi ajali nyingi zitatokea kwa sababu mashimo ni mengi halafu mashimo makubwa sana. Lakini Mhe. Mwenyekiti,

mashimo haya yalianza kidogo kidogo hayakuwa tu mashimo makubwa moja kwa moja. Sasa inaonekana hawa watu wa Idara ya Barabara kwenye bajeti yao ya matengenezo ya barabara labda itakuwa kifungu hicho hakipo au serikali bado hakijakiidhinisha.

Niombe sana katika bajeti hii kuwe na fungu kubwa haidhuru imejionesha lakini inajionesha kwa sababu ya hii mvua lakini hata kama mvua haipo matengenezo ya barabara iwe ni kitu cha lazima. Sasa hivi kuna barabara nyingi wenzangu wametaja barabara za Pemba lakini hata barabara za Unguja barabara inayotoka Kitundu kwenda Ndagaa sasa hivi mashimo mengi sana, lakini yameanza madogo baadae yanakuwa makubwa.

Sasa niwaombe sana watu wa Idara ya Barabara hasa niiombe serikali itenge mfuko kubwa watalaamu mimi naamini Idara ya Barabara wapo wa kutusaidia na ndio maana kuna Mhe. Omar Seif Abeid kuwa ikiwezekana hata hizi barabara zetu wa *UUB* wana uwezo wa kuzijenga na ikawa ziko kwenye kiwango. Kuna barabara ngapi tunapita huko ni nzuri kabisa na zimejengwa na Serikali ya SMZ.

Kwa hivyo, niombe sana fungu hili la matengenezo barabara kama lipo liongezewe kidogo ili barabara zetu ambazo zimepata mtihani huu wa mvua na kufanya mashimo makubwa sana wahakikishe kwa muda mfupi wanatengeneza kwa sababu tusipoziba ufa tutakuja kujenga ukuta na kwa sababu mashimo ni mengi ajali zitakuja kutokea nyingi, bara bara yetu ya Bububu ina mashimo mengi lakini na magari ni mengi.

Niombe sana Waziri pamoja na Naibu Waziri na watendaji wake wahakikishe ile barabara japo kifusi kwenye mashimo wakatie haraka haraka kwa sababu wanafanya ukarabati lakini kwa *speed* ndogo wakatie kwa haraka haraka ili kuepusha ajali ambazo zinaweza zikatokea.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, mimi niunge mkono hotuba hii baada ya Mhe. Waziri atakaponipa majibu kuwa barabara yangu ya Mndo inayokwenda Kiboje huko itajengwa basi itakuwa asilimia mia moja. Lakini kama hajanipa jibu zuri basi nitakuwa na asilimia tisini na tano na roho yangu itakuwa haikufurahi sana. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa ruhusa kuchangia.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwepo hapa kwa wakati huu tukiwa wazima na salama.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo pia nimpongeze Mhe. Waziri na Mhe. Naibu Waziri na Katibu Mkuu pamoja na watendaji wao wote kwa mashirikiano makubwa wanayotupa sisi wenzao. Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo na mimi nitaanza mchango wangu hasa kwa masuala ya barabara.

Kwanza nitaanza kutoa pongezi nitaishukuru serikali kupitia Wizara hii ya Mawasiliano na Ujenzi kwa kutujengea barabara ya Mgagadu - Kiwani kwa kiwango cha lami. Mhe. Mwenyekiti, kwa kipindi kikubwa sana tulikuwa tukihangaika sana hasa wakati wa mvua kutoka Mgagadu - Kiwani. Lakini leo tunamshukuru Mwenyezi Mungu barabara ile imemalizika ingawaje baada ya mvua zilizitokea kumetoa athari katika Daraja la Kiwani barabara pale imeharibika lakini kama alivyozungumza humu kwamba zitafanyiwa matengenezo barabara zile. Kwa hivyo, naipongeza serikali kwa jitihada zake hizo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo vile vile nataka nichangie kidogo kuhusiana na barabara ya Mtambile - Mwambe hii hasa nataka kuzungumzia jambo hususan. Mhe. Mwenyekiti, barabara hizi zimejengwa kwa kiwango hafifu kidogo na zilikuwa nyingi

hususan katika wilaya yetu ya Mkoani. Mhe. Mwenyekiti, barabara hizi zilipojengwa watu waliharibiwa vipando vyao viling'olewa na muda umeshakuwa mrefu lakini suala hili nimelizungumza hapa mwaka jana na huko nyuma limeshazungumzwa sana, wananchi wamelifuatilia kuhusu kulipwa fidia yao kwa muda mrefu mpaka hivi sasa tena wamefika pahala wametulia wamechoka. Sasa na mara hii nimesema vile vile suala hili nilizungumze tena.

Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa kutoa majibu basi atupe maelezo kwamba je, hawa wananchi watalipwa lini pesa zao muda umekuwa mkubwa na humu katika bajeti yake sioni ile sehemu inayosema kwamba kuna fungu ambalo kuwa limepangwa kwa ajili ya kulipa fidia wananchi kwa sababu ninavyofahamu mimi si barabara hii tu, hata barabara ya Gando iko huko Mheshimiwa wa Gando siku zote na yeye anapiga kelele.

Sasa tunamuomba Mhe. Waziri mara hii tena bajeti ya mwakani tusije hapa tukadai tena suala hili, muda umekuwa mkubwa inakaribia tena miaka minane au tisa tokea ijengwe barabara hii, wananchi wamechoka kudai fidia yao hii. Kwa hivyo, mara hii tunaiomba serikali kwa kupitia wizara muhakikishe kwamba mnapanga lengo maalum la hawa watu kulipwa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo kila mtu anapolia hulia mama yangu, na mimi nitazungumzia tena barabara ya Ole Kengeja. Mhe. Mwenyekiti, kwanza niipongeze serikali kwa kuona kwamba iko haja barabara ile ya Ole Kengeja kujegwa, kwa sababu ni barabara itakayokuwa mpya ujenzi wake. Lakini muda umekuwa mkubwa barabara hii imeanza kuzungumzwa zaidi ya miaka 10 nyuma na ujenzi wake unakwenda kwa kusuasua.

Mhe. Mwenyekiti, ile barabara kwa vile ni mpya ina gharama kubwa sana, hususan wakikaribia hapo Ndaambani Vizuke, pana bonde pale la maji kubwa sana. Sasa namuomba Mhe. Waziri barabara ya Ole Kengeja iangaliwe vizuri kabisa, tena tunamuomba Mhe. Waziri ile barabara ijengwe kwa kiwango madhubuti, kwa sababu sehemu zake ni mbovu kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile niseme kwamba ile barabara itakuwa ni barabara kubwa, lakini inaonesha kwamba ule ujenzi wake bado wananchi nyumba zao ziko karibu na ile barabara, sasa sijui kwamba wale wananchi hawajalipwa, au upimaji wake ukoje. Kwa sababu sababu kubwa ya watu wa Vitongoji mara hii kuingiliwa na maji wale waliokuwa karibu na ile barabara, ni sababu ya ile barabara haikuwekewa misingi vizuri. Sasa naiomba wizara hivi sasa imeshaanza kutia nyumba X hususan katika jimbo langu, kuanzia Kichaka mpaka Nanguji.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naiomba wizara kwamba wale watu waliowekewa X basi kabla ya ule ujenzi kuanza basi waanze kulipwa mwanzo, kwa sababu wale watu zile ni nyumba zao wanazoishi na hawana uwezo wa kujenga kabla ya kulipwa. Kwa hivyo, tunaiomba serikali ianze kulipa mwanzo fidia baadae ndio ije ivunje nyumba, kwa sababu mtu anapolipwa mwanzo atajua aelekee wapi.

Vile vile, kwa vile barabara itakuwa ni barabara kuu iweke mwisho kwamba mwisho watu wafike ikiwa mita 15, 10 au 20 basi ziwekwe kabisa, baada ya kwisha kupimwa tena asije kutokea mtu kuja karibu na barabara, haya ndio makosa yetu tunayoyafanya. Kwa sababu mara nyingi tunapojenga barabara hatuweki viwango vya mwisho, kwamba mtu akifika hapa huku asije ni sehemu ya barabara. Sasa naiomba serikali kwa kupitia wizara hii kwamba jambo hili katika ujenzi hususan wa barabara ile basi tuweke sehemu ambazo itakuwa ni mwisho kwamba

mwananchi yeyote akitaka kujenga kitu chochote hana ruhusa ya kuingia huku.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo vile vile nizungumzie Shirika la Meli na Uwakala. Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza nilipongeze shirika hili, halafu niipongeze serikali kwa kuliona tatizo la usafiri na wakatununulia meli hii nzuri Mapinduzi II.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka Mhe. Waziri atakapokuja aje anifahamishe hapa, kwa sababu kipindi kilichopita meli yetu imefanya safari za ndani 85. Lakini mara hii imepangiwa 168. Sasa nimuulize tu Mhe. Waziri je, hii meli itabadilishiwa *route* za kwenda tena Pemba na Unguja au *route* yake itakuwa ni hii hii, na ikiwa ni hii hii je, hapa hatuoni kwamba lengo lililowekwa ni kubwa zaidi. Kwa sababu kule tulikuwa na 85 kipindi kilichopita, lakini mara hii tumeweka 168, lakini ukiangalia hizi ni sehemu za safari za ndani. Hapa mimi nimeingiwa na wasi wasi kwamba hili lengo lililowekwa ni kubwa mno, kwa sababu meli ni hii hii moja ingekuwa angalau tuna meli mbili, meli iliopo ya pili ni MV Maendeleo lakini hapa tumeambiwa kwamba haifanyi kazi kwa sababu ya uchakavu wake. Kwa hivyo, je mtabadilisha *route* au *route* yenyewe itakuwa ni ile ile ya kawaida.

Halafu vile vile Mhe. Mwenyekiti, hapa tumeambiwa kwamba abiria pia katika kipindi kilichopita walikuwa 161,477, lakini abiria wanaotarajiwa mara hii ni 262,680 abiria wanaotarajiwa. Lakini vile vile nauliza kwamba hawa abiria mara hii wamepangwa wengi na safari ingawaje zimepangwa nyingi, lakini mimi wasiwasi wangu ni kwamba je hizo route zitabadilishwa hili hawa abiria waongezeke kutoka 161,477 hadi kufika 262,680.

Halafu vile vile Mhe. Mwenyekiti, kuna tani hizi zimepangwa, lakini huku kumeelezwa pamoja na magari 1,320 je, haya magari yatapakiwa kwa kutumia meli ipi, kwa sababu hii meli yetu ya Mapinduzi II tunaambiwa kwamba haitaki kutolewa zile sehemu

ambazo zilizopo, lakini hivi sasa tukienda na magari yetu tunataka kupakiliwa kupeleka Pemba huwa ni shida na suala hili mara nyingi huwa linazungumzwa. Lakini hapa imepangwa kwamba itapakia magari 1,320 yatapakiwa sehemu gani. Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Waziri atakapokuja basi na hili atueleze kwamba sasa tutatumia kipengele gani ili huu mzigo wa magari nao uweze kupakiwa.

Mhe. Mwenyekiti, pia niulize kwamba hii meli ya MV Maendeleo kila siku husika kwamba inataka kuuzwa zaidi ya mwaka hivi sasa. Je, hili suala hajatokea mteja wa kununua au bado serikali haijajipanga kwa sababu naona muda umeshakuwa mkubwa, tunaimba nyimbo tu tunataka kuuza meli, tatizo liko wapi hajatokea mteja au bado serikali haijaamua kwamba ile meli iuze kweli.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niulize kwamba na hii MV Ukombozi huko nyuma nilisikia nayo inataka kuuzwa, lakini hapa imeelezwa kwamba bado tutaendelea kuikodisha kwa wale wale wateja wetu wanaokodi. Je, hapa tushike lipi tutaendelea kukodisha au nayo inauzwa. Mhe. Waziri utakapokuja na hili tueleze ili tupate uhakika.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo vile vile mimi nizungumzie habari ya hizi *traffic light*. Hizi zimezungumzwa sehemu za kuwekwa mimi sina matatizo nazo. Lakini nilikuwa na wazo kwamba kwa maoni yangu kuna sehemu ambazo kuwa ni mbaya zaidi na ambazo zinastahiki nazo zipewe kipaumbele.

Kwa mfano, hapa Magomeni kwenda Mwanakwerekwe *round about* ile pale, pale kiukweli napo panakuwa na *traffic* kubwa sana ya magari. Halafu vile vile Amani. Sasa namuomba Mhe. Waziri tuangalie sehemu ambazo nazo zina tatizo kubwa zaidi baadae ndio twende sehemu nyengine.lakini vile vile na hizi nimesema nizizungumze muziangalie, wapi pana umuhimu zaidi

basi tuipeleke hiyo huduma. Kwa sababu pale Amani kuna baadhi ya siku nyengine ikifika Magharibi pale unaweza ukakaa kwa muda wa saa hujapata kupita.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo kwa vile wengi wamezungumza, mimi tu namuomba Mhe. Waziri atakapokuja, anijibu tatizo zaidi lililonithakili mimi, naunga mkono hotuba yake hii kwa asilimia 90, lakini namuomba Mhe. Waziri atakapokuja atowe uhakika wa lini wananchi walioharibiwa vipando vyao kwa ujenzi wa barabara ya Mtambile Mwambe watalipwa haki yao kwa sababu muda umekuwa mkubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naunga mkono hoja kwa asilimia 90, ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mussa Foum Mussa. Sasa nitamwita Mhe. Mwanaidi Kassim aendelee kuchangia hotuba hiyo na baadae Mhe. Suleiman Makame Ali, akifuatiwa na Mhe. Mussa Ali Mussa. Karibu Mhe. Mjumbe.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii kuweza na mimi kuchangia hotuba hii ha Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia mchana huu kuweza kuchangia bajeti hii.

Mhe. Mwenyekiti, pia nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kazi nzuri anazozifanya katika nchi yetu. Pia nimpongeze Mhe. Waziri kwa kutuwasilishia hotuba yake vizuri, tumemsikia na tumemfahamu. Vile vile nimpongeze Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wake wote wa wizara hii kwa mashirikiano mazuri wanayofanya kushirikiana pamoja na kamati.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi ni mjumbe wa kamati, kwa hivyo napokea pongezi kwanza kutoka kwa Mhe. Mwakilishi Nadir Abdul-latif kusema kwamba hotuba ya kamati imeeleza kila kitu na yote ni ya ukweli. Kwa hivyo, nampongeza sana Mhe. Mwakilishi na sisi wajumbe wa kamati tunapokea pongezi hizo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze na Idara ya *UUB*. Kusema kweli Mhe. Mwenyekiti, idara hii inastahili pongezi kubwa, inafanya kazi vizuri kama walivyosema wajumbe wameona bajeti yao haitoshi kutokana na matatizo wanayoyakabili.

Mhe. Mwenyekiti, idara hii ya *UUB* wakati wa kufanyakazi zao wana changamoto nyingi ambazo wanakutana nazo. Mhe. Mwenyekiti, *UUB* wakati wanafanya miundombinu ya barabara kuna matatizo wanayokabiliana nayo ya wizara na wizara, kama Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira na baadhi ya idara nyengine. Kwa hivyo, nawaomba kabla hawajaanza kazi zao basi wakae pamoja wizara pamoja na idara.

Kwa mfano, *UUB* wakitengeneza barabara Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa kupitia *ZAWA* wanakuja kuchimba kupitisha mabomba ya maji, tukizingatia hapo hapo mawasiliano yanakatwa, kwa hivyo pale inakuwa kazi ya mara ya pili. Barabara ikimalizika, barabara inakatwa inataka kupitishwa bomba mawasiliano tayari yameshakatwa, mawasiliano ambayo tayari yalikuwa wamewekwa ina maana hayafanyi tena kazi, ina maana tunarudi tena nyuma tunaanza kazi ile.

Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri suala hili ulisimamie ili tuone tunakwenda mbele sio tunarudi nyuma, tukimaliza barabara tuhakikishe tumemaliza barabara, sio tukimaliza barabara anayepitisha mabomba ya maji anakuja kuchimba, mwenye mawasiliano mawasiliano yamekatwa tunaanza tena, kwa hivyo pale tunakuwa tunapata hasara. Kwa hivyo namuomba hili alisimamie Mhe. Waziri ili tuone kadhia hii tunaondokana nayo.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea Idara hiyo hiyo ya *UUB* kuhusu wafanyakazi wa Kibele. Mhe. Mwenyekiti, wafanyakazi hawa walikuwepo Kibele pamoja na kule Pemba wanafanyakazi kwa mazingira magumu. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri awaangalie kwa makini ili kuona wanapatiwa posho la kazi ngumu. Mhe. Mwenyekiti, wafanyakazi wale wanafanyakazi kusema kweli ya kujitolea, lakini posho la mazingira magumu bado hawajapatiwa. Kwa hivyo kwa hili naomba waangaliwe na Mhe. Waziri ulisimamie katika bajeti hii tuwaone wafanyakazi wale tunawafikiria.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea hapa hapa *UUB* waheshimiwa wengi walisema kwamba barabara zetu hazina viwango. Ni kweli, lakini tukizingatia kama walivyochangia Waheshimiwa Wajumbe, hapa pana tatizo la vifaa, vifaa vyake vilivyopo ni vichakavu. Kwa wataalamu na wafanyakazi kupitia Idara hii ya *UUB*, wafanyakazi wapo na wanafanyakazi vizuri usiku na mchana, lakini vitendea kazi hakuna. Kwa hivyo, tukitaka tusitake lazima barabara zetu zitakuwa hazina viwango. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri na hili basi alisimamie kuona tunapata vifaa ili barabara zetu tuondokane na lile tatizo la kuwa barabara zetu hazina viwango.

Mhe. Mwenyekiti, pia nikiendelea naomba wizara hii basi waiangalie barabara ya Mwanakwerekwe. Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi hiki wakati tunakuja kwenye Baraza eneo lile pale la Mwanakwerekwe, naliacha eneo la Kibonde Mzungu kwa sababu tayari bajeti yake ipo inaendelea, lakini kutoka pale eneo la Mwanakwerekwe na Nyumbambili. Mhe. Mwenyekiti, kipindi hiki cha mvua tulikuwa tunapata shida wafanyakazi tunaokuja kazini asubuhi. Tunatoka majumbani kwetu mapema lakini tukifika pale hatujui tupite wapi kwa msongamano wa magari. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri aangalie tena, akae na wataalamu wake ili waone wanafanya nini pale. Kusema kweli pale palikuwa panatukera, yaani tunagombana kila mmoja anataka

kuwahi kupita ili awahi kufika. Kwa hivyo, wakiangalie tena kipande kile pale kinatuudhi. Tukija Barazani wengine tunachelewa, tunaondoka kwetu saa 12:00 lakini tukifika maeneo ya Nyumba Mbili foleni iko Fuoni, tunasubiri tupite pale Nyumba Mbili kinjia chenyewe kile chembamba, wengine tunapita katikati kwenye majumba tunaanza kukutana. Kwa hivyo, naomba akae na wataalamu wake waone wanafanya nini pale. Kama pale hawajapatengeneza ina maana mwisho lile daraja lililokuwepo pale litakatika sijui tutapita wapi, yaani tutagawana sijui tutapita wapi kusema kweli.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu nije Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Mhe. Mwenyekiti, kusema kweli nimpongeze Mkurugenzi kwa kazi nzuri anazofanya, kusema kweli anafanyakazi vizuri, anakusanya mapato vizuri kupeleka Hazina, lakini pana tatizo. Mhe. Mwenyekiti, baada ya kukusanya pesa kupelekwa Hazina, wakati wao hapa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege wanatatizo la eneo la kufikia wageni yaani banda wageni wakija, yaani tuseme siku ya Jumatano wanakuja watalii wengi. Kusema kweli pale panakuwa na msongamano mkubwa mpaka inafikia watalii wanazimia, kwa hivyo hii sio hali nzuri tunaiomba Wizara ya Fedha kupitia Hazina waangalie basi mapato wakati wanarejesha vizuri na wao wakileta maombi yao wawatizame ili waendeleze uwanja wetu, pale Mhe. Mwenyekiti, ukielezwa unaambiwa jinsi wageni wanavyojaa kuanzia ndani mpaka nje joto limewashika mule ndani wageni wanazimia na sisi hapa tunasema tuko zaidi kiutalii wakati mtalii mwenyewe akija anasimama nje kule hawezi kuingia pale akapata huduma kwa hivyo hili ni tatizo. Tunaomba Wizara ya Fedha kupitia Hazina wakati Mamlaka hii ya Viwanja vya Ndege inakusana mapato yake vizuri basi na wao muwatizame vizuri ili kuendeleza kuona nchi yetu inaingiza mapato.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nakuja hapo hapo kwenye Viwanja vya ndege mimi pia nawapongeza kwa kupata kituo cha Zimamoto na

magari mapya yaliyokuwepo pale, lakini katika kituo kile kilichokuwa kimefunguliwa kuna deni kubwa la umeme kwa hivyo naomba Mhe. Waziri walifuatilie hili suala waone lile deni linamalizika.

Lakini pia nimpongeze Mkurugenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Pemba, kusema kweli pale palikuwa na tatizo la *transformer* sasa hivi tayari imeshapatikana nasema Mkurugenzi hongera sana kwa sababu *transformer* iliyokuwepo pale mwanzo walikuwa wanatumia pamoja na wananchi katika maeneo yaliyozunguka uwanja wa ndege, lakini sasa hivi Uwanja wa Ndege wa Pemba *transformer* tayari imeshapatikana nasema hongera sana Mkurugenzi azidishe jitihada ili uwanja wa ndege ule uweze kuendelea.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea nije Shirika la Bandari hapa nimpongeze sana Mkurugenzi wa Shirika la Bandari na wafanyakai wake wote kwa kufanya kazi zao vizuri, tayari katika sherehe zetu za Mapinduzi tayari tumepata mashine ya kutolea makontena hapa nawapongeza sana lakini pia niwapongeze kwa kupata hatimiliki katika bandari yetu ya Mpigaduri na Mkokotoni, kusema kweli ni hatua nzuri na tuna matumaini ya kupata bandari wakati wowote.

Lakini nikija katika hatimiliki hili naomba Wizara isimamie zaidi hatimiliki ya Malindi ipatikane, hatimiliki ya Bandari ya Wete, Hatimiliki ya Bandari ya Mkoani, sio vizuri kusikia kama Serikali ni moja lakini hati miliki katika maeneo hayo hakuna. Pia katika maeneo ya minara kwa taarifa tulizokuwa tumepewa katika kamati kwamba tayari wamefanya hatua kupata hati miliki kwenye minara, lakini bado kupitia Wizara ya Ardhi hawajawatekelezea kuona minara ile inapata hati miliki kwa sababu minara ile inaingiza sasa bila ya kuwa na hati miliki hapa ni tatizo, kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri ayasimamie haya yote kuona imepatikana hati miliki.

Lakini pia nimuombe Mkurugenzi wa Bandari kuhusu mashine ya kukagua mizigo pamoja na kufanya kazi zake vizuri lakini tunamuomba pale katika bandari ya malindi ipatikane mashine ya kukagua mizigo, kwa hivyo namuomba ajitahidi kwa hatua ya awali alisema tayari mashine hiyo inatafutwa lakini na mimi namuomba ajitahidi zaidi kama alivyokuwa kapata mashine za kushushia makontena kwa hivyo na hii ipatikane.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea niende Idara ya Mawasiliano naomba Idara hii nawataka washirikiane na Mamlaka ya Mawasiliano ya Tanzania TCRA kuhakikisha wanaweka utaratibu wa kupambana na vitendo vya utapeli na udanganyifu unaofanyika kupitia mashirika ya simu za mikono, kusema kweli katika masuala ya mawasiliano hasa kuhusu kupitia simu za mikononi. Mhe. Mwenyekiti, utapeli umezidi kupitia simu za mikononi hasa katika masuala ya Tigo pesa wizi umekuwa mkubwa, mtu anatapeliwa kupitia kwenye simu ukifuatilia hatua ukisema uende Polisi anasema si lake, ukisema uende Mawasiliano wanasema si lao. Sasa sijui wananchi waende wapi au unaambiwa uende bara hili si letu sasa nawaomba basi hapa idara hii iwe na mashirikiano zaidi na Mawasiliano ya Tanzania *TCRA* ili kuona tatizo hili linamalizika.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nikija katika bodi nimpongeze Waziri katika kuwaona hawa watu wa bodi katika kipindi hichi cha bajeti na yeye kawaona lakini namuomba awaone kikweli kweli, kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, bodi inateuliwa Mwenyekiti wake anateuliwa na Rais lakini mpaka bodi inamaliza hawajafanya kazi hata siku moja, ukiuliza sababu gani tatizo hawana bajeti, kwa hivyo hili katika Wizara hii nimeona kwa kipindi hichi wamewaona. Kwa hivyo nawaomba basi washirikiane nao kuona kazi wanafanya haipendezi kuona bodi imeteuliwa imekaa mpaka inamaliza bodi haijafanya kazi halafu Mwenyekiti kachaguliwa na

Rais hii hapa sio nzuri. Kwa hivyo tunaomba wapeane mashirikiano ili bodi nazo zifanye kazi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa vile mimi ni mjumbe wa kamati nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi wachangie hotuba hii ya Mawasiliano lakini mabuti yasiwe makubwa kama mlivyotusifu hapa kamati imesema kweli, kwa hivyo tunakuombeni tupo kikweli zaidi mabuti yawe madogo tufanye kazi tuone ukweli wetu katika kamati hii.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Wanawake wa Mkoa wa Magharibi naunga mkono hoja asilimia kwa mia. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mwanaidi sasa nitamuita Mhe. Suleiman Makame Ali, na Mhe. Mussa Ali Mussa ajitayarishe.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kabla ya kuchangia kwanza nitoe pongezi zangu kwa Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kazi anazozichukua zenye bidii na nzuri za kuridhisha.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, kama Mhe. Waziri atakumbuka bajeti yake ya mwaka 2016/2017 nilimwambia kwamba watengenezee wananchi barabara zenye viwango mtu akitamani kulala barabarani basi alale, huenda kwa Mungu hakuna kubwa kwamba Mwenyezi Mungu si athumani huenda 2020 pengine ukapata nafasi ya Urais kwa sababu utendaji utakuwa unaonekana, kama Mhe. Magufuli kule bara . Kwa hivyo namuomba tena na mara hii Mhe. Balozi aendelee hivyo hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza niende kwenye barabara ya Madenjani/Mzambarauni huku tumeona kwamba barabara ya

Madenjani/Mzambarauni inahitaji tena shilingi bilioni mbili, kwa hivyo mimi nataka kumuuliza Mhe. Waziri hivi bilioni mbili za vipi na barabara ile imeshamalizika na *program* yao walioiombea pesa walitwambia hapa kwamba kwa mwaka wa fedha 2016/2017 wamepata asilimia 78%. Sasa asilimia 78 kwenye asilimia 100 nadhani zitabaki kama asilimia 22 kutimia asilimia mia moja, sasa leo bilioni mbili wakati kwa mie Ndagoni hakwendeki na roho ya Pemba iko Ndagoni kila siku nazungumza suala hilo hapa nitahitaji majibu. Mhe. Waziri akija anipe majibu vizuri kwamba bilioni mbili hizi ni za nini na barabara ile imeshamalizika na asilimia 78 ya pesa walizoomba wameshaipata, kwa hivyo nataka majibu hapa Mhe. Waziri angalia vizuri uje unipe majibu kwenye hili.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo niende kwenye barabara ya Wete/Chake ambayo imepita jimboni kwangu Ziwani, barabara hii walisema hapa kwa mwaka wa fedha 2016/2017 mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya Shilingi bilioni 6,380,000,000 na hadi kufikia Machi, 2017 hakuna fedha iliyotumika. Nataka nimuulize tena Mhe. Waziri maana ukisema kwamba hakuna fedha iliyotumika ni kwamba utakuwa unayo kidogo au utakuwa unayo hiyo pesa hujatumia. Kwa hivyo mimi nataka nijue hii pesa vipi ipo haijatumika tu au hawakupata, kwa sababu hapa hakutueleza ametwambia haijatumika kwa hivyo ukisema kamba haijatumika ni kwamba ipo. Kwa hivyo nataka kujua hapa. Lakini pia vile vile nimuombe Mhe. Waziri kwamba kutegeneza barabara ni kazi kubwa sana kuna mambo mengi utakumbana nayo kuna vilimo huko vya wananchi, kuna nyumba za wananchi, lakini pia vile vile nimuomba Mhe. Waziri aliangalie sana wakati wa kutengeneza barabara ile basi wale watu walipwe kabla ili mwenye kibanda chake cha mgongo aondoke njiani akatafute pahali akae, isijekuwa tena barabara tayari inataka kutengenezwa unamvunjia mananchi nyumba yake pakukaa hana pesa uliyompa haitoshi, ikawa mtihani Serikali kuvutana. Kwa hivyo namuomba sana Mhe. Waziri kwamba wananchi wote watakaopitiwa na

barabara ile basi kwa kila mwananchi alipwe pesa yake mapema, tena akishaila akitafutia changu atajua mwenyewe vya kufanya. Lakini ni kwamba yoyote atakayepewa pesa yake ajue tayari napewa pesa yangu hii nakwenda kuhamia wapi namuomba sana Mhe. Waziri achukue hatua hiyo wakati ukifika.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye Idara ya Usafiri na leseni nadhani sote ni mashahidi na wazungu waliotengeneza zile gari pamoja na vespa na vyombo vyengine vya moto wakatia *sight mirror* si wapumbavu wale. Leo Mhe. Mwenyekiti, ukipita humo mabarabarani unawakuta vijana na hata waliokuwa si vijana mpaka wazee wanaendesha vyombo hata *sight mirror* havina yaani gari ipo hapa unafunga *break* wanasababisha ajali wale. Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi naiomba sana Wizara walisimamie hili kuhakikisha kwamba wale waliokuwa hawataki kuzifuata zile shria na taratibu ikiwa mtu anaona tabu kutia *sight mirror* yake kwenye pikipiki au vespa basi anunue kwa lazima ikamatwe vespa yake apigwe faini elfu 50 anunue pale afunguwe. Kwa sababu atakuwa hawezi kufunga ati. Kwa hivyo namuomba sana Mhe. Waziri na hili walisimamie kwa sababu hawa wanasababisha ajali barabarani tena za kizembe kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye utunzaji wa matengenezo ya barabara. Mhe. Mwenyekiti, kila siku tukisema kwamba tunatunza barabara ni kweli lakini sasa ni kitu gani kinachosababisha kwamba barabara hizi zinatengenezwa leo kesho zina mashimo kama nyumba ya sungura, kila siku itakuwa tunatengeneza barabara hizo hizo hivi sisi hapa Zanzibar tuna kilomita ngapi za barabara Mhe. Mwenyekiti, hata kwamba barabara hizi zishindwe kumalizwa kila siku utengeneze barabara hiyo hiyo, nasema kwamba barabara zinazotengenezwa hazina viwango, viwango ni vidogo. Leo kama barabara ya Kiwani ile imefikwa na maafa sawa lakini hata mtaro ule wa kupitia maji barabara ile ilikuwa haina, sasa mvua iliyonyesha itafanya nini itakatika tu. Kwa hivyo namuomba Mhe. Mwenyekiti, kwamba

masuala haya ya kutunza ni mazuri sana lakini sasa kile kitu ukitunze mwanzo sio kwamba uje ukitunze badala ya kuharibika leo unatengeneza barabara ikinyesha mvua inaharibika. Mhe. Mohammed tumembadilisha jina hapa tunamuita mkuu wa mashimo siku hizi nadhani simuoni Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia Wizara yake hii kwamba wahakikishe wanapowaita wale wakandarasi wa kutengeneza barabara na wale ma-*engineer* basi wahakikishe barabara wanazozitengeneza zina viwango, leo kule Bara kuna barabara inatoka masafa si chini ya kilomita mia mbili huikuti barabara ile kuchimbuka wala kufanya chochote. Lakini sisi hapa Zanzibar barabara kilomita mbili au tatu kuna tatizo gani hata kwamba barabara hii inatengenezwa leo kesho inachimbuka sisi si wa kuwa tena hapa tunazungumzia suala la barabara Mhe. Mwenyekiti, si wa kuzungumzia suala la barabara kabisa lakini tatizo sijui ni nini. Labda Mhe. Waziri atakuja kuniambia lililokuweko huko.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nizungumzie suala la Bandari, jana hapa nilizungumza kuhusu suala la Bandari kwamba wafanyabiashara kule Pemba wanapata tabu, lakini kama Mhe. Mwenyekiti, utakumbuka tulipokwenda kusali iddi pale Mkoani kuna sehemu imezungushwa uzio, nikauliza hii sehemu ni ya vipi nikaambiwa ni sehemu ya makontena. Kwa hivyo nataka kumuuliza Mhe. Waziri ile sehemu ni ya makontena kweli na kama ni ya makontena kwa nini mpaka leo haijafanya kazi na kule wafanya biashara wanahangaika, jana Mhe. Waziri wa Biashara alinijibu akanambia majibu haya atakuja kupa Mhe. Waziri yeye alinijibu kidogo lakini na Mhe. Waziri leo atanipa majibu. Kwa hivyo namuomba tena Mhe. Waziri aniambie kwenye suala hili kwa nini eneo lile pale halijaanza kutumika kwa kuweka makontena ili wafanya biashara walioko Pemba na wao wakajisikia, hata ile *crane* ya kubebea mizigo ipo sasa lakini kitu gani kinachosumbua mpaka leo hii.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye suala la barabara ya Ndagoni katika jimbo langu nina barabara Michungwani, Birikau, Ndagoni lakini hizi zote ziko kwenye Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara maalum za SMZ nakubali hilo, lakini juzi hapa Mhe. Waziri huyu nilimuuliza akanambia kwamba Mhe. Suleiman si tatizo kutengeneza barabara ya Ndagoni lakini tatizo ni pesa, sasa leo kama pesa hana barabara iko kwake itatengenezwa lini.

Kwa hivyo mimi naiomba Wizara hii ya Mawasiliano kuwafikiria wananchi wa Ndagoni lakini kuwafikiria wananchi wa Pemba kwa sababu Ndagoni ndiko kwenye roho ya Pemba kila siku nalizungumza suala hili, leo imekuwa Ndagoni sijui wamekosa nin. Umeme upo umetoka kule maana ni hazina kusema ukweli lakini barabara ni mtihani haifikiki wale wanaofanya kazi kwenda kulinda umeme kule wale askari wetu wanapata tabu wananchi wanateseka, ilikuwa wanananchi kule wanachukuliwa kinamama kupitia kwenye vidau, wanachukuliwa kwenye magunia kwenda hospitali Chake Chake na pale Wesha kwenye kituo cha afya wanapata tabu mpaka sasa hivi imebidi tena lirudie suala lile lile.

Kwa hivyo namuomba sana Mhe. Waziri hili aliangalie hata kama hii barabara iko kwenye Tawala za Mikoa lakini aangalie kuhakikisha kwamba Ndagoni kuna roho ya Pemba, kwa sababu ikianguka nguzo ya umeme kule Pemba itakuwa totoro. Mhe. Mmanga nina imani hataweza kuona Chake Chake na itakuwa haing'ari kwa sababu Ndagoni ndio kwenye umeme Mhe. Mwenyekiti. Kwa hivyo namuomba sana Mhe. Waziri ahakikishe kwenye suala hili la barabara hii ya Ndagoni kwa sababu haiko kwenye ilani lakini aiangalie kwa sababu kule ndiko kwenye roho ya Pemba angalau na wale wananchi wa Ndagoni wapate kujua kwa sababu tangu ilipoumbwa dunia Mheshimiwa nathubutu kusema humu na siku zote nazungumza suala hilo hilo tangu kuumbwa Dunia, lakini sasa nasemea kwamba kule kuna roho ya Pemba na likija suala la umeme nitaizungumzia suala hilo hilo.

Kwa hivyo naiomba Wizara ya Mawasiliano, Tawala za Mikoa pamoja na Wizara ya Nishati na Mazingira wahakikishe kwamba barabara ile ya Ndagoni wameitengeneza kwa kiwango cha lami.

Mhe. Mwenyekiti, badala ya hayo naunga mkono asilimia thamanini, namsubiri Mhe. Waziri kwa asilimia ishirini nitamuachia akija akinijibu yale masuala niliyomuuliza likiwemo hususan suala la barabara ya Madenjani/Mzambarauni iliyotengewa tena Shs. bilioni 2 ambayo kwamba imeshamalizika barabara ile. Lakini pia na suala la Ndagoni kwa sababu ndio kwenye roho ya Pemba na mengineyo niliyomuuliza Mhe. Waziri naomba majibu.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono kwa asilimia thamanini. (Makofi)

Mhe. Mwenyekiti, ahsante Mhe. Suleiman sasa namuita Mhe. Mussa Ali Mussa na baadae Mhe. Nassor ajitayarishe kwa dakika tano.

Mhe. Mussa Ali Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na mimi kunipa nafasi hii kuchangia Hotuba hii ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. Lakini nimeona hapa hii Wizara imezungumzia kitita cha shs. 358,000,000/= ambazo wameshazilipa fidia kwa wananchi sasa hawakueleza hapa ni wananchi wangapi na ni wa jimbo lipi. Maana kama ni wananchi wa Jimbo la Ole basi hizi pesa itabidi waniletee kwa maandishi ndio nikubaliane na bajeti yake kwa sababu wananchi wangu wa Jimbo la Ole nyumba ambazo zimelipwa hazifiki 24 na kama hilo halitoshi ni watu 2 tu ambao wameingia milango ya shilingi milioni 28 waliobakia wote wameanza milioni 3,200,000/= milioni 4,600,000/= na milioni 5,000,000/= Sasa hichi kitita chote hichi cha pesa amelipwa nani.

Sasa ninachotaka kusema kwamba fidia inavyokuja fidia ni lazima unayemlipa fidia ni kama unaemuuzia mukubaliane kati ya muuzaji na mnunuzi, walikuwa hapa watu wa miundo mbinu wawaite wananchi wa Ole pamoja na sheha wao jamani tunataka kwenda kuvunja majumba kule Ole, tunataka kwenda kun'goa migomba Ole, tunataka kwenda kun'goa miembe Ole, tunataka kwenda kungowa mihogo Ole kwa ajili ya kupitisha barabara.

Sasa wewe kakae kwenye nyumba yako unakwenda pale na Kamati yako bwana nyumba yako ni milioni 10,000,000 aa milioni10,000,000 bwana mimi msinivunjie sipati nyumba basi tutakupa basi tutakupa 8,000,000 ni lazima mukubaliane mupatane, lakini sio unakaa ofisini huko na kiokozi chako na feni lako liko nyuma na kitu cha kuzunguka unamwita mwananchi, unamwambia tia saini nyumba yako kesho uivunje milioni zako 4,000,000 hizi hapa. Milioni 4,000,000 unapata kiwanja, milioni 4,000,000 unapata kiwanja maana nyumba basi mtafutie kiwanja kwanza. Halafu jengine baya zaidi kile kijiji cha Vitongoji, kuna eneo linaitwa Vumba hili eneo lina mto mkubwa sana ambao huo mto umo katikati ya mji watu wa miundo mbinu dogo lote walilolikwangukura kuanzia Kianga, Ole, Dodeani, wamekwenda kuufukia ule mto kwa sababu nani kuna muarabu pale anataka kujenga kawapa pesa kidogo wamekwenda kuufukia ule mto. *(Makofi)*

Sasa mvua zimekuja kubwa, mvua hazina salama pamoja na kuwa ni barka lakini haina salama, imekuja mvua mto ule uchafukiwa na wenzetu wa mawasiliano, washachukua pesa washaondoka maji sasa yamekuja majumbani. Wananchi twende kwa Mwakilishi na kuja kufatwa wewe ulitwambia nini sasa jamaa zao wanatuvunjia, nawapigia simu njooni bwana hawaji, tunakuja Muheshimiwa lakini hawaji. Kesi hii imetokana na barabara yao vile vile, wamejenga barabara yao mkate wa gae ule hawakuitia msingi matokeo yenyewe maji yamekwenda ndani ya majumba, wananchi wanapiga simu njooni twafa hawaji, wamenitia aibu

mara wananchi siku hizi hawaogopi alipokwenda Balozi kukagua maafa wamemueleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa sisi tusingepata maafa wizara yako ndio iliyotutia maafa maana tumewapigia siku tunazama njooni mpige misingi hawakuja, Balozi kabaki anasikitika sasa ndipo niliposema Mtume aliwambia Masahaba darasani (S.A.W) ukiwa huna la kusema nyamaza, utakapo nyamaza utapata thawabu kuliko kusema neno ambalo hulijui kwa nini kama huna la kusema hunyamazi, unakwenda kuwasifu watu wa miundombinu Pemba, ule ukumbi wa ZSSF, Mwenyekiti wao yuko pale siku ya mvua kubwa ile kawambia hili daraja ondosheni mlango kwenye daraja maji yapite yende pwani anawambia nipo, yupo na yeye pale anisute wakakataa matokeo yenyewe maji yamekwenda pale yamefungiwa yamepanda juu ya daraja yaliyobakia yamerudi hoteli ya Ukumbi wa ZSSF. *(Makofi)*

Wamemuingizia Muekezaji wetu hasara isiyojulikana, wanakuja saa tatu asubuhi wanasifiwa wao, baada ya kuwasifu Kikosi cha Zima Moto na Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba na Mkuu wa Wilaya na Muwakilishi jembe anakwenda kusifiwa, jamani tufuateni Sheria, kama mtu hana la kusema anyamaze. Ndivyo inavyosema dini yetu ya Kiislamu sasa ninacho taka kusema katika Bajeti hii sijakuta kuwa wananchi wa Ole ambao nyumba zao zimewekwa X tokea 2013 watamaliziwa lini kulipwa, hao wachaopoa vichocho basi, hawa ambao hawajapewa kabisa na nyumba zao zimeharibiwa watalipwa lini mbona humu haielezwi au wale ndio basi tena. Maana yake unafanya jambo, mimi wameshanambia bwana kama hatukukusikia unazitetea haki zetu basi huku usirudi. Sasa mimi Mhe. Mwenyekiti, mimi ukanibakishe Unguja sijui kusema kiunguja hebu nambie nataka kukaa vipi Unguja na nasijui kusema Kiunguja mie nasema Kipemba na kule sithubutu kurudi, kwa mikasa walionifanyia watu wa Mawasiliano na Miundo mbinu kukata barabara bwana

maji yanaingia katika majumba ya watu Ole haingii maji wamesababisha wao kuingia maji. *(Makofi)*

Namshukuru sana Katibu wao yule Mustafa Aboud kaja nyumbani kwangu namsifu sana, na kweli ni kiongozi nakubali ni kiongozi maana kaja tumefuatana mimi na yeye tumekwenda kwa wananchi, kaona wananchi walivyoharibikiwa akasikitika. Kisha akaniahidi mbele yao kwamba hawa Mheshimiwa tutawalipa, lakini hawajalipwa na bajeti humu haikutiwa na fungu lao huku halimo sasa ninachotaka kukwambia kwamba hali hii au bajeti hii kwa sababu mie hainitaki nirudi Pemba na mimi sitakubali ipite. Ama akija Waziri aje anambie Mhe. wa Jimbo wa Ole watu wako ambao nyumba zao zimewekwa X toka 2013 na migomba yao imen'golewa na mihogo yao na ile miti ambayo usiku inatuburudisha miasumini nao ile ni mali, nayo hiyo nitailipa akija kunithibitishia hilo ndio mimi nitakubaliana naye, lakini kama hilo halipo na mimi nitapigiwa kura leo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine nataka nimkumbushe Waziri unapokata tiket ya ndege kusafiri, tiket ya ndege unaposafiri kutoka Unguja kwenda Pemba ukitoka Pemba kuja Unguja au kutoka Unguja kwenda Dar es Salaam popote mpaka Ulaya ile tiketi imeshalipiwa kila kitu, wewe unachotakiwa pale ni kwenda na tiketi yako ukakaa juu ya kiti ukangojea *cheking* ukapanda ndege ukenda zako. Litakalo kutokezea pale lolote unatakia ufanyiwe bure, leo unashangaa unaingia maeneo ya *Airport* unataka kujisaidia unaambia utowe shilingi mia tano, hapa panapouzwa tiketi ukiingia mkono wa kushoto pana choo ya kulipia si aibu ile. *(Makofi)*

Airport, choo cha kulipia kasema sheria gani tiketi yako ina kila kitu kilicholipiwa wewe unakwenda kukaa pale mgeni atowe dollar moja mwenyeji atoe shilingi mia tano, kuna mambo mengine ni aibu kuyafanya. Mhe. Waziri utakapokuja uje na jawabu kamili vyenginevyo haya utaona kitakachoendelea, na

bahati nzuri mawaziri wote ni marafiki zangu lakini hili sitalikubali, nitalisemea. Mwanzo naingia katika Baraza hili nilisema kwamba wizara hii ina watu wa tarehe 33 ndio kikwazo cha hii wizara. Sasa wewe mtu wa tarehe 33 nani kakwambia kuna tarehe 33, sasa wale watu wa tarehe 33 ndo wanaomuangusha Waziri pamoja na Katibu Mkuu. *(Makofi)*

Nataka wale awatambuwe awaorodheshe tukifika Pemba kama yeye hawajui akija mimi nitamwambia huyu wa tarehe 33 na huyu wa tarehe 33 kwa sababu mimi nakaa Pemba kule, nasitokubali hata siku moja, sitokubali hata siku moja mwananchi wa jimbo langu avunjiwe nyumba yake, nimewatetea watu wa Mwera hapa haya je watu wa Jimbo la Ole kwa sababu kuna mambo ukiyafanya bwana kesho utafika mahali utaulizwa. Hapa tunapita tu utafika mahali utaulizwa unamvunjia wananchi nyumba yake unamwambia ni ya udongo wewe ulitoka ya tufali, kama si Mapinduzi ya 1964 hapa, pangekuwa na nyumba ya tofali, 1964 baada ya Utawala wa Karume ndio hapa imepatikana nyumba ya tofali nyumba zote zilikuwa za matope. Sasa unamvunjia nyumba yake mtu unampa shilingi milioni 4,000,500 unamwambia nyumba ilikuwa ya tofali chukua mabati yako ukajenge wapi, unafanya nini bwana 2020 ni kesho Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, 2020 ni kesho kuna watu wanatuharibia tusifichane tukija hapa tukipongezana tu, umefika wakati wa kufanya kazi kwa wenzetu jirani zetu wanafanya kazi na sisi tufanye kazi sasa kama mtu hawezi kufanya kazi atupishe. Kama basi letu linakwenda mbio teremka umpe nafasi mtu apande, ukenda maofisini watu wana kiburi, unamfanyia kiburi nani, nani uliyemuumba mbona siku ya mshahara na siku Dkt. Ali Mohamed Shein alipopandisha mshahara umecheka unakuja kuchukia wakati wa kazi, fanyeji kazi Mhe. Waziri nakwambia watu wako wambie wafanye kazi kama hawataki kazi usiwape maandazi, utampaje mtu kazi wakati hataki maandazi, unampaje maandazi wakati kazi. *(Makofi)*

Sasa nadhani Mhe. Mwenyekiti, nataka nirudi kidogo kwenye meli ya Mapinduzi. Meli ya Mapinduzi II kwa sababu sisi hatujawa na kingi tunakidogo tena kimoja kwa nini tukikodishe hicho kimoja tunataka Meli ya Mapinduzi II kwanza ikidhi haja za Wazanzibari kutoka Unguja kwenda Pemba kutoka Pemba kwenda Unguja, mpaka tutakapopata meli yengine ndo hii tutaiondosha. Kwa sababu sasa hivi kuna ushindani wa kibiashara, na sisi hatuko kwenye biashara tuko kwenye juhudi na jitihada za wananchi wetu.

Wananchi wetu wanadhikika jana imeingia Meli saa 3:00 za usiku hebu angalia watu wameingia saa ngapi Pemba, ingekuwepo Meli yetu ya Mapinduzi saa 6:00 watu wameshateremka, lakini jana wanaingia watu na watoto wachanga 3:00 usiku nipo bandarini sijasali tarawehe nipo bandarini nawangojea ndugu zangu tu wanaingia saa 3.00 mambo yanaliza kabisa. Meli imekuja juzi mpya, haidhuru ni mashine, mashine ni roho ya binaadamu lakini itakapokuja iwe na matumizi ya Unguja na Pemba, Pemba na Unguja mpaka tutakapopata nyengine. Hapo wanababaisha tu, hatujui kinachobabaishwa ni kipi. Meli ikenda ina watu lete likirudi lina watu tele njoo utake hesabu utizame bahati itakayokuangukia utaonekana sijui mtu wa maajabu wewe unataka hesabu itokee wapi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, leo ni mwezi Mtukufu wa Ramadhani na leo ni mwezi tano na mwezi wa Ramadhani ni mwezi wa kuzungumza mengi unaweza ukaja ukateleza, ukaja ukafungua na bahati nzuri Wawakilishi wananitegea niseme jambo wanibandike jina la tatu, maana mara ile walinita Mheshimiwa X, juzi wakanita ukuta, sijui leo watanita vipi. Sasa nawaacha kwanza.

Baada ya hayo naunga mkono hoja kwa sababu hii Wizara ina rafiki zangu zitaki kuwadanganya. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Mussa amechangamsha kidogo sasa naomba nimwite Mhe. Nassor Salim Ali (Jazira) dakika tano baadae atafuatia Mhe. Mtumwa Peya Yussuf dakika tano na Mhe. Maryam Thani ajitajarishe kwa dakika tano.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

Mheshimiwa kabla sijatoa mchango wako mdogo lakini na mimi nichukue fursa hii kumpongeza sana Mjumbe aliyepita Mhe. Mussa Ali Mussa Mwakilishi wa Jimbo la Ole kwa mchango wake mzuri na kuonesha kwamba ana uzalendo na upendo wa nchi yake na kutaka maendeleo ya nchi yetu, haya yote ni kutokana na mapenzi yake na ukereketwa wake wa Chama cha Mapinduzi hongera sana Mheshimiwa. *(Makofi)*

Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, mimi ni Katibu Msaidizi wa Mnadhim nichukue fursa hii kwa niaba ya Mnadhim kumpongeza sana na haya yote ni ujumbe huu ameutoa ni wa kwetu sote. Kwa sababu 2020 kweli si mbali na mimi ninaimani Mhe. Mussa 2020 atakuwa tena Mwakilishi wa Jimbo la Ole na sisi sote tuliomo humu ndani kwa kazi kubwa tunayoifanya ya kuleta maendeleo ya nchi yetu kwa uongozi mzuri wa Dkt. Ali Mohamed Shein na Mawaziri wetu na Watendaji wetu na kasi kubwa ambayo tunaisukuma sisi Serikali nina imani kwamba 2020 sote tutarudi tena katika mtindo huu tumuombe Mwenyezi Mungu atujaalie uhai, na uzima na kuleta maendeleo kwa faida ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa baada ya kusema hayo au kutanguliza hayo niseme tu kwamba waswahili wanasema “mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni” nimpongeze Mhe. Waziri sana pamoja na Naibu Waziri na Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii

kwa kazi kubwa wanayoifanya. Mheshimiwa hivi karibuni Zanzibar na Tanzania kwa ujumla na Ulimwenguni, kulitokea mvua kubwa ambayo imesababisha maafa barabara zetu kuharibika madaraja yetu kuharibika lakini kwa kazi nzuri aliyoifanya Mhe. Waziri ya wasaidizi wake na watendaji wa Wizara hii wameweza kurejesha hali nzuri ya barabara zetu kule Pemba. Barabara zinapitika sasa hivi na nina imani kwamba kwa kasi wanayokwenda nayo baada ya muda mrefu barabara zetu zitakuwa nzuri. *(Makofi)*

Lakini Mheshimiwa mbali na barabara za Pemba lakini hata barabara zetu za Unguja kuna nyingi ambazo zimechimbuka, na kufanya maafa katika barabara zetu zikiwemo pia katika maeneo ya mjini katika barabara ya makontena Michenzani pale, Muembe Kisonge, Muembeladu na maeneo mengine, kwa hivyo niombe Wizara kuhakikisha kwamba katika maeneo yake basi wanafanya matengenezo ili wananchi wasipate tabu katika barabara zetu.

Mheshimiwa nije katika programu hii ndogo ya utunzaji na utengenezaji wa barabara ambayo yote niliyoyasema lakini vile vile, kuna maeneo mengine ambayo yamepata athari ni kutokana mvua hizi, kuna barabara hii ambayo ya Mwanakwerekwe Mheshimiwa niombe sana Wizara hii kuhakikisha tunafanya mipango mbadala ili kuondokana na kadhia ile ambayo ipo Mwanakwerekwe. Mheshimiwa wananchi wetu wanapata tabu kutokana na barabara ile na hasa ukizingatia katika Mwezi Mtukufu huu wa Ramadhani, wananchi wetu wanapata tabu wanazunguka hata kupitia Mwera na katika barabara nyengine kwa hivyo niombe Wizara hii kuhakikisha kwamba wanakuja na miundo mbinu mpya, ili kuhakikisha kwamba barabara ile inafanyiwa miundo mbinu ili kuweza kupitikana kwa vizuri.

Lakini vile vile, Mheshimiwa Mwakilishi wa Jimbo la Muyuni Mhe. Jaku alizungumzia suala lile la barabara kutoka Fuoni kuja

zako Fumba – Kisauni Mhe. barabara ile ambayo inapita Kwarara, mimi nadhani ipo haja ya kuhakikisha kwamba Wizara yetu na serikali yetu, inaangalia kufanya kazi kila aina ili barabara ile iweze kujengwa ili iwe mbadala. Kwa sababu kama ingelikuwa barabara ile inapitika basi hayo matatizo yaliyokuwa yanatokea kwa wananchi wetu yasingetokea. Ni wajibu wetu kuhakikisha kuisemea serikali na kuikusha serikali ili kujenga miundombinu mizuri ili wananchi wetu waondokane na shida ambazo wanazipata.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutoka hapo nije kwenye programu ndogo ya Usimamizi wa Usafirishaji. Nichukue fursa hii kumpongeza sana Mkurugenzi wa Shirika la Bandari, anafanya kazi vizuri na sote tunaiona tukiwa kama Wajumbe wa Kamati, tumekuwa tukifatilia kipembe hadi kipembe, kona hadi kona. Maendeleo ambayo yanapatikana ni mazuri yote haya ni kutokana na juhudi za uongozi mzuri pamoja na wetendaji wote wa Wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, mbali na sifa hizo nizungumzie suala zima la mashine za pale bandarini ambalo limezungumzwa na Wajumbe wenzangu wengine. Nimewahi kusafiri kutoka Dar-es-salaam kuja pale Bandarini ambapo bahati nzuri siku hiyo tulisafiri pamoja na wageni wetu, tulikuwa tunatoka katika safari ya Sherehe za Jamhuri ya Muungao wa Tanzania. Tulipofika Bandarini pale kulikuwa na wageni walipata tabu na walisema maneno mengi ambayo kwa kweli tukiwa kama viongozi lazima tuyaangalie na kuweza kuyafanyia kazi. Ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba mashine inapatikana na haraka ili kuondoa kadhia ile ambayo wananchi wetu na wageni wetu wanaokuja katika nchi yetu wanaipata.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nizungumzie Shirika la Meli. Shirika la Meli limefanya kazi nzuri. Nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Rais wetu kwa kuweza kufanya kila njia na mipango

kuweza kununua meli yetu ile ya Mapinduzi II. Mbali na tatizo ambalo imelikumba meli yetu hii, lakini serikali yetu inahitajika kupewa pongezi. Niipongeze sana serikali yetu kwa ununuzi wa meli ile. Nina imani kwamba uongozi walionao chini ya Dkt. Ali Karume, Mhe. Jaku Hashim alisema ana matumaini nae huko mbele. Nina matumaini nae hivi sasa ili kuweza kubadilisha Wizara hii na kuhakikisha kwamba tunakwenda na wakati kuondoa matatizo yote ambayo yanaikabili Wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, nimuombe sana Mhe. Waziri, kwamba meli ile ambayo ni tegemeo la Wazanzibari, ndugu zetu, jamaa zetu wa Pemba wanaitumia sana meli ile katika shughuli zao za kibiashara, kusafiri kutoka Pemba kuja Unguja kutoka Unguja kwenda Dar-es-Salam. Mimi nadhani ipo haja ya kuhakikisha kwamba meli ile madhali tupo katika makataba bado kuhakikisha kwamba tunakwenda na wakati ili kuhakikisha yale matatizo madogo madogo yaondokane. Ni vyema Baraza lako Tukufu kujua tatizo gani ambalo limeikumba meli ile katika tatizo ambalo limetokea hivi karibuni.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa dakika zako zimeshazidi, nimekupa dakika tano umeshachukua saba, nimekuongezea dakika mbili. Kwa hivyo naomba umalizie.

Mhe. Nassir Salim Ali: Namalizia Mheshimiwa kwa haraka haraka. Nimalizie katika Programu Ndogo ya Huduma za Usafirishaji kuhusiana na suala zima pale Bandarini katika uuzaji wa tiketi. Kumekuwa na changamoto kubwa kwa wale wanaununua tiketi pale Bandarini tatizo hili limekuwa ni sugu, sisi sote ni mashuhuda, Kamati yetu imeshawahi kushuhudia tatizo hili. Kwa hivyo nimuombe Mkurugenzi Mkuu wa Shirika hili na Katibu Mkuu ili kufanya kazi ili kuendana na wakati kutanua mashine ambayo ya kuuza zile tiketi, sio tiketi za kuuza mikononi ili wananchi wetu waondokane na kutapeliwa na matapeli.

Baada ya kusema hayo Mheshimiwa nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote. Nawaomba Waheshimiwa wenzangu Wawakilishi wenzangu tuiyunge mkono bajeti hii ili Waziri aende wakafanye kazi, tutakapokuja mwaka 2018/19 basi tumuulize amefika wapi ili kuleta maendelea kwa taifa letu. Naunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mwenyekiti: Naomba nimwite Mhe. Mtumwa Peya kwa dakika tano kama alivyoomba na baadaye atafuatia Mhe. Mariyam Thani kwa dakika tano.

Mhe. Mtumwa Peya Yussuf: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi hii kuweza kuchangia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji na mimi nitaongea kwa ufupi kwa sababu wenzangu wengi wameshayaongea mengi. Moja kwa moja nimpongeze sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kazi zao nzuri wanazofanya lakini pia kwa mashirikiano yao ambayo wanayotuonyesha.

Mimi nakuja moja kwa moja kwenye barabara ya Bububu Mkokotoni wenzangu wameshaizungumzia barabara hii lakini mimi nakuja kwenye madaraja kuanzia Kazole, Kitope na Mtomchanga. Kwa kweli yale madaraja sasa hivi yana hatari sana, kwani yamechimbika vibaya sana na yapo hatarini. Pale linaweza kutokezea tatizo lolote na wakati wowote. Nimuombe sana Mhe. Waziri, lile eneo la pale kwenye madaraja yale matatu kuna mashimo ambayo yamechimbika. Namuomba Mhe. Waziri kwa hisani zenu tukayazibe pale ile ni hatari kubwa, linaweza kutokezea tofauti na ambavyo tunavyotegemea wakati bado ile barabara haijawa tayari kujengwa.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nakuja katika suala hilo hilo la barabara, kutoka Bumbwini kwenda Kiongwe kulifanyika ujenzi

wa barabara na wananchi wengi walikatiwa vipando vyao. Wananchi wale mpaka leo bado hawajapatiwa malipo yao baada ya kukatwa vipando vile. Nimuombe Mhe. Waziri atakapokuja anambie ni lini wananchi wale watalipwa fidia kwa ajili ya vipando vyao. Lakini pia nimwambia hapo hapo kwamba barabara ilijengwa kwa njia ya kifusi na tayari imeshachimbika sana. Aje anambia tu Mhe. Waziri ni lini barabara ile itajengwa kwa kiwango cha lami.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ni kuhusiana na hii mvua ya Masika iliyonyesha kipindi hichi. Mheshimiwa kutoka Bumbwini kwenda Pangatupu ile ni njia kubwa ambayo wanatumia wananchi kutoka Bumbwini, Pangatupu, Mahonda na hali yake sasa hivi ni mbaya sana. Ukiangalia sasa hivi ile njia haiwezi kupitika, wanafunzi kutoka Pangatupu kwenda Misufini wanashindwa kwenda Skuli. Pia wananchi huduma za afya wanazifuata Misufini, imekuwa ni usumbufu mkubwa kwa wananchi wale kufanya huduma za afya kule misufini.

Nimuombe sana Mhe. Waziri afanye ziara ya makusudi twende sote Pandatupu halafu tuone njia gani za kuweza kuwasaidia wanchi wale waondokane na tatizo lile lilokuwepo kule Pangatupu. Nakuomba sana Mhe. Waziri utakapokuja unambie ni lini tutoke hata ukisema twende leo mimi niko tayari kwa adha kubwa iliyopo Pangatupu, wananchi wale nawaonea huruma kwa kazi iliyokuwepo hawafiki popote na hawafanyi kazi zao zozote kwa njia ile ya Pangatupu.

Mimi nilikuwa sina mengi sana ya kuchangia kwa sababu mengi yameshazungumzwa lakini yangu mimi yalikuwa ni hayo machache na naunga mkono hoja lakini pia Mhe. Waziri ukija naomba sana haya niliyoyazungumza unipe majibu na unambie lini twende Pangatupu. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante naomba nimwite Mhe. Mariyam Thani dakika tano.

Mhe. Mariyam Thani Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa fursa hii ili kuchangia machache ambayo yaliyomo katika bajeti hii. Mimi moja kwa moja nizungumzie suala la barabara ambalo ni kilio cha wengi katika nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, katika mvua hizi zilizonyesha barabara ya Wete/Gando ilipata athari kubwa sana tena barabara hii iliathirika sana, najua kwamba ni kudra ya Mwenyezi Mungu sio mategemeo yetu.

Mhe. Mwenyekiti, katika utengenezaji wa barabara Wizara ya Mawasiliano ina *guarantee* ya miaka mingapi. Juzi Mhe. Waziri alijibu kwamba *guarantee* yao ni mwaka mmoja. Mimi nasema mwaka mmoja ni kidogo sana, kudra ya Mwenyezi Mungu hatuwezi kuijua kama Wizara wangejua kwamba *guarantee* hii ya mwaka mmoja tufanye angalau ya miaka miwili kabla ya mvua nyingi zile hazijanyesha kujua hali gani ya mvua itakavyonyesha barabara itaathirika vipi.

Vile vile niseme kwamba Kampuni hii ambayo imetengeneza barabara hii ya Wete/Gando kwa kweli ni mtihani kwa sababu barabara yangu ya Gando ilipokwishakutengenezwa tuliona kwamba ni nzuri lakini athari iliyojitokeza ni mbaya sana. Mhe. Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alivyokuwa Waziri wa Mawasiliano barabara ikishakutengenezwa lazima aikaguwe, aipime, aiangalie ina kiwango gani ndiyo awaruhusu wakandarasi kwamba barabara ile kuitumia. Lakini sisi hapa Zanzibar hatufanyi hivi na ndio maana barabara zetu za Zanzibar zikawa zinaharibika baada ya matengenezo. Barabara ya Gando mwaka mmoja au miaka miwili lakini sasa hivi barabara ile ni mbaya.

Mhe. Mwenyekiti, najua Wizara inachukua hatua nzuri sana na naipongeza kwa hilo wala siwezi kuilaumu kwa sababu wanafanya jitihada hizo, lakini kama alivyosema Mhe. Nadir Abdulatif anapokuja kiongozi wasitie fusi ili kuficha yale mashimo au zile athari waache kiongozi yule anapokuja ajue kwamba barabara hii imeathirika vipi ili ajue la kufanya, sio wakazibe fusi kwa sababu kiongozi anapita. Mimi niseme waache vile vile kiongozi anayepita kukagua ajue athari iliyotokea kwenye barabara na ndiyo wafanye matengenezo au marekebisho.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye barabara zetu ambazo zipo katika Kijiji cha Chaani na kijiji cha Chozi. Nimwambie Mhe. Waziri barabara hizi ni mbaya tena ni mbaya sana, wengefanya utaratibu wao barabara zile kuziwekea angalau fusi. Barabara ni refu na ni kubwa kama Mwakilishi siwezi nikazimudu barabara zile bila ya kuingia nyinyi watu wa Wizara ya Mawasiliano. Nawaomba kwa heshima zote mjitahidi barabara zile mzifanyie matengenezo kwa hali ya juu.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye Bandari, ni siku nyingi sana kulisema suala hili la Bandari ya Wete. Mkoa wa Kaskazini Pemba ndiyo Mkoa ambao una wafanyabiashara wengi, ndizi tunazokula Unguja ni kutoka Mkoa wa Kaskazini Pemba, mihogo tunayokula na kila kitu cha matunda unachokijua kinatoka Mkoa wa Kaskazini Pemba. Naiomba Wizara kwenye bajeti iliyopita walitwambia kwamba tayari wameshaongea na mkandarasi ili kuitengeneza Bandari ile ya Wete, lakini hadi sasa hatujapata jawabu lolote. Mimi nataka kujua ni hatua gani iliyofanyika hadi kufikia leo, hatujapata jawabu lolote kwamba bandari hii inafanyiwa matengenezo ama inajengwa au tayari mkandarasi ameshaanza kujenga. Nataka jawabu.

Mhe. Mwenyekiti, nizungumzie suala la fidia kwa sababu na mimi inaniuma sana watu wangu wa Gando hadi hii leo, barabara

nyengine zinajengwa watu wanalipwa fidia lakini wao hawajamaliziwa kulipwa fidia. Najua kwamba hili suala limeshazungumzwa sana. Najua kwamba Mhe. Rais anajua lakini nataka nijue Mhe. Waziri anambie ni lini wananchi wangu wa jimbo la Gando waliokuwa hawajamaliziwa fidiwa watalipwa lini kwa sababu wengi wao ni masikini na ndiyo hao wenye hivyo vijumba vya udongo kwa hivyo walipwe.

Baada ya hayo naona muda umeshamaliza naiyunga mkono hotuba hii kwa asilimia 90 mengineyo mpaka nijibiwe.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mariyam, Waheshimiwa Wajumbe naomba niwatangazie ambao watakaokuwa wachangiaji wa kesho. Waheshimiwa Wajumbe muda uliobakia ni mdogo na kulingana na saa ilivyo pamoja na matatizo iliyonayo, naomba niwatangaze Wajumbe watakaochangia nao ni Mhe. Hassan Khamis Hafidh atakuwa ni mchangiaji wa mwanzo kesho asubuhi tukijaaliwa, Mhe. Abdalla Ali Kombo, Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa) na Mhe. Miraji Khamis Mussa, ndiyo watakaokuwa wachangiaji wa mwanzo kesho tukijaaliwa.

Baada ya hapo nichukue fursa hii kuwashukuru nyote na kuwapongeza kwa utulivu wengu na michangio mizuri ambayo inatoka kwa Waziri ni imani yangu kwamba atajiandaa vyema kwa ajili kutoa hoja zilizokuwa nzuri. Kesho tukijaaliwa ndiyo bajeti hii tunaipitisha.

Baada ya muda huu sasa naomba niliakhirishe Baraza hadi kesho saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 9:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 1/6/2017 saa 3:00 za asubuhi)